**LINDI MWAMBAO COOPERATIVE UNION LTD**

REG. NO: AFF-LND-LND-MC-2023-24

P.O.BOX 140, LINDI

**Email:lindimwambaocoopunion@yahoo.com**

# MPANGO MKAKATI WA MIAKA MITANO

# (2026/27 hadi 2030/31)

**Mawasiliano**

Meneja Mkuu

Lindi Mwambao Cooperative Union (LMCU) Ltd

S.L.P 140 Lindi, Tanzania

Simu : (+255) 685 543 131

Baruapepe: lindimwambaocoopunion@yahoo.com

**Februari, 2026**

**YALIYOMO**

YALIYOMO ..... ii
NENO LA MWENYEKITI WA CHAMA ..... v
NENO LA MENEJA MKUU WA CHAMA ..... vi
MUHTASARI WA MPANGO MKAKATI ..... vii
ORODHA YA MAJEDWALI ..... viii
ORODHA YA MAUMBO ..... ix
VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA ..... x
VIAMBATANISHO ..... xii
WAJUMBE WA BODI YA LMCU LTD ..... xiii
WATENDAJI WA NGAZI ZA JUU WA LMCU LTD ..... xiv
UIDHINISHAJI ..... xv
TAFSIRI YA MANENO YA MSINGI ..... xvi
SURA YA KWANZA ..... 1
UTANGULIZI ..... 1
1.1 Historia Fupi ya Ushirika Nchini ..... 1
1.2 Historia Fupi ya Chama ..... 4
1.3 Malengo ya Chama ..... 5
1.4 Umuhimu wa Mpango Mkakati ..... 6
1.5 Mpangilio wa Mpango Mkakati ..... 7
1.6 Mchakato na Mbinu za Uandaaji wa Mpango Mkakati ..... 8
SURA YA PILI ..... 9
UCHAMBUZI WA HALI YA CHAMA ..... 9
2.1 Mambo Tunayojivunia ..... 9
2.2 Mambo Tuliyojifunza ..... 10
2.4 Muundo wa Utawala na Mifumo ya Uendeshaji ..... 12
2.5 Tathmini ya Maendeleo ya Chama kwa Miaka Mitano Iliyopita ..... 13
2.6 Tathmini ya Kifedha ya Chama ..... 20
2.7 Uchambuzi wa Mazingira ya Chama ..... 22

2.7.1 Uchambuzi wa UMAFUCHA (SWOC Analysis) ....................22
2.7.2 Uchambuzi wa Mazingira ya Makuu ya Kibiashara (CoopPESTEL Analysis) ....................29
2.8 Uchambuzi wa Wadau wa Chama na Kujenga Mahusino ....................34
2.9 Uchambuzi wa Vihatarishi na Mpango wa Udhibiti ....................40
MPANGO WA CHAMA KATIKA MIAKA MITANO IJAYO (2026/27 – 2030/31) ....................50
3.1 Tamko la Dira ....................50
3.2 Tamko la Dhamira ....................50
3.3 Kauli Mbiu ....................50
3.4 Maadili ....................50
3.5 Kanuni za Misingi za Chama ....................51
3.6 Kanuni za Kimenejimenti Zitakazofuatwa ....................52
3.7 Vipaumbele vya Mpango Mkakati ....................52
3.8 Nguzo za Uandaaji wa Mpango Mkakati ....................69
3.9 Madhanio ya Msingi Kuhusu Utekelezaji wa Mpango Mkakati ....................70
SURA YA NNE ....................72
MPANGO WA UTEKELEZAJI ....................72
4.1 Mfumo wa Utekelezaji ....................72
4.2 Mpango wa Utekelezaji ....................73
4.3 Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Shughuli za Kimkakati ....................73
4.4 Wajibu wa Wadau wa Chama Katika Utekelezaji ....................73
4.5 Kugharamia Utekelezaji wa Mpango Mkakati ....................74
4.6 Maboresho ya Mpango Mkakati ....................74
SURA YA TANO ....................75
UFUATILIAJI NA TATHMINI ....................75
5.1 Malengo ya Ufuatiliaji na Tathmini ....................75
5.2 Ufuatiliaji ....................75
5.3 Tathmini ....................75
5.4 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ....................76
5.5 Matumizi ya Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini ....................77

SURA YA SITA ....................78
MABADILIKO KATIKA MUUNDO WA CHAMA ....................78
6.1 Mahitaji ya Rasilimali Watu na Sifa Husika ....................78
6.2 Mapendekezo ya Idara na Vitengo ....................79
6.3 Mapendekezo ya Mabadiliko ya Muundo wa Chama ....................80
VIAMBATANISHO ....................82

## NENO LA MWENYEKITI WA CHAMA

Ninayo furaha kuona Chama chetu kimefikia hatua hii ya kuwa na Mpango Mkakati. Ni jambo la heri na la kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima na afya hata kuweza kutekeleza jambo hili. Ni mafanikio makubwa kwa Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao Ltd. Tunashukuru pia kwa uwepo wa hali ya amani na utulivu katika nchi yetu hata tunaweza kupanga na kutekeleza mipango na shughuli zetu kwa kujiamini. Tunaamini kuwa juhudi zetu zitaendelea kuleta matokeo makubwa ikiwemo kuimarisha Uchumi wa Chama, Wanachama, wakulima wetu na kusaidia pia maendeleo ya taifa letu. Nachukua nafasi hii kutoa pongezi nyingi kwa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna inavyoendelea kuweka mazingira mazuri yanayowezesha uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika nchini.

Nawashukuru sana wadau mbalimbali waliotuunga mkono katika zoezi zima la kuandaa Mpango Mkakati wa Chama chetu wa miaka mitano ijayo (2026/27 hadi 2030/31). Kila mmoja kwa nafasi yake alitoa muda wake, uzoefu na maoni muhimu yaliyotuwezesha sisi kuandaa Mpango Mkakati huu. Sasa tunao mwongozo sahihi unaotuwezesha kupanga na kutekeleza shughuli zetu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Naanza kwa kuwashukuru sana Wanachama wetu, wajumbe wenzangu wa Bodi na Watendaji wa Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao Ltd kwa jinsi walivyoshiriki kikamilifu kuwezesha maandalizi ya Mpango Mkakati wetu.

Kwa niaba ya Chama, natumia nafasi hii pia kuwashukuru wadau mbalimbali kutoka nje ya Chama ambao wameshirikiana nasi wakati wa kuandaa Mpango Mkakati huu na hata shughuli nyingine za maendeleo ya Chama. Katika hili, tunamshukuru sana Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Lindi na Maafisa Ushirika wote wa eneo la Chama chetu. Tunakishukuru sana Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU)-Ofisi ya Mkoa ya Mtwara na Lindi na Shirika la Ukaguzi wa Hesabu za Vyama vya Ushirika na Usimamizi (COASCO). Shukrani zetu pia ziende kwa wadau wengine wakiwemo; Mrajis wa Vyama vya Ushirika Tanzania, Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Naliendele, Bodi ya Stakabadhi za Ghala (WRRB), Shirika la Bidhaa Tanzania (TMX), Mradi wa Pamoja wa Vyama Vikuu vya Korosho (KCJE Ltd) na wadau wengine. Mungu awabariki sana.

**Ushirika, Pamoja Tujenge Uchumi**

………………………

**Mwenyekiti**

**Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao (LMCU) Ltd**

## NENO LA MENEJA MKUU WA CHAMA

Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwamabo (LMCU) Ltd kimeanza kufanya shughuli zake rasmi tangu mwaka 2018. Kwa miaka hii michache tunajivunia kwamba tumeweza kufanya mambo mbalimbali ya kimaendeleo kwa manufaa ya Wanachama na wakulima wetu walioko katika Halmashauri za Kilwa, Lindi Manispaa na Mtama. Pamoja na mafanikio mbalimbali tuliyopata tangu Chama chetu kianze, hatukuwahi kuandaa Mpango Mkakati rasmi wa kuongoza shughuli za maendeleo ya Chama. Kwa hiyo ninayo furaha kuwa tumefanikiwa kuandaa Mpango Mkakati huu uliobeba vipaumbele mbalimbali vya Chama chetu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo (2026/27 hadi 2030/31). Ni imani yetu kubwa kuwa, uwepo wa Mpango Mkakati huu utawawezesha wajumbe wa Bodi, Watendaji, Wanachama, Wakulima na wadau wengine kubaini wajibu wao na kukuza ushirikiano ili tufanikishe malengo, mikakati na shabaha zetu za kimaendeleo.

Kupitia Mpango Mkakati huu tutaweza kupanga vizuri shughuli za Chama na kuzitekeleza, kufuatilia na kutathmini mafaniko yake. Tunaweza pia kukuza ufanisi ikiwemo kuwa na matumizi mazuri ya rasilimali zetu. Utekelezaji wa Mpango Mkakati huu utakifaidisha Chama, Wanachama, wakulima, jamii na hata taifa letu. Tumeweza kuandaa dira yetu ya kutuongoza pamoja na dhamira, malengo na mikakati mahsusi itakayotekelezwa. Haya yatasaidia kutupa mwongozo katika usimamizi na uendeshaji wa shughuli zetu. Tumeweza pia kuchambua hali yetu ndani na nje ya Chama, wadau wakushirikiana nao katika utekelezaji, rasilimali zinazohitajika, mpango wa utekelezaji na kubaini vihatarishi tarajiwa na udhibiti wake. Mpango Mkakati huu utatuwezesha pia kubaini mahitaji ya rasilimali muhimu ili kufanikisha utekelezaji wa mipango yetu. Mpango Mkakati wetu umebeba jumla ya vipaumbele tisa (9) vitakavyotekelezwa na Chama katika miaka mitano ijayo.

Tunaamini kuwa wadau wote wa ndani wa Chama (wajumbe wa Bodi, watendaji na Wanachama), wakulima na wadau wengine watashiriki ipasavyo kuhakikisha kuwa tunafanikisha malengo, mikakati na shabaha tulizojiwekea. Hakika tutafikia pale tunapotamani kufika kwa kuwa sasa tuna mwongozo sahihi wa maendeleo ya Chama chetu hivyo kuongeza uwajibikaji na ufanisi. Mpango Mkakati huu ni kama ukurasa mpya kwa Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao (LMCU) Ltd. Mungu atusaidie.

**Ushirika ni Biashara**

………………………

**Meneja Mkuu**

**Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao (LMCU) Ltd**

## MUHTASARI WA MPANGO MKAKATI

Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao (LMCU) Ltd ni Chama kilichoko katika Mkoa wa Lindi. Chama hiki kilianzishwa baada ya kugawanyika kwa Chama Kikuu cha Ushirika Ilulu mwaka 2014 ambacho kilikuwa kikihudumia Mkoa mzima wa Lindi. LMCU Ltd ilianza kufanya shughuli zake ikiwa kama Kamati ya Muda kuanzia mwaka 2014 na kupata usajili rasmi mwaka 2018 chini ya Sheria Na. 6 ya mwaka 2013 na Kanuni za Vyama vya Ushirika za 2015. Chama kinafanya shughuli zake katika Halmashauri tatu (3) ambazo ni; Kilwa, Lindi Manispaa na Mtama. Hadi Februari 2026, Chama kilikuwa na jumla ya Wanachama (AMCOS) 61. Chama kinatoa huduma mbalimbali kwa wanachama wake kama vile; kuratibu upatikanaji wa pembejeo, kutoa huduma za ugani, kusafirisha na kuhifadhi mazao, kusimamia miradi na mali za Chama, kusimamia mauzo na malipo ya wakulima, kutoa elimu na mafunzo na kusaidia huduma za kijamii. LMCU Ltd inatambua kuwa ni lazima ijiendeshe kimkakati kwa kuwa na mipango rasmi mizuri itakayoongoza utekelezaji wa shughuli zake kwa kuzingatia vipaumbele na rasilimali zake ili kuwanufaisha Wanachama na wakulima. Hivyo Chama kimeandaa Mpango Mkakati huu ili kuongoza utekelezaji na usimamizi wa shughuli zake kwa kipindi cha miaka mitano ijayo (2026/27 hadi 2030/31). Katika Mpango Mkakati huu, maono (dira) ya Chama ni "Kuwa Chama Kikuu kinachoaminika katika kuwezesha maendeleo endelevu ya Wanachama na Wakulima kupitia kilimo cha kibiashara". Dhamira/Dhima ya Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao Ltd ni "kuwaendeleza Wanachama na Wakulima ili kustawi kiuchumi na kijamii kupitia huduma bora, usimamizi mzuri, ubunifu na uwekezaji wa kimkakati katika sekta ya kilimo". Katika miaka mitano ya Mpango Mkakati huu, Chama kinalenga kutekeleza jumla ya vipaumbele tisa (9). Vipaumbele hivi ni; Uanachama; Usimamizi wa huduma; Uzalishaji na ubora wa mazao; Masoko na uhusiano na wadau; Usimamizi endelevu wa miradi na uwekezaji; Usimamizi wa fedha na mali; Uongozi, utawala bora na menejimenti ya rasilimali watu; Matumizi endelevu ya TEHAMA; na Utunzaji wa mazingira asilia na kujali jamii. Chama kitakuwa kikiandaa mipango kazi ya mwaka ili kuiongoza Bodi na Menejimenti kutekeleza vyema Mpango Mkakati huu na kuweka mfumo wa ufuatiliaji na kupima ufanisi. Pia Chama kitaendelea kuandaa sera na mipango mingine midogo midogo kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa Mpango Mkakati huu. Bodi, Menejimenti na Wanachama watakuwa wakifanya maboresho ya Mpango Mkakati huu wakati wowote wakiona inafaa kufanya hivyo. Chama kinatarajia kuwa kwa miaka yote ya utekelezaji kutakuwa na ushirikiano mzuri kutoka kwa wadau na kutakuwa na rasilimali za kutosha kutekeleza Mpango Mkakati huu.

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Korosho, Ufuta na Mbaazi kwa Msimu wa 2021/22 hadi 2025/26 .........15

Jedwali Na. 2: Makusanyo na Mauzo ya Mazao ya Kibiashara Kipindi cha 2021/22 hadi 2025/26.....17

Jedwali Na. 3: Bei za Korosho na Ufuta kwa Mwaka 2021/22 hadi 2025/26 ........................................17

Jedwali Na. 4: Madaraja ya Ubora Iliyouzwa Mwaka 2021/22 na 2025/26...........................................18

Jedwali Na. 5: Huduma za Kijamii Zilizotolewa Mwaka 2021/22 na 2025/26 .....................................19

Jedwali Na. 6: Hali ya Kifedha ya Chama kwa Kipindi cha 2020/21 hadi 2024/25 ..............................20

Jedwali Na. 7: Mapato na Matumizi ya Chama kwa kipindi cha 2020/21 hadi 2024/25 .......................21

Jedwali Na. 8: Uchambuzi wa Uwezo, Madhaifu, Fursa na Changamoto katika Chama ......................23

Jedwali Na. 9: Uchambuzi wa Wadau Muhimu wa Chama ...................................................................35

Jedwali Na. 10: Vihatarishi katika Utekelezaji wa Mpango Mkakati ...................................................40

Jedwali Na. 11: Mpango wa Udhibiti wa Vihatarishi ............................................................................42

Jedwali Na. 12: Maadili ya Chama katika Kutekeleza Mpango Mkakati...............................................50

Jedwali Na. 13: Mahitaji na Sifa za Watendaji Wapya ..........................................................................78

## ORODHA YA MAUMBO


Umbo Na. 1: Mihimili Muhimu katika Muundo wa Utawala wa Chama ............................................13

Umbo Na. 2: Ongezeko la Wanachama wa LMCU Ltd kufikia 2025/26..............................................14

Umbo Na. 3: Ukuaji wa Hisa kwa Kipindi cha Mwaka 2020/21 hadi 2023/24 ....................................15

Umbo Na. 4: Mapendekezo ya Muundo Mpya wa Utawala wa LMCU Ltd..........................................81

## VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

| | |
|---|---|
| AAACO | Alliance Africa Agricultural Cooperatives Organization |
| AMCOS | Agricultural Marketing Co-operatives Societies |
| CBT | Cashewnut Board of Tanzania |
| COASCO | Co-operative Audit and Supervision Corporation |
| COPRA | Cereals and Other Produce Regulatory Authority |
| ICA | International Co-operative Alliance |
| KCJE | Korosho Cooperative Joint Enterprise Ltd |
| LMCU | Lindi Mwambao Cooperative Union |
| MK | Mkakati |
| MoCU | Moshi Co-operative University |
| MUVU | Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika |
| NEMC | National Environmental Management Council |
| RUNALI | Ruangwa, Nachingwea na Liwale |
| SACCOS | Savings and Credit Co-operative Society |
| TADB | Tanzania Agriculture Development Bank |
| TANESCO | Tanzania Electric Supply Company |
| TARI | Tanzania Agriculture Research Institute |
| TARURA | Tanzania Rural Roads Agency |
| TBS | Tanzania Bureau of Standards |
| TCDC | Tanzania Co-operative Development Commission |
| TFC | Tanzania Federation of Cooperatives |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TMX | Tanzania Mercantile Exchange |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| TZS | Tanzania Shillings |
| UMAFUCHA | Uwezo, Madhaifu, Fursa na Changamoto |
| USTAJaSU | Ushirika, Siasa, Teknolojia, Asilia, Jamii, Sheria na Uchumi |
| UVIKO-19 | Ugonjwa wa Virusi vya Korona-19 |
| WMA | Weights and Measures Agency |

| | |
|---|---|
| WRRB | Warehouse Receipts Regulatory Board |

## VIAMBATANISHO

Kiambatanisho Na. 1: Mpango wa Utekelezaji wa Miaka Mitano ........................................................82
Kiambatanisho Na. 2: Muundo wa Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Shughuli za Kimkakati ............122
Kiambatanisho Na. 3: Majina ya Wadau Walioshiriki Katika Kuandaa Mpango Mkakati..................123
Kiambatanisho Na. 4: Majina ya Wajumbe wa Bodi wa Chama ........................................................123
Kiambatanisho Na. 5: Majina ya Watendaji wa Chama .......................................................................124

## WAJUMBE WA BODI YA LMCU LTD



**Ismail M. Nalinga**
**Mwenyekiti**



**Hassan M. Mnumbe**
**Makamu Mwenyekiti**



**Issa A. Baraka**
**Mjumbe wa Bodi**



**Said M. Shahame**
**Mjumbe wa Bodi**



**Juma A. Issa**
**Mjumbe wa Bodi**



**Hawa A. Mbundu**
**Mjumbe wa Bodi**



**Rashidi H. Masudi**
**Mjumbe wa Bodi**

## WATENDAJI WA NGAZI ZA JUU WA LMCU LTD



**Nurdin S. Swallah**
**Meneja Mkuu**



**Lisa E. Mgonja**
**Mhasibu Mkuu**



**Bakari S. Saidi**
**Mkaguzi wa Ndani**



**Hassan S. Dossa**
**Afisa Manunuzi**



**Glory I. Makere**
**Afisa Masoko na Uhamasishaji**

## UIDHINISHAJI

Sisi tuliosaini, tunaidhinisha yaliyomo na tuko tayari kushirikiana kutekeleza Mpango Mkakati huu.

1. Jina: ______________________________________________

   Cheo:______________________________________________

   Tarehe:_____________________________________________

2. Jina: ______________________________________________

   Cheo:______________________________________________

   Tarehe:_____________________________________________

3. Jina: ______________________________________________

   Cheo:______________________________________________

   Tarehe:_____________________________________________

**MPANGO MKAKATI HUU UMESAJILIWA NA:**

4. Jina: ______________________________________________

   Cheo:______________________________________________

   Tarehe:_____________________________________________

## TAFSIRI YA MANENO YA MSINGI

| | |
|---|---|
| Afisa Ugani Mkulima | Humaanisha mkulima aliyepata mafunzo ya kilimo bora cha mazao mbalimbali ya kibiashara yanayohusiana na Chama ili kuwahudumia wakulima wengine katika eneo lake kwa elimu, taarifa na ushauri wa kilimo |
| Chama | Humaanisha Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao Ltd yaani Lindi Mwambao Cooperative Union (LMCU) Ltd |
| Eneo la Chama | Humaanisha eneo ambalo Chama kinaendesha shughuli zake na ndio mahali Wanachama na wakulima wanakotokea na kuendesha shughuli zao, yaani Halmashauri za Kilwa, Lindi Manispaa na Mtama |
| Mazao ya kibiashara | Humaanisha mazao yote yaliyobainishwa katika Masharti ya Chama ambayo huzalishwa na wakulima na Wanachama na kuuzwa kupitia Chama. Mazao haya ni pamoja na; korosho, ufuta, mbaazi na mazao mengine yatakayokubaliwa na Mkutano Mkuu wa Wanachama. |
| Mkutano Mkuu | Humaanisha Mkutano Mkuu wa LMCU Ltd |
| Ofisi ya Kanda | Humaanisha Ofisi ndogo ya LMCU Ltd iliyoanzishwa katika eneo la Chama ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa Wanachama na Wakulima na majukumu mengine ya Chama |
| Wadau wa Ndani | Humaanisha watu wote walioko ndani ya Chama wanaounda mihimili mikuu ya Chama, yaani Mkutano Mkuu, Bodi na Menejimenti (Watendaji) |
| Wadau wa Nje | Humaanisha mtu/watu au taasisi muhimu kutoka sekta binafsi na Serikali ambao hufanya kazi na Chama katika mambo mbalimbali kwa namna tofauti tofauti |
| Wanachama | Humaanisha Vyama vya Msingi vya Ushirika vya Kilimo na Masoko (AMCOS) ambavyo huunda Chama |
| Wakulima | Humaanisha watu wote ambao ni Wanachama wa Vyama vya Msingi vya Ushirika vya Kilimo na Masoko (AMCOS) na wale wasiojiunga uanachama, ambao wote hujihusisha na uzalishaji wa mazao ya korosho, ufuta, mbaazi na mazao mengine ya kibiashara na huhudumiwa na Wanachama na Chama |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Historia Fupi ya Ushirika Nchini

Ushirika hapa kwetu Tanzania una historia ndefu inayoanzia tangu enzi za utawala wa kikoloni. Historia hii inaanzia mkoani wa Kilimanjaro ambapo Wakulima wa zao la kahawa walibaini haja ya kuunda umoja wao ili kutetea na kulinda maslahi yao pamoja na kupata huduma za msingi. Hii ilipelekea kuundwa kwa Chama cha kwanza cha wakulima mwaka 1925 kilichojulikana kama Kilimanjaro Native Planters Association (KNPA). Kwa ujumla KNPA ilianzishwa kwa lengo la kutetea maslahi ya wakulima wadogo wa kahawa na kuwawezesha kupata huduma za; ugani, masoko, elimu, pembejeo na nyingine kwa lengo la kuinua uchumi wao. Serikali ya kikoloni ilibaini ukuaji wa wa Vyama vya Wakulima hivyo ikatunga Sheria ya Vyama vya Ushirika iliyojulikana kama Co-operative Society Ordinance mwaka 1932.

Vyama vya Ushirika vilipoongezeka mkoani Kilimanjaro na mabadiliko hayo ya kisheria ilisababisha kuungana kwa Vyama vya Wakulima hivyo KNPA ilibadilishwa na kuundwa Chama Kikuu cha Ushirika kilichojulikana kama Kilimanjaro Native Cooperative Union (KNCU) Ltd mwaka 1933. KNCU Ltd ilijihusisha na mambo ya jamii na kuboresha hali za kiuchumi kwa Wanachama wake kwa kulinda maslahi yao ikiwemo kupata masoko ya uhakika na bei nzuri ya kahawa, kutoa elimu na mafunzo, kuwezesha upatikanaji wa pembejeo, kuongeza uzalishaji na huduma nyingine. Kwa ujumla, KNCU Ltd kilikuwa Chama Kikuu cha Ushirika cha mfano kilichohamasisha uanzishaji wa Vyama vya Ushirika maeneo mengine nchini. Mnamo mwaka 1936 Vyama vitatu (3) vya Ushirika wa tumbaku huko Songea viliungana kuunda Chama Kikuu cha Ushirika cha Ngoni-Matengo (*Ngoni-Matengo Cooperative Union*).

Katika kipindi cha miaka ya 1940 hadi 1950, Vyama Vikuu vingine viliundwa na kusajiliwa. Baadhi ya Vyama hivyo ni pamoja na; Chama Kikuu cha Ushirika cha Bugufi yaani Bugufi Cooperative Union Ltd wilayani Ngara na Chama cha Wakulima wa Kahawa Mwakaleli (Mwakaleli Coffee Growers Association) huko Rungwe ambacho baadae kiliitwa Rungwe African Cooperative Union (RACU) Ltd. Vyama vingine vilikuwa ni Chama Kikuu cha Ushirika Bukoba yaani Bukoba Native Cooperative Union (BNCU) Ltd Wilaya ya Bukoba na Chama cha Wakulima wa pamba maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria (Lake Province Growers Association) ambacho baadae kiliitwa Victoria Federation of Cooperative Unions (VFCU) Ltd.

Miezi michache kabla ya Tanganyika kujipatia uhuru, mwezi Novemba 1961 ndipo Shirikisho la Vyama vya Ushirika lililojulikana kama Cooperative Union of Tanganyika (CUT) lilianzishwa. Lengo kuu la CUT lilikuwa ni kusimamia Vyama vyote vya Ushirika nchini. Baadhi ya majukumu ya CUT yalikuwa kutoa huduma za kiusimamizi na uhasibu, msaada wa kisheria pamoja na kuandaa na kusambaza machapisho mbalimbali ya ushirika. Mwaka 1962, Benki ya Ushirika ya Tanganyika yaani The Cooperative Bank of Tanganyika (CBT) ilianzishwa. Ilipofika mwaka 1963 Serikali ilianzisha Chuo cha Ushirika Moshi (Cooperative College Moshi) kwa lengo la; kufundisha watalaam kwa ajili ya Vyama Vikuu, kusimamia mfuko wa ukaguzi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika na wadau wengine wa Ushirika. Chuo pia kilipewa jukumu la kuandika na kuchapisha maandiko mbalimbali kwa ajili ya kutolea elimu na mafunzo ya ushirika.

Mabadiliko mengine katika ushirika yalitokea mwaka 1964 ambapo Vyama 18 vya Akiba na Mikopo (SACCOS) viliungana na kuunda Shirikisho la Vyama Vya Ushirika vya Akiba na Mikopo yaani Savings and Credit Cooperative Union League of Tanzania (SCCULT). Majukumu ya SCCULT yalikuwa ni pamoja na; kutoa elimu na mafunzo ya ushirika kwa Wanachama, kuandika na kuchapisha maandiko ya ushirika na pia kuwa wakala wa bima kwa Vyama vya Ushirika. Mwaka huo huo wa 1964, benki ya kitaifa ya Ushirika yaani National Cooperative Bank (NCB) ilianzishwa hivyo kuchukua ya iliyokuwa Benki ya Ushirika ya Tanganyika (CBT). Benki hii ilijihusisha na utoaji wa mikopo kwa Vyama vya Ushirika ili kununua mazao ya Wanachama.

Mwaka 1967, Azimio la Arusha liliundwa kwa ajili ya kujenga viongozi waadilifu na kumilikisha uchumi kwa Wananchi. Hili lilitekelezwa pia kupitia Vyama vya Ushirika. Hadi mwaka 1968, Tanzania ilikuwa ndio nchi yenye vuguvugu la ushirika kubwa na imara zaidi barani Afrika. Mwaka huo pia kulitungwa Sheria ya kwanza ya Vyama vya Ushirika baada ya uhuru (The Cooperative Socieities Act of 1968) ambayo pamoja na mambo mengine ilihimiza uanzishaji wa Vyama Vikuu vya Ushirika ngazi za mikoa. Benki ya Ushirika (NCB) ilikuja kubadilishwa na kuwa Benki ya Taifa ya Maendeleo Vijijini mwaka 1972 yaani Tanzania Rural Development Bank (TRDB). Serikali ilitunga Sheria ya Vijiji na Ujamaa mwaka 1975 (Ujamaa and Villagization Act). Katika kutekeleza Sheria hiyo, mwaka 1976 Serikali ilivunja Vyama vyote vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) vilivyoko maeneo ya vijijini pamoja na Vyama Vikuu. Baada ya kuvunjwa, vijiji vyote vilipewa kazi ya kufanya majukumu yaliyokuwa ya AMCOS na shughuli za Vyama Vikuu zilichukuliwa na Mamlaka za Mazao, Mashirika ya Biashara ya Mikoa, Mashirika ya Maendeleo ya Wilaya na ya kitaifa.

Kutokana na malalamiko ya wadau wa ushirika na Serikali kutambua umuhimu wa Vyama vya Ushirika ilitunga upya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 14 ya mwaka 1982 na kuvirudisha rasmi Vyama vya Ushirika mwaka 1984. Pia Benki ya Taifa ya Maendeleo Vijijini (TRDB) ilibadilishwa mwaka 1984 ili kuhudumia na Vyama vya Ushirika hivyo ikaitwa Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini yaani Cooperative and Rural Development Bank (CRDB). Hata hivyo, pamoja na kuvirudisha Vyama na kutunga Sheria hiyo mpya, bado wadau wengi ikiwemo Vyama vya Ushirika hawakuridhishwa na utekelezaji wa Sheria hiyo. Mfano Vyama vya Msingi vya Ushirika vingi vilianzishwa bila upembuzi yakinifu wa hali ya kiuchumi (feasibility study). Hii ilisababisha kuanzishwa kwa Vyama vingi dhaifu na visivyo endelevu. Ili kukabiliana na hali hii, Serikali ilitunga Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika Na. 15 ya mwaka 1991. Sheria hii ilijaribu kutatua changamoto za Sheria ya 1982 na kutoa mamlaka zaidi kwa Vyama vya Ushirika kuamua mambo yao bila kuingiliwa sana na Serikali. Mkutano Mkuu ulipewa mamlaka kuwa chombo cha juu cha kufanya maamuzi ya mwisho kabisa katika Vyama vya Ushirika.

Baada ya kuja kwa mfumo wa soko huria nchini Tanzania hasa kuanzia miaka ya 1990, Vyama vingi vya Ushirika vilianza kuyumba kutokana na mabadiliko ya kiuchumi katika mifumo ya uzalishaji na masoko. Ushindani mkubwa katika soko huria ikiwemo wazalishaji binafsi wenye nguvu za mitaji na uzalishaji pamoja na masharti ya maendeleo kutoka kwa mashirika ya kimataifa na kupungua kwa jukumu la Serikali katika uendeshaji wa Vyama, vilifanya Vyama vya Ushirika kushindwa kuhimili ushindani. Mwaka 1996, Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini (CRDB) ilifanyiwa mabadiliko ya kiuendeshaji na kisha kubinafsishwa na kuwa CRDB Bank.

Mwaka 1997, Serikali ilitunga Sera ya kwanza ya Maendeleo ya Ushirika na kisha kuifanyia maboresho kwa kutunga Sera mpya mwaka 2002. Baadaye Serikali pia ilitunga Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 20 ya mwaka 2003 na Kanuni za Vyama vya Ushirika za mwaka 2004. Ilipofika mwaka 2013 ilitungwa Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na baadae Kanuni za Vyama vya Ushirika 2015. Maboresho ya Sheria yamefanyika pia mwaka 2025 kwa baadhi ya vifungu vya Sheria Na. 6 ya mwaka 2013. Chama Kikuu cha Ushirika LMCU Ltd ni sehemu ya historia ya ushirika nchini kwa kuwa ni zao la Chama Kikuu cha Ilulu kilichokuwepo hapo kabla na imeendelea na jukumu la kuendeleza ushirika katika eneo lake. Hivyo Chama kinatarajia kuendelea kuimarisha shughuli zake katika eneo lake, kuchochea maendeleo ya Wanachama na wakulima wake na hata kuchangia maendeleo ya tasnia ya ushirika kitaifa na kimataifa na kuchangia uchumi wa Tanzania.

## 1.2 Historia Fupi ya Chama

Mwanzo mkoa wa Lindi ulikuwa ukihudumiwa na Chama Kikuu cha Ushirika Ilulu yaani Ilulu Cooperative Union (ICU) Ltd. Mwaka 2014, Chama Kikuu cha Ushirika Ilulu Ltd kilikoma uhai wake hivyo kuwa chini ya Mfilisi. Baada ya ukomo huo, Vyama Vikuu viwili vikazaliwa mkoa wa Lindi. Vyama hivyo ni Chama Kikuu cha Ushirika RUNALI Ltd na Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao (LMCU) Ltd. Kwa upande wa LMCU Ltd, shughuli zake zilianza tangu tarehe 1 Oktoba mwaka 2014 baada ya Kamati ya Muda ya Uanzilishi ilipoundwa. Kamati hii ilisimamia shughuli za awali za kutoa huduma kwa Wanachama na kukamilisha taratibu za usajili. Tarehe 23 Machi, 2015 kulifanyika Mkutano Mkuu maaluma Wanachama ulioitishwa kwa lengo la kupitisha Masharti ya Chama na maandalizi ya usajili. Chama kilipata usajili wa muda wa miaka miwili ilipofika tarehe 31 Machi, 2017. Chama kilifanya Mkutano Mkuu wake wa kwanza tarehe 27 Septemba, 2017. Baada ya kutimiza vigezo, Chama kilipata usajili wake mnamo tarehe 19 Februari, 2018 na kupata namba ya usajili 5596.

Chama kilianza na Wanachama yaani Vyama vya Msingi vya Ushirika vya Kilimo na Masoko (AMCOS) 39 kati ya 40 vinavyolima korosho kwa kipindi hicho. Kulikuwa na AMCOS nyingine 11 zilizokuwa zinajihusisha na ufuta hazikujiunga na Chama kwa kuwa zao la ufuta halikuwepo kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani hadi ilipofika msimu wa 2018/19. Vyama hivyo vimeendelea kujiunga na Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao Ltd. Hadi kufikia Februari 2026, Chama kilikuwa na jumla ya Wanachama (AMCOS) 61. Wanachama wanatoka katika Halmashauri tatu (3) za Mkoa wa Lindi ambazo ni; Manispaaa ya Lindi, Mtama na Kilwa. Hadi sasa, AMCOS zote katika Chama zinajihusisha na zao la korosho. Kuanzia msimu wa mwaka 2018/19 Vyama hivyo pia vilianza kuzalisha na kuuza zao la ufuta na mbaazi. Makao makuu ya Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao yako Manispaa ya Lindi katika Kata ya Rasibula, mtaa wa Mitwero.

Kwa miaka yote Chama kimekuwa kikikaguliwa kila mwaka na Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (COASCO). Ili kuhakikisha kuwa shughuli zake zinaendeshwa vizuri, Chama kina Bodi yenye wajumbe saba (7) na watendaji kumi na sita (16) katika nafasi mbalimbali. Aidha Chama kimekuwa na uhusiano mzuri na wadau mbalimbali wa maendeleo ya Ushirika na Kilimo nchini. Chama pia ni mwanachama wa Shirikisho la Ushirika Tanzania (TFC) na Shirikisho la Vyama vya Ushirika vya Sekta ya Kilimo Africa (AAACO). Kwa nyakati mbalimbali, Chama pia kimekuwa kikishiriki makongamano na mikutano ya wadau wa Ushirika kimataifa ikiwemo ya Shirikisho la Ushirika Duniani (ICA). Chama kina matarajio makubwa kimaendeleo.

Bodi na Menejimenti ya Chama inayo imani kuwa kupitia Mpango Mkakati huu kitaweza kufikia mafanikio makubwa. Pia uwepo wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Bodi ya Korosho Tanzania, Mamlaka ya Udhibit wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Sera na Sheria ya Ushirika pamoja na taasisi wadau wanaofanya kazi na Chama vitasaidia uendelevu wa Chama. Aidha kupitia Mpango Mkakati huu, Chama kinataweza kuongeza uzalishaji wa korosho, ufuta na mbaazi (na mazao mengine) hatimaye kuinua hali za kiuchumi na kijamii kwa Wanachama, wakulima na jamii kwa ujumla hata uchumi wa nchi yetu. Mnamo tarehe 13 Januari 2023, Chama kilisajiliwa mpya wa kidigitali kwenye mfumo wa Usimimizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) na kupewa namba ya usajili AFF-LND-LND-MC-2023-24.

### 1.3 Malengo ya Chama

Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao (LMCU) Ltd kimeanzishwa kwa lengo la kuchochea na kuendeleza hali za kiuchumi na kijamii za Wanachama na wakulima katika eneo lake. Hii hufanyika kwa kupanga na kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni, misingi na taratibu za Vyama vya Ushirika nchini na duniani kwa ujumla. Hivyo, malengo maalum ya kuwepo kwa LMCU Ltd ni pamoja na;

(a) Kuratibu ukusanyaji, uhifadhi na utafutaji wa masoko ya korosho, ufuta, mbaazi na mazao mengine ya kibiashara kutoka kwa Wanachama na wakulima;

(b) Kununua, kuuza na kusambaza pembejeo na zana za kilimo kwa Wanachama na wakulima kwa bei nafuu na kuwapa huduma za ugani ili kuboresha uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula;

(c) Kutoa huduma za ushauri wa kitaalaam kwa Wanachama ikiwemo huduma za uhasibu na fedha, ushauri wa kibiashara, uandaaji wa sera na miongozo mbalimbali, mipango ya maendeleo, ukaguzi na huduma nyingine wanazohitaji;

(d) Kutoa elimu ya Ushirika, biashara na masuala mtambuka kwa Wanachama na wakulima na kuwaendeleza watendaji wa Chama kulingana na majukumu yao ili kukuza ufanisi na kuimarisha uchumi wa Chama, Wanachama na wakulima;

(e) Kumiliki, kukodi na kuendeleza ardhi, majengo na rasilimali nyingine kwa manufaa ya Chama, Wanachama na wakulima;

(f) Kubuni, kuanzisha, kusimamia na kuendeleza miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii kwa manufaa ya Wanachama, wakulima na jamii kwa ujumla;

(g) Kukodi, kununua na kuendesha mitambo na maghala ili kuweza kutoa huduma zinazohitajika na Wanachama na wakulima kwa shughuli za kilimo;

(h) Kusimamia vizuri fedha na mali za Chama kwa niaba ya Wanachama na kuhakikisha wananufaika na rasilimali hizo;

(i) Kuongeza thamani ya mazao mbalimbali yanayozalishwa na Wanachama na wakulima na kuyatafutia masoko ya uhakika ndani na nje ya Nchi; na

(j) Kufanya mambo mengine halali au ya lazima yenye manufaa kwa Wanachama na wakulima kwa kuzingatia Sera, Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika pamoja na miongozo mingine ya kitaifa na kimataifa.

## 1.4 Umuhimu wa Mpango Mkakati

Uwepo wa Mpango Mkakati ni muhimu katika kutoa mwongozo sahihi wa undeshaji na usimamizi wa Chama kimkakati. Mpango Mkakati huu wa miaka mitano unatoa mwongozo kwa LMCU Ltd kuhusu namna sahihi ya kupanga na kutekeleza shughuli mbalimbali kwa ufanisi na tija. Uandaaji wa Mpango Mkakati huu umezingatia vipaumbele mbalimbali vya maendeleo ambavyo Chama kitatekeleza katika kipindi cha mwaka 2026/27 hadi 2030/31. Mpango huu utakisaidia Chama kujiendesha kwa kuzingatia vipaumbele na malengo sahihi na kutumia vyema rasilimali zilizoko hivyo kufanikisha malengo na matamanio ya Wanachama na wakulima. Kwa ujumla, utekelezaji wa Mpango Mkakati huu utakinufaisha Chama kwa namna zifuatazo;

(a) Kubaini malengo, mikakati na shughuli muhimu zinazotakiwa kutekelezwa kwa wakati husika na rasilimali zinazotakiwa;

(b) Kuongeza ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa Chama kwa kupanga na kutekeleza malengo muhimu yanayoakisi vipaumbele na uwezo wa rasilimali;

(c) Kuimarisha nguvu ya Chama katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku kwa kuzingatia mikakati sahihi na shabaha zinazotekelezeka;

(d) Kuboresha mifumo ya uwajibikaji miongoni mwa Wanachama, Bodi na Menejimenti ya Chama pamoja na wadau wa nje hivyo kufanikisha malengo ya Chama;

(e) Kuwa na uwezo wa kutekeleza mipango ya maendeleo kwa wakati na kuimarisha uwezo wake kwa kukabiliana na ushindani;

(f) Kukiwezesha Chama kuwa endelevu na kutekeleza shughuli zake kwa miaka mingi;

(g) Kukiwezesha Chama kupata mwongozo wa jinsi ya kufuatilia na kutathmini malengo yake ya kimaendeleo; na

(h) Kutambua changamoto mbalimbali zinazoweza kutokea na vihatarishi tarajiwa hivyo kuweka mipango wa udhibiti.

### 1.5 Mpangilio wa Mpango Mkakati

Mpango Mkakati huu umeandaliwa kwa kuzingatia muundo wa kitaalam wa uandishi wa mipango mikakati ya taasisi za kibiashara. Kimuundo Mpango Mkakati huu una sura sita (6) zinazohusiana. Sura hizo ni;

- ❖ Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi: Sehemu hii inazungumzia kuhusu; historia fupi ya ushirika nchini, historia ya Chama, malengo ya Chama, umuhimu wa Mpango Mkakati, mpangilio wa Mpango Mkakati, Mchakato na mbinu za uandaaji.
- ❖ Sehemu ya Pili ni Uchambuzi wa Hali ya Chama: Sehemu hii imejikita katika kuelezea kuhusu; mambo ya kujivunia katika Chama, mambo ambayo Chama kimejifunza tangu kuanzishwa kwake, huduma za Chama, Muundo wa utawala na mifumo ya uendeshaji, tathmini ya maendeleo ya Chama kwa miaka mitano iliyopita, uchambuzi wa mazingira ya Chama, uchambuzi wa wadau pamoja na uchambuzi wa vihatarishi na udhibiti wake.
- ❖ Sehemu ya Tatu ni Mpango wa Chama kwa Miaka Mitano Ijayo: Sehemu hii inazungumzia kuhusu; tamko la dira na dhamira, kauli mbiu, maadili ya Chama, kanuni za Ushirika, kanuni za kimenejimenti, vipaumbele vya Mpango Mkakati, Mahusiano ya Mpango Mkakati na Sera, sheria na mipango mingine ya kitaifa na kimataifa (Nguzo za Mpango Mkakati), pamoja na madhanio ya msingi katika utekelezaji wa Mpango Mkakati.
- ❖ Sehemu ya Nne ni Mpango wa Utekelezaji: Sehemu hii inaelezea kuhusu; mfumo wa utekelezaji, mpango wa utekelezaji wa miaka mitano, mpango kazi wa mwaka, wajibu wa wadau katika utekelezaji, kugharamia Mpango Mkakati na maboresho ya Mpango Mkakati.
- ❖ Sehemu ya Tano ni Ufuatiliaji na Tathmini: Sehemu hii inaelezea kuhusu; malengo ya ufuatiliaji na tathmini, ufuatiliaji, tathmini, mfumo wa tathmini na ufuatiliaji na matumizi ya taarifa za ufuatiliaji na tathmini, na
- ❖ Sehemu ya Sita ni Mapendekezo ya Mabadiliko ya Muundo wa Chama: Sehemu hii inaelezea kuhusu; mahitaji ya rasilimali watu na sifa husika, mapendekezo ya vitengo na idara, na mapendekezo ya mabadiliko ya muundo wa utawala

## 1.6 Mchakato na Mbinu za Uandaaji wa Mpango Mkakati

Mpango Mkakati huu umeandaliwa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wa ndani na nje ya Chama. Ushiriki wao ndio umekiwezesha Chama kupata maoni na uzoefu wao uliowezesha kuandaa Mpango Mkakati huu. Wadau wa ndani wa Chama walioshiriki walikuwa ni; wajumbe wa Bodi, watendaji na wawakilishi wa Wanachama kutoka Kilwa, Lindi Manispaa na Mtama. Pia kulikuwa na ushiriki wa wadau wa nje ya Chama ambao ni pamoja na; Maafisa Ushirika (wa Kilwa, Lindi Manispaa na Mtama), Mwakilishi wa Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Lindi na Mratibu wa Programu Mkoa kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU)-Ofisi ya Mkoa ya Mtwara na Lindi. Jumla ya wadau ishirini na tano (25) kutoka ndani na nje ya Chama walishiriki

Shughuli za ukusanyaji wa data na maoni ya kuandaa Mpango Mkakati zilifanyika kwa muda wa siku nne (4). Siku tatu (3) zilitumika kufanya warsha ya wadau ili kukusanya maoni yao na siku moja (1) ilitumika kufanya rejea ya nyaraka mbalimbali za Chama (*desk review*). Katika siku ya kwanza, washiriki walipata mafunzo mafupi kuhusu dhana ya Mpango Mkakati ikiwemo; maana yake, umuhimu wake kwa Chama na muundo wa uandishi. Mafunzo yalilenga kuwapa washiriki uelewa wa kina ili waweze kushiriki kikamilifu katika kutoa maoni ya kuwezesha maandalizi ya mpango huu.

Kwa kila jambo husika, Mwezeshaji alianza kwa ufafanuzi wa malengo na matarajio kutoka kwa washiriki kisha kuwagawa katika vikundi vidogo vinne (4) ambapo walipewa kazi za kujadili mambo mbalimbali na kuyawasilisha. Baada ya mawasilisho, washiriki wote walijadiliana na kukubaliana kwa pamoja kuhusu mambo sahihi vya kujumuishwa katika Mpango Mkakati. Hivyo, kwa sehemu kubwa, ushiriki huu wa wadau ndio uliowezesha kuandaa Mpango Mkakati huu. Rasimu ya mpango iliandaliwa kisha kuwasilishwa kwenye warsha ya wadau ya siku mbili (2) kwa ajili ya mapitio yaani validation workshop. Wadau walipitia rasimu ya Mpango Mkakati na kisha kutoa maoni yao kuhusu mambo ya kuboresha na maoni hayo yalifanyiwa kazi.

Chama kiliwasilisha pia rasimu iliyoboreshwa kwa Wanachama katika Mkutano Mkuu wa Mwaka 2025/26. Wanachama waliipokea na kuukubali rasimu ya Mpango Mkakati huo, kisha ikapelekwa kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika kuidhinishwa. Baada ya haya yote, nyaraka rasmi ya Mpango Mkakati ilikamilika tayari kutumiwa na Chama katika miaka mitano ijayo (2026/27 hadi 2030/31).

# SURA YA PILI

# UCHAMBUZI WA HALI YA CHAMA

Sura hii ni msingi wa uandaaji wa mipango ya miaka mitano ijayo katika Chama. Uchambuzi wa hali ya Chama umefanyika ili kutambua hali iliyoko sasa na mambo gani ya kuboresha na mikakati sahihi ya kutekeleza. Sura hii imechambua mambo mbalimbali ikiwemo; mambo ambayo Chama kinajivunia (*best practices*) na yale ambayo kimejifunza kwa miaka yote ya uwepo wake (*lessons learnt*). Pia imechambua; huduma za Chama, muundo wa utawala, maendeleo ya Chama kwa miaka mitano (5) iliyopita, na uchambuzi wa mazingira ya Chama, wadau na vihatarishi. Uchambuzi wa haya yote umeoneshwa katika vipengele hapa chini.

## 2.1 Mambo Tunayojivunia

Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao Ltd kimeweza kupata uzoefu wa kutosha katika kuendesha shughuli zake baada ya kufanya kazi tangu mwaka 2018. Kwa miaka yote ya uwepo wake, Chama kinajivunia mambo yafuatayo;

(i) Chama kimeweza kufanikiwa kuratibu vyema utoaji wa huduma za msingi kwa Wanachama ikiwemo usambazaji wa pembejeo, vifungashio, uhifadhi na usafirishaji wa mazao pamoja na kutafuta masoko kwa manufaa ya Wanachama na wakulima na kuwalipa kwa wakati;

(ii) Chama kimeweza kumiliki mali mbalimbali ikiwemo ardhi, majengo (ofisi na maghala) na vyombo vya usafiri na kufanya uwekezaji katika taasisi mbalimbali za fedha;

(iii) Idadi ya Wanachama na Wakulima imekuwa ikiongezeka tangu Chama kuanzishwa na wamekuwa na imani kubwa na Chama chao;

(iv) Uwepo wa wakulima wengi wanaojihusisha na mazao ya kibiashara hivyo kutoa uhakika wa uendelevu wa Chama;

(v) Chama kimekuwa kikisaidia shughuli za maendeleo ya jamii katika Halmashauri zake hivyo kujenga taswira nzuri kwa jamii na wadau wake kwa ujumla;

(vi) Chama kimeweza kuaminiwa na wadau mbalimbali kutoka taasisi za Serikali na sekta binafsi hivyo kupata ushirikiano wa kutosha katika shughuli zake;

(vii) Chama kinafanya kazi eneo lenye ardhi kubwa inayofaa kwa shughuli za kilimo;

(viii) Chama kimekuwa na hali ya utulivu na uhusiano mzuri na wadau mbalimbali hivyo kufanikisha utekelezaji wa shughuli zake;

(ix) Chama kimekuwa na viongozi na watendaji wenye uwezo mzuri hivyo kufanikisha malengo mbalimbali ya Chama;

(x) Kwa miaka mingi Chama hakijakumbwa na migogoro mikubwa ya kuathiri utekelezaji wa mipango na shughuli zake; na

(xi) Chama kimewawezesha Wanachama kupata vitendea kazi muhimu ili kuwahudumia Wakulima.

Katika miaka mitano ya utekelezaji wa mpango mkakati huu, Chama kitaendelea kuzingatia mambo haya yote na kuboresha uendeshaji na usimamizi wa shughuli zake ili kufikia malengo yake.

## 2.2 Mambo Tuliyojifunza

Tangu kuanzishwa kwake, Chama pia kimejifunza mambo mbalimbali. Mambo hayo ni pamoja na yafuatayo;

(i) Kutoa huduma bora kwa Wanachama na wakulima kwa wakati huongeza uaminifu wao kwa Chama na kushiriki ipasavyo katika maendeleo ya Chama;

(ii) Uuzaji wa mazao kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani umekuwa mkombozi wa wakulima kwa kuwezesha upatikanaji wa masoko ya uhakika na kuinua kipato cha Wanachama na wakulima;

(iii) Bodi na watendaji ni lazima wawashirikishe Wanachama kabla ya kutekeleza jambo lolote na pia kuwapa mrejesho juu ya mambo yaliyotekelezwa ili kujenga imani, mshikamano na uwajibikaji na kufanikisha malengo ya Chama;

(iv) Uwajibikaji na ushirikiano miongoni mwa wajumbe wa Bodi, watendaji na Wanachama ni muhimu sana ili kukiwezesha Chama kufanikisha malengo mbalimbali ya kimaendeleo;

(v) Jitihada za kukuza uzalishaji wa mazao mbalimbali ni muhimu sana kwa Chama kuweza kufikia malengo yaliyowekwa;

(vi) Wajumbe wa Bodi na watendaji hutakiwa wakati wote kufanya kazi kwa weledi, kuzingatia misingi ya ushirika na utawala bora na kuwa wabunifu katika kusimamia na kuendesha shughuli za Chama hivyo kuleta utulivu, umoja na udhibiti migogoro;

(vii) Chama kinatakiwa kuendelea kutafuta masoko mbadala ya mazao mbalimbali ya wakulima na Wanachama na kuwekeza katika kuongeza thamani ili kupunguza utegemezi wa masoko yaliyoko;

(viii) Chama kinahitaji kuwa na mipango ya maendeleo na miongozo mbalimbali ili kuweza kufanya kazi kwa vipaumbele, kusimamia vyema rasilimali na kuongoza jinsi shughuli mbalimbali zitakavyofanyika na kuweka mfumo wa uwajibikaji;

(ix) Chama hutakiwa kuendelea kuimarisha uwezo wa Wajumbe wa Bodi, Watendaji, Wanachama na Wakulima ili kuimarisha ufanisi katika uendeshaji na usimamizi wa Chama;

(x) Chama hutakiwa kubuni na kusimamia vyanzo mbadala vya mapato ili kukuza mtaji wa ndani hivyo kuwa na uwezo zaidi kutoa huduma na kuwekeza katika vitega uchumi mbalimbali;

(xi) Chama kinahitaji kushirikiana kwa ukaribu na wadau wengine wa ushirika ili kukuza uwezo wa kutoa huduma kwa Wanachama, kujenga nguvu ya pamoja ya ushawishi kuhusu masuala yenye maslahi mapana kwa wana ushirika na kudhibiti muingiliano wa kisiasa; na

(xii) Matumizi ya TEHAMA katika Chama na Wanachama ni muhimu katika kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma na kupunguza gharama za uendeshaji.

Katika utekelezaji wa Mpango Mkakati huu, Chama kitaendelea kuzingatia mambo yote kiliyojifunza ili kufikia malengo yake. Pia Chama kitaendelea kujifunza mambo mengine zaidi yenye manufaa kutoka ndani na nje ya Chama kwa lengo la kuongeza ufanisi katika shughuli zake za kila siku.

## 2.3 Huduma za Chama

Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao Ltd kimeanzishwa kwa lengo la kutoa huduma mbalimbali zinazolenga kuchochea maendeleo ya Wanachamana na wakulima katika eneo lake la kazi. Baadhi ya huduma hizo ni pamoja na;

(a) Kuratibu upatikanaji na usambazaji wa pembejeo, vifungashio na zana za kilimo kwa Wanachama na wakulima;

(b) Kutoa huduma za ugani kwa wakulima;

(c) Kusimamia ukusanyaji wa mazao ya Wanachama na wakulima;

(d) Kusafirisha mazao na kuyahifadhi katika maghala;

(e) Kusimamia mauzo ya mazao na malipo ya wakulima na Wanachama;

(f) Kuwajengea uwezo viongozi na watendaji wa Chama na Wanachama ili kuimarisha ufanisi katika kuendesha na kusimamia shughuli za kila siku;

(g) Kuanzisha na kusimamia miradi mbalimbali au kufanya uwekezaji katika taasisi za kibiashara kwa niaba ya Wanachama;

(h) Kusimamia fedha na mali za Chama kwa niaba ya Wanachama; na

(i) Kutoa vitendea kazi muhimu na huduma za ushauri wa kitaalam kwa Wanachama ikiwemo uendeshaji na usimamizi wa Vyama

## 2.4 Muundo wa Utawala na Mifumo ya Uendeshaji

Muundo wa utawala wa LMCU Ltd umezingatia muundo ulioko kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika. Muundo huo unajumuisha mihimili mikuu mitatu (3) yaani; Mkutano Mkuu, Bodi ya Chama na Menejimenti (watendaji) kama ilivyooneshwa katika Umbo Na. 1. Wakati wa kutekeleza Mpango Mkakati huu, Chama kitaendelea kuzingatia muundo huo kwa mujibu wa Sheria. Kwa sasa Bodi ya Chama ina Wajumbe saba (7) waliochaguliwa na Mkutano Mkuu. Pia Chama kina jumla ya watendaji kumi na saba (17) ambao wako Makao Makuu ya Chama na Ofisi za Kanda.




**Umbo Na.1: Mihimili Muhimu katika Muundo wa Utawala wa Chama**

Mkutano Mkuu huundwa na Wanachama wa LMCU Ltd. Mkutano Mkuu ndiyo chombo cha juu kabisa cha maamuzi katika Chama. Mkutano Mkuu wa Mwaka na wa Kawaida huundwa na Wanachama (Wenyeviti na Wawakilishi kutoka AMCOS). Bodi ya LMCU Ltd huchaguliwa na Mkutano Mkuu. Bodi ndio mhimili uliokasimiwa madaraka na Wanachama kupitia Mkutano Mkuu ili kusimamia utekelezaji wa shughuli za kila siku za Chama, kuandaa sera na miongozo ya uendeshaji pamoja na kutekeleza maazimio ya Mkutano Mkuu. Bodi ya sasa ya Chama ina wajumbe saba (7) ambao hutoka katika eneo la Chama. Meneja Mkuu wa Chama ndiye mtendaji mkuu wa shughuli za kila siku za Chama na anawajibika kwa Bodi. Chama kina watendaji wengine katika vitengo mbalimbali Makao Makuu na katika Ofisi za Kanda. Katika uendeshaji na usimamizi wa shughuli zake, Chama pia kinatumia mifumo mbalimbali ya TEHAMA. Mifumo hii ni pamoja na Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU), Mfumo wa Usambazaji wa Pembejeo kutoka Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) na Mfumo wa Uhasibu na Fedha (EightSkies).

### 2.5 Tathmini ya Maendeleo ya Chama kwa Miaka Mitano Iliyopita

Ili kuweza kupanga vizuri mipango ya miaka ijayo, tathmini ya maendeleo ya Chama kwa miaka iliyopita imefanyika. Hivyo, sehemu inalenga kubaini utendaji wa shughuli za Chama kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita ka ma ilivyoelezewa katika sehemu zifuatazo.

#### 2.5.1 Wanachama na Wakulima

Wanachama ni mhimili muhimu katika maendeleo ya Chama. Wanachama ndio hutoa maamuzi ya mwisho, humiliki Chama na kudhibiti shughuli zake na ndio watumiaji na wanufaika wa shughuli na

huduma za Chama. Idadi kubwa ya Wanachama (na wakulima) huongeza nguvu ya kiuchumi ya LMCU Ltd ikiwemo kukuza uzalishaji na mtaji wa kuendesha shughuli zake. Hadi kufikia Februari 2026, Chama kilikuwa na jumla ya Wanachama (AMCOS) 61 kutoka Halmashauri za Kilwa, Lindi Manispaa na Mtama. Chama pia kinahudumia zaidi ya Wakulima 100,000 katika AMCOS hizi.




**Umbo Na. 2: Ongezeko la Wanachama wa LMCU Ltd kufikia 2025/26**

Katika Mpango Mkakati huu, LMCU Ltd inalenga kufikisha angalau wanachama 65 ifikapo 2030/31. Chama kitaendelea kufanya uhamasishaji katika Halmashauri zote ili kukuza idadi wa wakulima wanaojiunga na AMCOS. Hili litafanyika kwa ushirikiano na Maafisa Ushirika na Ofisi ya Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Lindi. Umbo Na. 2 linaonesha mwenendo wa ongezeko la Wanachama kuanzia 2015 hadi 2026.

### 2.5.2 Hisa na Viingilio vya Uanachama

Kulipa hisa huwapa Wanachama nguvu ya umiliki wa Chama na kunufaika na huduma zote zinazotolewa. Katika Masharti ya Chama, kila mwanachama hutakiwa kulipa jumla ya hisa tano (5) zenye thamani ya TZS 500,000/= (hisa 1 = TZS 100,000/=). Pia Mwanachama mpya atatakiwa kulipa kiingilio chenye thamani ya TZS 50,000/=. Chama kitaendelea kuhamasisha Wanachama walioko kulipa hisa zao kwa wakati ili kukamilisha uanachama wao na wale wapya watahamasishwa kulipa hisa zote ndani ya miezi 24 (miaka miwili) tangu kujiunga. Kila mwaka Wanachama hutakiwa kulipa ada ya uanachama ya TZS 50,000/=. Mwenendo wa ulipaji wa hisa za uanachama umeoneshwa katika Umbo Na. 3. Katika utekelezaji wa Mpango Mkakati huu, Chama kitakuwa kikihuisha viwango vya hisa, viingilio na ada ya uanachama kila inapohitajika.




**Umbo Na. 3: Ukuaji wa Hisa kwa Kipindi cha Mwaka 2020/21 hadi 2023/24**

### 2.5.3 Uzalishaji wa Mazao

Mazao ya kibiashara yanayouzwa kupitia LMCU Ltd yanazalishwa na wakulima AMCOS. Mazao haya ni korosho, ufuta na mbaazi. Kwa kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita yaani 2021/22 hadi 2025/26 hali ya uzalishaji wa mazao ya kibiashara ni kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 1. Katika Mpango Mkakati huu, Chama pia kinalenga kukuza uzalishaji wa mazao hayo na mengine ikiwemo choroko na alizeti. Takwimu zinaonesha kuwa kwa miaka mitano iliyopita Chama kimekuwa na hali nzuri ya uzalishaji wa mazao ya kibiashara. Hii inaonesha uhakika wa uhai wa Chama na utekelezaji wa mipango yake ya maendeleo. Chama kinalenga kuongeza zaidi uzalishaji wa mazao ya kibiashara katika miaka mitano ya Mpango Mkakati huu.

**Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Korosho, Ufuta na Mbaazi kwa Msimu wa 2021/22 hadi 2025/26**

| Na. | Zao | Jumla ya uzalishaji (kilo) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2021/22** | **2022/23** | **2023/24** | **2024/25** | **2025/26** | **Jumla** | **Wastani wa uzalishaji kwa mwaka** |
| 1 | **Korosho** | 19,440,559 | 14,622,801 | 15,208,627 | 41,853,885 | 42,583,740 | 133,709,612 | 26,741,922.4 |
| 2 | **Ufuta** | 27,238,263 | 27,260,960 | 29,557,407 | 33,528,046 | 50,744982 | 168,329,658 | 33,665,931.6 |
| 3 | **Mbaazi** | - | - | 2,114,006 | 3,801,521 | 4,001,477 | 9,917,004 | 3,305,668 |
| | | | | | | | | |

### 2.5.4 Utoaji wa Huduma kwa Wanachama na Wakulima

#### 2.5.4.1 Kuratibu Upatikanaji na Usambazaji wa Pembejeo kwa Wanachama

Tangu kuanzishwa kwake, Bodi na Menejimeti ya LMCU Ltd imekuwa ikiratibu upatikanaji wa pembejeo kwenda kwa wakulima wake. Chama kinatumia mfumo ulioratibiwa na Serikali kupitia Bodi ya Korosho Tanzania (CBT). Manunuzi ya pembejeo hufanyika kupitia Mradi wa Pamoja wa Vyama Vikuu vya Korosho (KCJE) Ltd. Msimu wa mwaka 2021/22, Chama kilisambaza viuatilifu aina salfa tani 898.775, dawa za maji lita 86,843 na viuatilifu vya chenga (unga) kilo 4,210. Mwaka 2022/23 Chama kilisambaza salfa tani 2,058.975 na dawa za maji lita 121,068. Mwaka 2024/25, Chama kilisambaza salfa tani 3,999.75, dawa za sumu lita 38,919 pamoja na dawa za magonjwa za maji lita 19,531 na za unga kilo 42,087. Mwaka 2025/26, Chama kilisambaza salfa tani 5,050.55, dawa za sumu lita 76,144 pamoja na dawa za magonjwa za maji lita 104,133 na za unga kilo 28,963. Katika Mpango Mkakati huu, Chama kitaendelea kuweka mikakati ili kuwezesha upatikanaji wa pembejeo za kutosha ikiwemo viuatilifu, vifungashio (viroba na magunia), mbegu na zana za kilimo kwa Wanachama na wakulima. Pia kitaanzisha maduka makubwa na mfuko wa ndani wa pembejeo. Haya yote yataongeza uzalishaji na ubora wa mazao.

#### 2.5.4.2 Kusimamia Ukusanyaji, Uhifadhi, Usafirishaji na Uuzaji wa Mazao ya Wanachama

LMCU Ltd ina jukumu la kusimamia ukusanyaji wa mazao yanayozalishwa na wakulima kupitia Wanachama. Kwa kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita, Chama kilikusanya na kuuza korosho, ufuta na mbaazi kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 2. Katika kutekeleza Mpango Mkakati huu, Chama kinalenga pia kuratibu ukusanyaji wa mazao mengine hasa alizeti na choroko kutoka kwa Wanachama na wakulima. Chama kina jukumu pia la kuratibu usafirishaji wa mazao kutoka kwa Wanachama kwenda maghala makuu kwa ajili ya kuuzwa kupitia minada. Chama kimekuwa kikitumia Wasafirishaji binafsi kutoa huduma ya hizo na sasa kimeanzishwa mradi wake wa usafirishaji. Aidha, Chama kimejenga maghala yake katika eneo lake ili kuimarisha uwezo wa kuhifadhi mazao ya Wakulima. Hii ni pamoja na ghala jipya la kisasa lilijengwa eneo la Hoteli Tatu katika Wilaya ya Kilwa. Maghala mengine mapya yatajengwa katika miaka hii mitano.

**Jedwali Na. 2: Makusanyo na Mauzo ya Mazao ya Kibiashara kwa Kipindi cha 2021/22 hadi 2025/26**

| Na. | Zao | Jumla ya makusanyo na mauzo (kilo) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2021/22** | **2022/23** | **2023/24** | **2024/25** | **2025/26** | **Jumla** |
| 1 | **Korosho** | 19,440,559 | 14,622,801 | 15,208,627 | 41,853,885 | 42,583,740 | 133,709,612 |
| 2 | **Ufuta** | 27,238,263 | 27,260,960 | 29,557,407 | 33,528,046 | 50,744982 | 168,329,658 |
| 3 | **Mbaazi** | - | - | 2,114,006 | 3,801,521 | 4,001,477 | 9,917,004 |
| | | | | | | | |

LMCU Ltd huhusika pia na kusimamia mchakato wote wa malipo kwa wakulima baada ya kuuza mazao yao kupitia minada. Wastani wa bei za mazao kwa miaka mitano iliyopita ni kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 3. Katika kutekeleza Mpango Mkakati huu, Chama kitaendelea kuimarisha usimamizi wa mauzo ya mazao yote ya Wanachama na wakulima. Chama kitaweka juhudi zaidi za kutafuta masoko mapya ya mazao ndani na nje ya nchi ili kupata bei nzuri zaidi hatimaye kukuza nguvu ya kiuchumi ya Chama, Wanachama na wakulima. Chama pia kitaratibu uuzaji wa mazao mapya ambayo hayako katika mfumo wa Stakabadhi Ghalani kama vile; alizeti na choroko. Ili kuimarisha huduma za malipo, Chama kitajenga Ofisi ya Kanda katika Halmashauri za Kilwa (Kilwa Masoko) na Manispaa ya Lindi. Pia kimenunua kiwanja cha kujenga Ofisi nyingine eneo la Kiwalala katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtama.

**Jedwali Na. 3: Bei za Korosho, Ufuta na Mbaazi kwa Mwaka 2021/22 hadi 2025/26**

| Na. | Mwaka | Bei ya korosho (TZS) | | Bei ya ufuta (TZS) | | Bei ya mbaazi (TZS) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Bei ya chini** | **Bei ya juu** | **Bei ya chini** | **Bei ya juu** | **Bei ya chini** | **Bei ya juu** |
| 1 | 2021/22 | 1,600/= | 2,286 /= | 2,201/= | 2,597/= | - | - |
| 2 | 2022/23 | 1,310/= | 1,851/= | 3,015/= | 3,184 /= | - | - |
| 3 | 2023/24 | 1,010/= | 2,075/= | 3,580/= | 4,062 /= | 1,905/= | 2,152/= |
| 4 | 2024/25 | 1,990/= | 3,865/= | 3,110/= | 3,696 /= | 1,410/= | 1,840/= |
| 5 | 2025/26 | 1,700/= | 2,650/= | 2,110/= | 2820/= | 680/= | 800/= |
| | | | | | | | |

Kwa upande wa ubora wa korosho, Chama kimekuwa kikiuza korosho ya daraja A (*Standard grade*) kwa kiasi kikubwa na kiasi kidogo cha daraja B (*Second grade*). Jedwali Na. 4 linaonesha madaraja ya korosho iliyokusanywa na kuuzwa kwa kipindi cha 2021/22 hadi 2025/26. Katika kutekeleza Mpango Mkakati huu, Chama kitaendelea kuimarisha usimamizi wa ubora wa korosho na mazao mengine kwa kushirikiana na Wanachama na Mamlaka husika. Chama huuza mazao ya wakulima kupitia mfumo

wa stakabadhi ghalani unaosimamiwa na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) kupitia minada inayoendeshwa na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX). Uuzaji wa korosho husimamiwa na Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) na uuzaji wa ufuta na mbaazi husimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA).

**Jedwali Na. 4: Madaraja ya Ubora wa Korosho Iliyouzwa Mwaka 2021/22 hadi 2025/26**

| Na. | Mwaka | Daraja A (kilo) | Daraja B (kilo) |
|---|---|---|---|
| 1 | 2021/22 | 18,979,838 | 460,721 |
| 2 | 2022/23 | 14,419,569 | 203,232 |
| 3 | 2023/24 | 14,680,652 | 527,975 |
| 4 | 2024/25 | 40,650,367 | 750,534 |
| 5 | 2025/26 | 42,583,740 | 1,006,819 |
| | **Jumla** | **131,314,166** | **2,949,281** |

### 2.5.4.3 Huduma za Elimu na Mafunzo kwa Chama na Wanachama

LMCU Ltd imekuwa pia ikitekeleza kwa vitendo msingi Na. 5 wa Vyama vya Ushirika duniani ambao ni elimu, mafunzo na taarifa. Hivyo kila mwaka, Chama hutenga asilimia kumi (10%) ya mapato yake kutoa elimu na mafunzo kwa wajumbe wa Bodi, watendaji na Wanachama. Pia Chama kimekuwa kikiwezesha utoaji wa mafunzo kwa viongozi, watendaji na wakulima wa AMCOS zake. Wakati wa kutekeleza Mpango Mkakati huu, Chama kitaendelea kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya elimu na mafunzo. Chama kitatoa mafunzo kupitia programu zake za ndani na kwa ushirikiano na wadau mbalimbali ikiwemo Kamati ya Elimu ya Ushirika Mkoa wa Lindi, Bodi za Mazao na wengine. Ziara za mafunzo kwa vitendo pia zitakuwa zikifanyika ndani na nje ya nchi.

### 2.5.4.4 Uanzishaji na Usimamizi wa Miradi/Uwekezaji

Chama pia kina wajibu wa kuanzisha na kusimamia miradi mbalimbali na kuwekeza katika taasisi mbalimbali za kibiashara kwa niaba na maslahi ya Wanachama na Wakulima. Hii inalenga kujenga mtaji wa Chama na kukuza uwezo wa kutoa huduma kwa Wanachama na wakulima. Tangu kuanzishwa kwake, Chama kimefanikiwa kufanya uwekezaji katika Benki ya Ushirika Tanzania (Coop Bank), ujenzi wa maghala na ununuzi wa mashamba (ekari 63 ziko eneo la Narwadi, Mtama DC ambazo zimelimwa korosho). Katika utekelezaji wa Mpango Mkakati huu, Chama kitaendelea kubuni, kutekeleza na kusimamia vyema miradi yake. Miradi mipya itakayotekelezwa ni pamoja na; ujenzi wa hoteli ya kisasa, kujenga kiwanda cha kuzalisha mafuta ya kupikia, kuanzisha mashamba

makubwa ya korosho (na mazao mengine), ununuzi wa magari ya usafirishaji mizigo, ujenzi wa maghala na ukumbi wa kisasa wa mikutano na kuanzisha maduka ya pembejeo. Chama pia kitaendelea kununua hisa katika Benki ya Ushirika Tanzania na kwenye taasisi nyingine. Wanachama nao watahamasishwa kufanya uwekezaji mbalimbali kujenga uchumi wao ikiwemo kujenga maghala na majengo mengine ya kibiashara, kununua magari ya mizigo, kuanzisha viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ikiwemo kubangua korosho na miradi mingine.

#### 2.5.4.5 Huduma za kijamii

Ikiwa ni sehemu ya kutekeleza msingi wa Na. 7 wa Vyama vya Ushirika duniani yaani "Ushirika Kuijali Jamii", Chama kimekuwa kikitumia sehemu ya rasilimali fedha zake kusaidia shughuli za maendeleo ya jamii. Hivyo hata wakati wa kutekeleza Mpango Mkakati huu, Chama kitaendelea kusaidia shughuli za kijamii katika eneo lake ikiwemo masuala ya elimu, afya, maafa, watu wenye mahitaji maalum na kusaidia miradi ya kijamii. Chama kitaandaa sera maalum kuongoza utoaji wa huduma kwa jamii. Kwa miaka mitano iliyopita, Chama kimechangia maendeleo ya jamii kama iliyooneshwa katika Jedwali Na. 5.

**Jedwali Na. 5: Huduma za Kijamii Zilizotolewa Mwaka 2021/22 na 2025/26**

| Na. | Mwaka | Aina ya huduma | Mnufaika | Halmashauri | Kiasi cha fedha kilichotumika (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2022/23 | Laptop 62 | Wanachama (AMCOS) | Halmashauri ya Kilwa, Mtama na Lindi Manispaa | 57,040,000/= |
| 2 | 2023/24 | Printa 62 | Wanachama (AMCOS | Halmashauri ya Kilwa, Mtama na Lindi Manispaa | 45,260,000/= |
| | | Madawati 50 | Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa | Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa | 6,000,000/= |
| 3 | 2024/25 | Viti mwendo (Wheel Chair) 2 | Wenye Mahitaji maalumu | Halmashauri ya Lindi Manispaa | 500,000/= |
| | | Chakula Sikukuu ya Eid | Wanafunzi shule ya Sekondari ya WAMA SHARAF | Halmashauri ya Lindi Manispaa | 150,000/= |
| | | Matairi ya Gari 4 | Jeshi La Polisi Wilaya ya Lindi | Lindi Manispaa | 1,200,000/= |
| 4 | 2025/26 | Taulo za Kike | Siku ya Mtoto wa Afrika (16 Juni 2025) yalifanyika Wilaya ya Liwale | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Lindi | 370,000/= |
| | | Viti 62 na Meza 62 | Wanachama (AMCOS | Halmashauri ya Kilwa, Mtama na | 31,000,000/= |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Lindi Manispaa | |
| | | Wheel Chair 2 | Watu wenye mahitaji maalumu | Halmashauri ya Lindi Manispaa | 800,000/= |
| | | | | **Jumla** | **142,320,000/=** |

### 2.6 Tathmini ya Kifedha ya Chama

Sehemu hii imefanya uchambuzi wa hali ya kifedha ya Chama kwa kipindi cha mwaka 2020/21 hadi 2024/25. Lengo kubwa ni kubaini hali ya usimamizi wa fedha na mambo ya kuboresha wakati wa utekelezaji wa Mpango Mkakati huu. Uchambuzi huu umefanyika kwa kuzingatia taarifa za fedha za Chama zilizokaguliwa na Shirika la Ukaguzi wa Hesabu na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) za mwaka 2020/21 hadi 2023/24 pamoja na taarifa za mwaka 2024/25 ambazo zimekaguliwa kwa ukaguzi wa ndani tu. Uchambuzi huu umehusisha tathmini ya hali ya kifedha ya Chama pamoja na mapato na matumizi ya Chama. Hali ya kifedha ya Chama imeoneshwa katika Jedwali Na. 6

**Jedwali Na. 6: Hali ya Kifedha ya Chama kwa Kipindi cha 2020/21 hadi 2024/25**

| | **Mwaka** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mali** | **2020/21** | **2021/22** | **2022/23** | **2023/24** | **2024/25** |
| | **TZS** | **TZS** | **TZS** | **TZS** | |
| Jumla ya Mali za muda mrefu | 70,486,880/= | 139,044,051/= | 504,697,373/= | 1,061,290,616/= | 1,872,399,402/= |
| Jumla ya Mali za muda mfupi | 2,612,201,107/= | 2,412,934,282/= | 1,207,125,599/= | 335,337,779/= | 1,297,573,353/= |
| **Jumla ya Mali** | **2,682,687,987/=** | **2,551,978,333/=** | **1,711,822,972/=** | **1,396,628,396/=** | **3,169,972,755/=** |
| | | | | | |
| **Dhima (Madeni)** | | | | | |
| Jumla ya madeni ya muda mrefu | - | - | - | - | 774,389,352/= |
| Jumla ya madeni ya muda mfupi | 2,938,290,752/= | 2,541,314,856/= | 1,902,733,194/= | 646,012,269/= | 1,317,105,358/= |
| **Jumla ya Madeni** | **2,938,290,836/=** | **2,541,314,856/=** | **1,902,733,194/=** | **646,012,269/=** | **2,091,494,709/=** |
| | | | | | |
| **Jumla ya Mtaji** | **(255,602,765/=)** | **10,663,477/=** | **(190,910,221/=)** | **750,616,127/=** | **1,078,478,046/=** |
| **Jumla ya Mtaji na Dhima** | **2,682,687,987/=** | **2,551,978,333/=** | **1,711,822,972/=** | **1,396,628,396/=** | **3,169,972,755/=** |

#### 2.6.1 Hali ya Ukuaji wa Mali, Mtaji na Dhima katika Chama

Hali ya mwenendo wa kifedha wa Chama kwa miaka mitano (5) iliyopita kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 6 hapo juu inaonesha kuwa mwenendo wa ukuaji wa mali umekuwa ukipungua mwaka

hadi mwaka hadi ongezeko lilipotokea mwaka 2024/25. Chama kitaweka mikakati mbalimbali kukuza mali zake. Hii ni pamoja na kufanya uthaminishaji wa mali na kufuata viwango vya kimataifa vya uhasibu na fedha kuhusu usimamizi wa mtaji wa uendeshaji (working capital). Madeni ya Chama yamekuwa yakipungua mwaka hadi mwaka kuonesha kuwa madeni ya wadai mbalimbali yamekuwa yakilipwa. Madeni yaliongezeka tena mwaka 2024/25 kwa sababu Chama kilichukua mkopo mkubwa wa uwekezaji kwa ajili ya ujenzi wa ghala. Ukuaji wa mtaji wa Chama umekuwa hasi kwa baadhi ya miaka ila uliongezeka mwaka 2023/24 na 2024/25.

Katika Mpango Mkakati huu, Chama kitaweka mikakati ya kukuza mtaji wake ikiwemo kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuanzisha mifuko ya ndani ya matengo ya hiari (revenue reserves) mfano; mfuko wa ujenzi, mfuko wa pembejeo, mfuko wa tengo la badiliko la msimu (revolving fund) na mingine. Bodi na Menejimenti ya Chama wataendelea kuimarisha usimamizi mzuri wa fedha na kuhakikisha kuwa mali zilizoko zinaendelezwa na kuzalisha ili kuleta faida na tija kwa Chama na Wanachama. Chama kitaimarisha uthibiti wa ndani, kujenga uwezo wa watendaji walioko ikiwemo wale wa Kitengo cha Uhasibu na Fedha na kuajiri watendaji wapya wenye sifa. Chama pia kitaandaa sera mbalimbali ili kuimarisha usimamizi wa fedha na mali za Chama, kuandaa taarifa za fedha kwa viwango sahihi pamoja na kufanya uhakiki wa madeni na kuyalipa.

### 2.6.2 Hali ya Mapato na Matumizi

Tathmini ya uwiano wa mapato na matumizi huonesha uwezo wa Chama kuhimili matumizi yake kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya mapato vilivyoko. Tathmini ya hali ya mapato na matumizi kwa kipindi cha mwaka 2020/21 hadi 2024/25 imeoneshwa katika Jedwali Na. 7. Kwa ujumla, Chama kimekuwa na mapato mengi kuliko matumizi katika mwaka 2020/21 na 2021/22. Kwa mwaka 2022/23 na 2023/24, Chama kilikuwa na matumizi yaliyozidi kidogo mapato yake wakati mwaka, 2024/25 Chama kiliweza kutengeneza ziada kutokana na biashara zake.

**Jedwali Na. 7: Mapato na Matumizi ya Chama kwa kipindi cha 2020/21 hadi 2024/25**

| Mwaka wa fedha | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
|---|---|---|---|---|---|
| Mapato TZS (A) | 702,604,450/= | 1,507,694,115/= | 1,396,890,231/= | 1,519,329,657/= | 2,978,742,105/= |
| Matumizi TZS (B) | 635,938,435/= | 1,045,830,317/= | 1,604,837,450/= | 1,641,318,829/= | 2,510,367,933/= |
| Tofauti (A-B) | 66,665,015/= | 461,863,797/= | (207,947,219/=) | (121,989,173/=) | 468,374,172/= |
| Uwiano wa ukuaji wa mapato na matumizi (A/B) | 1.1 | 1.4 | 0.9 | 0.9 | 1.2 |

Chama kinatambua kuwa kina wajibu wa kuthibiti matumizi yake ili kuwa na ustawi mzuri kifedha. Kupitia Mpango Mkakati huu, Chama kitatekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo; kufuata bajeti ya mwaka iliyoidhinishwa, kupunguza gharama za uendeshaji na matumizi yasiyo ya lazima na kuhakikisha kuwa hakitumii zaidi ya 85% ya mapato yake ya mwaka.

## 2.7 Uchambuzi wa Mazingira ya Chama

Sehemu hii inaelezea uchambuzi wa mazingira ya Chama. Uchambuzi huu unalenga kubaini mambo mbalimbali ambayo yanaweza kuwa rafiki au kikwazo kwa Chama katika kutekeleza Mpango Mkakati huu na shughuli nyingine. Uchambuzi wa mazingira ya Chama umefanyika kwa kutumia nyenzo mbili (2) za uchambuzi ambazo ni; UMAFUCHA (*SWOC Analysis*) na USTAJaSU (*CoopPESTEL Analysis*). Uchambuzi wa mazingira kwa kutumia kila nyenzo umeelezewa hapa chini.

### 2.7.1 Uchambuzi wa UMAFUCHA (SWOC Analysis)

Katika sehemu hii, uchambuzi wa mazingira ya Chama umefanyika kwa kuangalia mambo makuu manne (4). Mambo haya ni; Uwezo (U) wa Chama, Madhaifu (MA) yaliyopo, Fursa (FU) zilizopo na Changamoto (CHA). Jedwali la Uchambuzi Na. 8 linaonesha uchambuzi wa UMAFUCHA.

**Jedwali Na. 8: Uchambuzi wa Uwezo, Madhaifu, Fursa na Changamoto katika Chama**

| Eneo la Uchambuzi | Sifa | Matokeo yake kwa Chama (+ au -) | Mambo ya kufanya (mikakati) |
|---|---|---|---|
| | | | |
| **Uwezo (nguvu)** | Uwepo wa uzalishaji mkubwa wa mazao kutoka kwa wakulima | Hukiwezesha Chama kuwa na nguvu ya ushawishi sokoni na uhakika wa kuendelea kuwepo kwani kitaendelea kufanya biashara na kupata mapato hivyo kuimarisha uwezo wa kutoa huduma na kufanya uwekezaji | Chama kitaendelea kuimarisha huduma za ugani na upatikanaji wa mitaji kukuza uzalishaji wa mazao kutoka kwa Wanachama na wakulima. Pia kitaendelea kuratibu upatikanaji wa masoko ya uhakika. |
| | Uwepo wa uongozi imara na wenye maono ya maendeleo | Chama kinakuwa na uhakika kuwa shughuli zake za kila siku, mali na fedha za Chama, huduma na miradi mbalimbali vitasimamiwa vizuri kwa manufaa ya Chama na Wanachama. | Chama kitaendelea kufanya kazi kwa kuzingatia misingi ya ushirika na utawala bora. Chama pia kitaendelea kujenga uwezo wa wajumbe wa Bodi ili wasimamie vyema shughuli za Chama. |
| | Watendaji wenye ujuzi, maarifa na uzoefu wa kutosha kutekeleza majukumu yao | Utekelezaji wa shughuli za kila siku za Chama na utoaji wa huduma kwa Wanachama na wakulima vinafanyika kwa urahisi na ufanisi. Miradi na mali za Chama zitasimamiwa vizuri na pia mipango mbalimbali ya maendeleo inaweza kufanikiwa kwa wakati. | Chama kitaendelea kujenga uwezo wa watendaji wake na kuendelea kuajiri watendaji wengine ili kukidhi mahitaji ya Chama ikiwemo utekelezaji wa Mpango Mkakati huu. |
| | Idadi ya kuridhisha ya Wanachama na wakulima wanaohudumiwa na Chama | Chama kina fursa ya kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo na kupata usaidizi mzuri kutoka kwa Wanachama. Inasaidia pia kufanikisha lengo la Chama kukuza uzalishaji wa mazao ya kibiashara na kupata malighafi endapo kikianzisha mradi ya kiwanda cha kuzalisha mafuta ya kula na hata kubangua korosho miaka ya baadae. | Chama kitashirikiana na Maafisa Ushirika na Maafisa Ugani kuhamasisha wakulima zaidi kijiunga na Wanachama (AMCOS) |
| | Uwepo wa Ofisi ya kisasa ya Chama, Ofisi za Kanda na vitendea kazi muhimu | Hukiwezesha Chama kuwa na mazingira mazuri ya kufanyia kazi hivyo kuwawezesha wajumbe wa Bodi na Watendaji kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Inasaidia pia kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa Wanachama na wakulima. | Chama kitaendelea kutunza vyema Ofisi zake, kununua vitendea kazi muhimu na kuimarisha utoaji wa huduma kwa Wanachama na wakulima. |
| | Uwepo wa maghala ya kisasa ya kuhifadhi mazao na bidhaa nyingine | Chama kinaweza kuhifadhi mazao ya Wanachama na wakulima na kuwezesha uhifadhi na usambazaji wa pembejeo na vifungashio kwa urahisi. | Chama kitaendelea kusimamia vizuri maghala yake na kujenga mengine kuimarisha huduma za uhifadhi wa mazao na bidhaa. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Ushirikiano mzuri kati ya Bodi, watendaji na Wanachama | Chama kimeweza kuwa na hali ya utulivu na kufanikisha malengo yake. Hii itasaidia utekelezaji wa Mpango Mkakati huu kwa urahisi. | Kwa muda wote, Chama kitaendeleza uhusiano na ushirikiano mzuri ulioko. Pia Chama kitaandaa sera za huduma kwa wateja na utatuzi wa migogoro. |
| | Usimamizi mzuri wa usambazaji wa pembejeo na mahitaji mengine ya Wakulima | Chama kimewazesha wakulima kupata pembejeo bora na mahitaji mengine (mfano magunia na viroba) kwa wakati. Hii pia itatoa uzoefu wakati wa kutoa pembejeo za uzalishaji wa mazao mengine. | Chama kitaendelea kuratibu upatikanaji wa pembejeo na mahitaji mengine na kuimarisha usimamizi wake ili kuwafikia wakulima wote kwa wakati |
| | Uwepo wa wakulima wanaopenda maendeleo kupitia Ushirika | Uhakika wa kufanikisha malengo ya mpango huu ikiwemo kukuza uzalishaji na ubora wa mazao ya kibiashara na kushawishi watu wengine kujiunga na AMCOS | Chama kitaendelea kushirikiana kwa ukaribu na Wanachama kukuza uzalishaji na ubora wa mbalimbali na kuhamasisha Wakulima wengine kujiunga na AMCOS |
| | Uwepo wa ardhi ya kutosha kwa uwekezaji na shughuli nyingine inapohitajika | Kupata nafasi ya kuongeza vitega uchumi vingine kwa maendeleo ya Chama | Chama kitaendelea kununua na kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kujua aina ya miradi inayoweza kuanzishwa baadae katika eneo lake |
| | Usimamizi mzuri wa mauzo na malipo ya wakulima | Chama kina uhakika wa kuendelea kuhudumia Wanachama na Wakulima wake kwani wamejenga imani kwa Chama chao. Hii itakuwa pamoja na usimamizi wa mauzo ya mazao mbalimbali. | Viongozi na watendaji wa Chama wataendelea kuweka juhudi kuimarisha usimamizi wa mauzo na kuhakikisha kuwa wakulima wanalipwa kwa wakati kwa mazao waliyouza kupitia Chama. |
| | Uwepo wa hali ya kuridhisha ya kifedha | Chama kinaweza kutekeleza vizuri miradi na mipango mbalimbali ya maendeleo kwa wakati | Chama kitaendelea kuimarisha usimamizi wa fedha za ndani na kubuni vyanzo vingine vya mapato |
| | Kuaminika zaidi na taasisi za fedha na wadau wengine | Kumekiwezesha Chama kupata huduma za kifedha na huduma nyingine muhimu bila changamoto kubwa | Chama kitaendelea kudumisha ushirikiano na uaminifu wake kwa wadau na kutimiza wajibu wake ikiwemo kulipa mikopo kwa wakati na kuzingatia makubaliano ya kibiashara iliyoko na taasisi za fedha na kufuata Sheria na taratibu kama inavyotakiwa na Mamlaka mbalimbali za Serikali. |
| | | | |
| | | | |
| **Madhaifu** | Kutegemea zaidi mazao machache ya kibiashara (korosho, mbaazi na ufuta) | Hukizuia Chama kupata mapato ya kutosha na kukuza biashara zake. Chama huweza kupata vihatarishi vya kimasoko kama vile bei ndogo ya mazao kutokana na utegemezi huo. | Chama kitaweka juhudi kuhamasisha uzalishaji, kuzinhgatia ubora na upatikanaji wa masoko. Kitawezekeza pia katika uongezaji thamani wa mazao mbalimbali na uzalishaji wa mazao mbadala kama vile alizeti na choroko. |
| | Kukosekana kwa mafunzo ya mara kwa mara kwa viongozi na watendaji | Huweza kikikwamisha Chama kuwa na viongozi na watendaji wenye weledi wa kutosha kukabiliana na | Chama kitabaini mara kwa mara mahitaji ya mafunzo, kuandaa programu ya mafunzo na kutoa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | wa Chama kujenga uwezo wao zaidi | mabadiliko katika uendeshaji na usimamizi wa shughuli za Chama. | mafunzo husika kwa wajumbe wa Bodi na Watendaji. |
| | Utegemezi mkubwa wa ushuru kama chanzo kikuu cha mapato ya Chama | Chama kinashindwa kupata rasilimali fedha kwa wakati kutekeleza shughuli/mipango mbalimbali iliyoko | Chama kitaendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato ikiwemo kuanzisha miradi (vitega uchumi) mbalimbali ili kufanikisha malengo yake ya kimaendeleo na kukuza mtaji wa ndani. |
| | Kutokuwa na mpango maalumu wa urithishaji wa ujuzi na madaraka | Huathiri uwezo wa Chama kuwaandaa viongozi na watendaji wazuri watakaoweza kukitumikia Chama miaka ya baadae | Mpango wa urithishaji madaraka na/ujuzi utaandaliwa |
| | Matumizi hafifu ya TEHAMA miongoni mwa watendaji na viongozi wa AMCOS katika shughuli za kila siku | Kunaathiri uandaaji na utunzaji wa taarifa. Pia watendaji wanatumia watu nje ya Wanachama hivyo kuathiri utunzaji wa taarifa/siri za Wanachama. | Chama kitasaidia upatikanaji wa mafunzo ya TEHAMA na vitendea kazi muhimu katika AMCOS zake |
| | Uhaba wa rasilimali watu ya kutosha kwa baadhi nafasi (kada) | Huathiri ufanisi wa Chama katika baadhi ya maeneo ya kiutendaji | Chama kitatenga rasilimali fedha za kutosha na kuajiri watendaji wapya wenye sifa katika nafasi mbalimbali |
| | Ukosefu wa elimu ya kutosha kwa viongozi, watendaji na wakulima katika AMCOS | Huathiri ushiriki mzuri wa Wanachama na wakulima katika masuala ya Chama, uzalishaji na mambo mengine | Chama kitaratibu utoaji wa elimu ya Ushirika, uongozi, kilimo na masuala mengine ili kujenga uwezo wa wakulima, viongozi na watendaji wa AMCOS kwa kushirikiana na wadau wake. Pia kitakuwa kikitenga fedha za kutosha kwa ajili ya elimu na mafunzo kwa Wanachama. |
| | Ukosefu wa baadhi ya sera, mipango biashara na miongozo mingine muhimu ya kuendesha shughuli za Chama | Huzuia Chama kupata mwongozo sahihi wa kutekeleza mambo mbalimbali na kufanya maamuzi | Bodi itaandaa na kuhuisha sera na miongozo muhimu ya uendeshaji na usimamizi wa Chama |
| | | | |
| | | | |
| **Fursa** | Uwepo wa ardhi kubwa inayofaa kwa kilimo katika eneo la Chama | Hukipa Chama uhakika wa mafanikio katika juhudi za kukuza uzalishaji wa mazao ya kibiashara na miradi inayolenga wakulima katika maeneo ya Chama. Pia huwezesha ongezeko la idadi ya Wanachama na wakulima. | Chama kitashirikiana na Serikali, Wanachama na wadau wengine katika kuhamashisha kilimo cha mazao mbalimbali ya kibiashara pamoja na kushawishi wakulima wengi kujiunga na Wanachama (AMCOS) katika maeneo yao. |
| | Sifa nzuri ya Chama katika jamii kufuatia michango yake katika maendeleo ya jamii na mahusiano | Inasaidia kujenga taswira nzuri ya Chama na kuaminika na jamii na wadau wake. Inaweza pia kuchochea wakulima wengine kujiunga na AMCOS | Chama kitaendelea kusaidia shughuli za maendeleo ya jamii na kutoa elimu kwa umma kuhusu Ushirika na faida zake. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | yake na wadau mbalimbali | au kuanzisha vyama vyao. | |
| | Uwepo wa miongozo mbalimbali inayotolewa kwa ajili ya Vyama vya Ushirika | Husaidia kuweka mazingira mazuri kwa Chama na Wanachama kufanya shughuli zao kwa kuwa na miongozo sahihi ya utekelezaji wa shughuli zao | Chama kitaendelea kufuatilia na kutumia miongozo yote inayotolewa na Mamlaka mbalimbali ili kufanikisha shughuli zake. |
| | Ukaribu na watoa huduma na taasisi mbalimbali zinazohusika na maendeleo ya kilimo na ushirika | Huwezesha Chama kupata huduma mbalimbali kwa urahisi kama vile huduma za usimamizi, mikopo, usafirishaji, sheria, elimu na ushauri, masoko na huduma nyingine kwa urahisi. | Chama kitadumisha uhusiano mzuri na watoa huduma walioko na Mamlaka husika za maendeleo ya ushirika na kilimo. Pia Chama kitaendelea kubaini watoa huduma wengine muhimu na kufanya nao kazi. |
| | Uwepo wa miundombinu ya barabara katika sehemu nyingi ndani ya eneo la Chama | Hukiwezesha Chama kusafirisha kwa urahisi mazao ya kibiashara kutoka kwa wakulima kwenda sokoni au kwenye kiwanda chake. Pia inasaidia kusafirisha pembejeo kwenda kwa wakulima na kusambaza bidhaa mbalimbali kutoka katika miradi ya Chama. | Chama kitaendelea kushiriki katika kutunza miundombinu iliyopo ikiwemo kufanya kazi na Mamlaka husika za Serikali (Halmashauri za Wilaya na TARURA) |
| | Uhakika wa uendelevu wa uhitaji wa mazao ya korosho, ufuta, mbaazi katika masoko ya ndani na nje ya nchi | Hutoa uhakika wa kuendelea kufanya uwekezaji, uzalishaji na kutoa huduma zinazolenga mazao ya kibiashara bila wasiwasi wowote. | Chama kitaendelea kusimamia uzalishaji na ubora wa mazao yote ya kibiasahra kutoka kwa Wanachama na wakulima ili kuendelea kuhimili ushindani na kupata masoko mazuri. Chama kitatafuta masoko mapya nje ya nchi ili kuuza mazao na bidhaa za viwandani moja kwa moja. |
| | Mahitaji makubwa ya huduma za usafirishaji wa mazao, pembejeo na bidhaa nyingine | Chama kinaweza kuwekeza katika mradi wa usafirishaji | Chama kitatenga rasilimali za kutosha kuwekeza katika mradi wa usafirishaji |
| | Uwepo wa hali ya amani katika nchi | Kunasaidia shughuli za Chama, Wanachama na wakulima wake kufanyika vizuri bila hofu yoyote. | Chama kitatumia fursa hii kutekeleza majukumu yake na kuimarisha huduma zake kwa ustawi wa Chama na Wanachama. Pia kitaendelea kuwa sehemu ya kudumisha amani na utulivu katika eneo lake la kazi. |
| | Uwepo wa mahitaji endelevu ya mafuta ya kula miongoni mwa watu nchini | Hukipa Chama uhakika wa mafanikio ikiwemo kupata masoko ya uhakika na mapato zaidi kwa kuwekeza katika kiwanda cha kuzalisha mafuta ya kula | Chama kitaendelea kuhamasisha wakulima kulima mazao ya mbegu za mafuta ikiwemo alizeti na kuwapa mbegu bora kwa wakati ili kupata malighafi za kutosha kwa ajili ya kiwanda cha kuzalisha mafuta ya kula<br><br>Chama kitaandaa mpango biashara na kufuata taratibu husika ili kuanzisha kiwanda cha kuzalisha mafuta ya kula |
| | Matarajio ya uwekezaji mkubwa | Chama kinapata fursa ya kuwekeza katika miradi | Chama kitawekeza katika miradi ya hoteli na ukumbi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | katika sekta ya gesi na miradi mingine ya kimkakati katika mkoa wa Lindi | yenye tija kulingana na fursa zilizoko sasa na zitakazojitokeza hapo baadae | wa kisasa<br>Chama kitaendelea kubaini fursa nyingine za uwekezaji wa kimkakati zinazoibuka |
| | | | |
| | | | |
| **Changamoto (Matishio)** | Mabadiliko ya hali hewa | Huweza kuathiri kiwango cha uzalishaji wa mazao ya kibiashara kutoka kwa Wanachama, Wakulima na hata mashamba ya Chama | Chama kitahamasisha wakulima kutumia mbegu bora za mazao mbalimbali na miche bora ya korosho. Pia kitawapa mafunzo wakulima kuhusu mbinu bora za kilimo kwa kushirikiana kwa ukaribu na wadau wa kilimo. |
| | Uwepo wa baadhi ya wauzaji wa pembejeo zisizo na ubora | Huweza kuathiri uzalishaji na ubora wa mazao ya kibiashara na chakula kwa Wakulima | Chama kitashirikiana na Mamlaka husika kudhibiti usambazaji wa pembejeo zisizo na viwango sahihi |
| | Mwingiliano wa kisiasa katika shughuli za Chama | Huweza kuathiri utekelezaji wa mipango ya Chama ya kimaendeleo hasa endapo matamko ya kisiasa yameagiza Chama kufanya vitu vingine bila kujali vipaumbele vyake. | Chama kitashirikiana kwa ukaribu na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) na Vyama Vikuu vingine ili kuunda nguvu ya pamoja kudhibiti ushawishi wa wanasiasa katika uendeshaji wa shughuli za Chama. Pia Chama kitazingatia Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika, kushiriki majukwaa ya wadau wa ushirika kitaifa na kimataifa na kuepuka kutekeleza jambo lolote nje ya vipaumbele vyake kwa shinikizo la kisiasa. |
| | Kuyumba kwa bei ya mazao ya kibiashara katika soko | Hali hii huathiri kiasi cha mapato kwa Chama, Wanachama na wakulima. Pia huweza kupunguza moyo wa kujituma miongni mwa wakulima kuendelea kuzalisha mazao ya kibiashara kwa wingi. | Chama kitaendelea kushirikiana na Viongozi na Watendaji wa AMCOS kusimamia uzalishaji, ukusanyaji na ubora wa mazao. Chama pia kitawekeza katika miradi ya kuongeza thamani ya mazao ya wakulima ikiwemo kuanzisha kiwanda cha kuzalisha mafuta ya kula. Pia Chama kitatafuta masoko mbadala nje ya nchi. |
| | Uwepo wa wanunuzi binafsi wa mazao ya kibiashara kwa mfumo usio rasmi (kama vile *kangomb*a) | Huathiri makusanyo na mauzo ya mazao kupitia Chama na kushusha kiwango cha mapato tarajiwa kwa Chama, Wanachama na wakulima | Viongzi na Watendaji wa Chama watashirikiana kwa ukaribu na Wanachama na Mamalaka husika katika kuratibu biashara ya mazao ya kibiashara, kutoa elimu endelevu ya ushirika na uwajibikaji na kufanya vikao kazi kabla ya msimu na kuweka mikakati ya kuwadhibiti uuzaji wa mazao katika mfumo wa masoko usio rasmi. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Ushiriki mdogo wa wanawake na vijana katika uanachama na uongozi wa AMCOS | Hii huzuia ukuaji wa idadi ya wakulima wanaojiunga na AMCOS na kuathiri uwezo wa kujenga viongozi wengi katika AMCOS | Chama kitaanda mpango wa uhamasishaji na kutoa elimu kwa jamii ili kuvutia vijana na wanawake wengi kujiunga na AMCOS kushiriki ipasavyo katika masuala ya kilimo na ushirika. |
| | Upotevu wa mazao ya Wakulima katika maghala | Huweza kupunguza kiasi cha mazao yanayotakiwa kuuzwa hivyo kuathiri mapato ya Chama, Wanachama na wakulima | Chama kitashirikiana kwa ukaribu na Wanachama na Mamlaka husika katika kudhibiti upotevu wa mazao ghalani. Pia kitawachukulia hatua kali wahusika wote. |
| | Chama kutokuwa na uwezo wa kupanga bei za mazao ya Wanachama na wakulima sokoni | Chama kinashindwa kuwezesha upatikanaji wa bei kubwa ya mazao yaliyozalishwa | Chama kitaweka juhudi katika kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao yote ili kuongeza nguvu yake katika soko. Pia Chama kitaendelea kutafuta masoko mapya ya mazao yake na kuwekeza zaidi katika kuongeza thamani kupitia ujenzi wa viwanda. |
| | | | |
| | | | |

Kupita uchambuzi huu wa UMAFUCHA, Chama kimebaini hali yake ndani na nje. Chama kitaendelea kujiimarisha uwezo wake, kuondoa madhaifu, kukabili changamoto na kutumia fursa zilizoko ili kufanikisha utekelezaji mzuri wa Mpango Mkakati. Chama kitashirikiana kwa ukaribu na wadau mbalimbali katika kutekeleza shughuli zake.

### 2.7.2 Uchambuzi wa Mazingira ya Makuu ya Kibiashara (CoopPESTEL Analysis)

Kama ilivyo kwa taasisi nyingine za kibiashara, LMCU Ltd hufanya kazi katika mazingira ya kibiashara yanayohusisha mambo mbalimbali ambayo kwa pamoja huweza kufanikisha au kukwamisha maendeleo yake kwa namna mbalimbali. Sehemu hii imefanya uchambuzi wa mazingira makuu ya kibiashara kwa mtazamo wa kitaifa na kimataifa. Uchambuzi huu umejikita katika mambo yaliyo nje ya ushawishi wa moja kwa moja wa Chama na umefanyika kwa kutumia nyenzo ya USTAJaSU (CoopPESTEL analysis). Nyenzo hii imekichambua Chama katika maeneo makuu saba (7) ambayo ni mazingira ya; Ushirika (U), Siasa (S), Teknolojia (T), mazingira ya asili (A), mazingira ya kijamii (Ja), Sheria (S) na Uchumi (U) kama ilivyoelezewa hapa chini.

#### 2.7.2.1 Mazingira ya Ushirika (na Kilimo)

Uwepo wa Vyama vya Ushirika vya aina mbalimbali nchini umeleta faida kubwa katika maendeleo ya Wanachama, jamii na uchumi wa nchi kwa jumla. Maendeleo ya Vyama hivi hutegemea mambo mbalimbali ikiwemo uwepo wa uwajibikaji, rasilimali, uwezo wa watendaji na viongozi na mahusiano yao mazuri na Serikali na wadau wengine. Kwa miaka mingi katika nchi yetu kumekuwa mazingira rafiki ya usimamizi na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika. Serikali imeendelea kuweza jitihada zinazolenga kuimarisha ushirika nchini. Baadhi ya jitihada hizi ni pamoja na kuanzisha taasisi mbalimbali kusaidia maendeleo ya Vyama vya Ushirika na kilimo kwa ujumla.

Taasisi hizi ni kama vile; Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Ofisi za Ushirika na Kilimo katika Halmashauri za Wilaya, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Shirika la Ukaguzi wa Hesabu na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI)-Naliendele, Bodi ya Stakabadhi za Ghala (WRRB), Wakala wa Vipimo (WMA), Wizara ya Kilimo na nyingine. Taasisi hizi zote zimekuwa zikitoa miongozo mbalimbali ili kuongoza usimamizi na uendeshaji wa shughuli za kila siku na biashara katika Vyama vya Ushirika. Kwa miaka yote ya uwepo wake Chama kimekuwa na uhusiano mzuri na wadau mbalimbali kutoka taasisi za Serikali na sekta binafsi.

Wakati wa kutekeleza Mpango Mkakati huu, LMCU Ltd itaendelea kufanya kazi kwa ukaribu na wadau hawa ushirika na kilimo. Pia Chama kitafuata miongozo kutoka kwa wadau mbalimbali. Chama kitaendelea kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Ushirika nchini Tanzania (TFC) na wadau wengine wa kimataifa ikiwemo Shirikisho la Vyama vya Ushirika vya Sekta ya Kilimo Africa

(AAACO), Shirikisho la Vyama vya Ushirika duniani (ICA) na wadau wengine wanaohusika na maendeleo ya ushirika na kilimo duniani.

#### 2.7.2.2 Mazingira ya Siasa

LMCU Ltd inatambua kuwa uwepo wa mazingira mazuri ya kisiasa katika nchi huweza kuleta ustawi kwa Vyama vya Ushirika. Kwa miaka mingi, Serikali katika awamu mbalimbali imeendelea kuweka mazingira mazuri ya kisiasa na umoja wa kitaifa ili shughuli za kimaendeleo zifanyike bila wasiwasi. Serikali imeendelea kufanya kazi kwa ukaribu sana na Vyama vya Ushirika na kuvitumia katika kufikisha huduma kwa wananchi. Chama kinatarajia kuwa kwa kipindi chote cha kutekeleza Mpango Mkakati huu, mazingira ya kisiasa yataendelea kuwa rafiki kwa Chama, Wanachama na wakulima. Pia Serikali itaendelea kusaidia maendeleo ya Ushirika na kuhakikisha nchi inakuwa na amani na utulivu wakati wote ili kuviwezesha Vyama vya Ushirika kupanga na kutekeleza mipango na shughuli zao bila wasiwasi.

Chama pia kitaendelea kushirikiana na viongozi mbalimbali wa Serikali na wa kisiasa pale inapobidi ili kuweza kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, endapo kitaingiliwa kisiasa kwa namna yoyote inayoweza kuathiri shughuli zake, Chama kitawasiliana na wadau mbalimbali husika kutatua changamoto hizo ikiwemo kumshirikisha Mrajis/Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Maafisa Ushirika, TFC na kutumia Majukwaa ya Ushirika. Chama pia kitajiepusha kushiriki shughuli za kisiasa wakati wote wa kutekeleza Mpango Mkakati huu. Kwa upande mwingine Chama kinatambua kuwa Ilani ya Chama kilichoko madarakani kwa sasa imeweka kipaumbele kuendeleza ushirika nchini. Hivyo LMCU itatumia fursa hivyo kujiimarisha ikiwemo kufanya uwekezaji mbalimbali.

#### 2.7.2.3 Mazingira ya Uchumi

Kwa miaka mingi, Tanzania imekuwa moja ya nchi zenye ukuaji mzuri wa kiuchumi barani Africa. Pamoja na uwepo wa janga la mlipuko wa ugonjwa wa virusi ya korona (UVIKO-19), kuzorota kwa uchumi wa duniani kutokana na mgogoro unaoendelea Ulaya Mashariki bado hali ya uchumi wa nchi imeendelea kuwa ya kuridhisha. Changamoto za kiuchumi duniani pia zimeleta madhara kwenye mnyororo wa usambazaji wa bidhaa mbalimbali ikiwemo uagizaji wa pembejeo, vifungashio, zana za kilimo na hata kuathiri soko la mazao na bidhaa za kilimo. Chama kitaendelea kuweka juhudi za kuhakikisha kuwa kinasimamia vyema mfumo wa stakabadhi ghalani na kuendeleza mahusiano mazuri na wanunuzi wa mazao na Mamlaka zinazosimamia uuzaji wa mazao.

Kumekuwa na wito mkubwa wa Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuvitaka Vyama vya Ushirika kuwekeza katika uongezaji wa thamani na kusaidia upatikanaji wa bidhaa muhimu ikiwemo mafuta ya kula. Chama kinaona fursa kubwa ya kuwekeza katika kiwanda cha kuzalisha mafuta ya kula kupunguza uhaba wa bidhaa nchini. Kwa upande wa mitaji, Chama kinatambua kuwa kumekuwa na juhudi nzuri za Serikali kupitia Benki Kuu ikiwemo kupunguza riba za mabenki kwa mikopo ya uwekezaji sekta ya kilimo (kufikia 9%) pamoja na uanzishaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na Benki ya Ushirika Tanzania (Coop Bank) ili kusaidia upatikanaji wa huduma za kifedha kwa Chama na wanachama wake. Haya yote yanatoa fursa kwa Chama kupata huduma za kifedha pale inapohitajika na kutekeleza shughuli zake. Katika Mpango Mkakati huu, Chama kitaanzisha pia SACCOS yenye nguvu ili Wanachama na wakulima wapate huduma za kifedha kwa masharti nafuu.

Kwa muda mrefu kumekuwa na changamoto ya udogo wa soko la ndani ya nchi kwa mazao yanayouzwa na Chama mfano Korosho, mbaazi na ufuta. Hii imepelekea Chama kutegemea zaidi masoko ya nje. Chama kinatambua kuwa kinahitaji kuweka juhudi zaidi katika kuongeza thamani ya mazao husika na kutafuta masoko mengine mbadala ndani na nje ya nchi. Upatikanaji wa pembejeo umekuwa ni rafiki kwani kuna utaratibu mzuri wa manunuzi na usambazaji kwa ushirikiano kati ya Serikali na Vyama vya Ushirika, mfano mfumo wa manunuzi makubwa kupitia Mradi wa Pamoja wa Vyama Vikuu vya Ushirika vya Korosho (KCJE Ltd) na wadau wengine.

Chama kimeendelea pia kuwa mdau tegemeo katika kuchangia maendeleo ya kiuchumi kwa taifa kwa kulipa kodi stahiki za Serikali kuu na tozo za Halmashauri za Wilaya na kitaendelea kufanya hivi kipindi chote cha kutekeleza Mpango Mkakati huu. Aidha, kwa miaka mitano ijayo, Chama kitafanya kazi kwa ukaribu na wadau kutoka taasisi mbalimbali za Serikali na sekta binafsi zinazojihusisha na maendeleo ya ushirika, viwanda na kilimo.

#### 2.7.2.4 Mazingira ya Kijamii

Chama kinatambua kuwa uko umuhimu wa kufanya kazi kwa ukaribu na jamii inayokizunguka. Wanachama, wakulima pamoja na wadau wa Chama hutokea ndani ya jamii mbalimbali. Hadi sasa, Chama kina mahusiano mazuri na wadau mbalimbali na jamii kwa ujumla katika eneo lake na sehemu nyingine nchini. Chama kimeendelea kuwa mstari wa mbele kusaidia maendeleo ya jamii katika masuala ya afya, elimu, kusaidia waliokumbwa na majanga mbalimbali na shughuli nyingine. Chama kitaendelea kusaidia shughuli za maendeleo ya jamii na watu wenye uhitaji. Haya yote yataendeleza hadhi ya Chama, imani kwa wadau wake na kuonesha uwajibikaji wake kwa jamii. Viongozi na

watendaji wa Chama wamekuwa na mahusiano mazuri na Wanachama na wadau wengine wa nje kutoka taasisi za Serikali na sekta binafsi pamoja na Vyombo vya Habari. Pia Chama na Wanachama wake kwa miaka yote hawajawa na migogoro mikubwa inayoweza kuathiri shughuli zao.

Chama pia kinazungukwa na jamii ya watu ambao kwa sehemu kubwa wana uelewa wa kuhusu Vyama vya Ushirika (AMCOS) na faida zake, hivyo watakuwa na mtazamo chanya kuhusu Chama na shughuli zake. Kwa miaka ya hivi karibuni, baadhi ya sehemu katika eneo la Chama (hasa Wilaya ya Kilwa) zimekuwa na ongezeko kubwa la uhamiaji wa watu kutoka mikoa mingine nchini. Kwa kiasi fulani imesaidia ongezeko la uzalishaji, hasa ufuta. Elimu zaidi ya ushirika kwa jamii ya wahamiaji na wakulima inahitajika kwani wengi wao pamoja na uzalishaji wa mazao hawapendi kujiunga uanachama katika AMCOS.

Chama pia kinatambua kuwa kuwekuwa na tamaduni zisizo rafiki ikiwemo vikwazo vya umiliki wa ardhi kwa wanawake na vijana hivyo kuzuia ushiriki wao mkubwa kwenye AMCOS. Katika kutekeleza Mpango Mkakati huu, Chama kitashirikiana na wadau mbalimbali kuhamasisha ushiriki wa wanawake na vijana katika ushirika (AMCOS) ikiwemo kuwa Wanachama na kushiriki katika uongozi. Aidha, Chama kitaendelea kushirikiana na wadau kutatua migogoro inayojitokeza, shughuli za maendeleo ya jamii na kutoa elimu ya ushirika, kilimo na masuala mengine.

#### 2.7.2.5 Mazingira ya Teknolojia

Mafaniko ya Chama na Wanachama wake hutegemea pia matumizi ya teknolojia rafiki kwa shughuli mbalimbali. Hii inaweza kuwa katika masuala ya uzalishaji, uhifadhi na uongezaji thamani ya mazao na hata usimamizi na uendeshaji wa Chama na AMCOS zake. Wanachama wanahitaji kutumia teknolojia mbalimbali ili kurahisisha kazi na kuongeza ufanisi. Chama kitaendelea kuwezesha upatikanaji wa; mashine bora za kupulizia madawa kwenye mazao, Vifaa vya kielektroniki (kompyuta, printer, mizani za kidigitali), vipima unyevu vya kutosha na teknolojia nyingine. Kumekuwa na uelewa mdogo wa matumizi ya TEHEMA katika AMCOS miongoni mwa watendaji na viongozi hususani matumizi ya kompyuta katika shughuli za kila siku. Hivyo Chama kinatambua hitaji hili na kitaweka mikakati ya kuwezesha mafunzo ya matumizi ya kompyuta kwa watendaji na viongozi wa AMCOS.

Katika kulipa Wakulima na wadau wengine, Chama kitendelea kutumia mifumo ya kibenki na mitandao ya simu kufanya malipo. Chama pia kinatambua kuwa kinatakiwa kutumia teknolojia mbalimbali ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma na kutekeleza shughuli zake. Hivyo

kitaendelea kubaini mahitaji ya teknolojia husika na kutafuta wazabuni wenye sifa. Chama kitatumia mashine za kisasa na teknolojia nyingine katika viwanda vitakavyojengwa ikiwemo kile cha kuzalisha mafuta ya kula ili kuzalisha bidhaa bora na pia katika hoteli na ukumbi wake. Haya yote yatasaidia kuimarisha ufanisi wa shughuli mbalimbali katika miradi husika na kuhimili ushindani. Kwa upande wa ubora wa bidhaa, Chama kitahakikisha kinafuata viwango vya ubora vya kitaifa na kimataifa kwa bidhaa kutoka katika kiwanda chake.

Katika shughuli za kila siku, Chama kinatambua umuhimu wa kuwa na mifumo ya uhakika ya TEHAMA. Chama kitaboreha mfumo wa kielektroniki ulioko wa uhasibu na fedha, kuanzisha tovuti ya Chama na kuimarisha matumizi ya mitandao ya kijamii na uwezo wa kudhibiti vihatarishi katika TEHAMA ikiwemo udukuzi wa taarifa na mifumo. Chama kitaendelea kutenga fedha za kutosha na kushirikiana na wadau wake ili kupata teknolojia rafiki kwa shughuli zake na zile za Wanachama. Kwa mradi wa usafirishaji, Chama kitahakikisha kinanunua magari ya kisasa yenye uwezo mkubwa wa kubeba mazao na mizigo mingine. Kwa sehemu kubwa, teknolojia muhimu zinazohitajika na Chama na Wanachama zinapatikana kutoka kwa wauzaji na watoa huduma walioko ndani ya nchi.

#### 2.7.2.6 Mazingira ya Sera, Sheria na Kanuni

Siku zote, uwepo wa Sera, Sheria na Kanuni rafiki huwezesha ukuaji wa ushirika nchini. LMCU Ltd inatambua kuwa inawajibika kufanya shughuli zake kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali za nchi. Hivyo wakati wote, Chama kinajiendesha kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika na miongozo mingine inayotolewa mara kwa mara na Mamlaka mbalimbali za Serikali. Kwa miaka mingi Serikali imeendelea kuweka mazingira bora ya Sera, Sheria, Kanuni na miongozo kwa maendeleo ya Vyama vya Ushirika na kilimo na kufanya kazi kwa ukaribu na Vyama. Wakati wa kutekeleza Mpango Mkakati huu, Chama kitafanya kazi kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni na miongozo mingine. Chama pia kitashiriki katika mijadala na michakato ya wadau ya kushauri Serikali na Mamlaka zake kuhusu maboresho ya Sera, Sheria, Kanuni na miongozo mingine. Ushiriki huu unaweza kuwa wa moja kwa moja au kupitia majukwaa ya wadau. Chama pia kitakuwa kikihuisha na kutunga sera na miongozo mingine ya ndani kulingana na mahitaji yake.

#### 2.7.2.7 Mazingira ya Asilia

Kwa miaka mingi kumekuwa na wito wa Serikali na wadau wengine nchini na duniani kwa ujumla unataka shughuli za maendeleo kwenda sambamba na utunzaji wa mazingira. Msisitizo ni kuwa mazingira yatunzwe kwa faida sasa na baadae. Chama, Wanachama na wakulima wake wanatambua

kuwa wakati wote wanatakiwa kutunza mazingira wakati wa kutekeleza shughuli zao za kiuchumi ikiwemo kilimo, viwanda n.k. Hadi sasa eneo la Chama lina hali nzuri ya hewa ikiwemo mvua za kutosha na kiwango kidogo cha uharibifu wa mazingira (misitu) na ukame.

Wakati wa kutekeleza Mpango Mkakati huu, Chama kitaweka juhudi za kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za kilimo kwa mazao yote kutoka kwa Wanachama na wakulima na utunzaji wa mazingira. Chama kinatambua kuwa mikakati yake ya kuhamasisha ongezeko la uzalishaji wa mazao huweza kusababisha ukataji wa miti kuanzisha mashamba mapya na matumizi ya kemikali za kilimo. Chama kitatoa elimu endelevu ya kilimo (ikiwemo matumizi sahihi ya pembejeo, kutumia mbegu na miche bora), matumizi bora ya ardhi na utunzaji wa mazingira. Chama kitajenga miundombinu na kuweka vifaa muhimu katika Ofisi na miradi yake ikiwemo mashamba na viwanda ili kuthibiti taka na kuzuia uchafuzi wa mazingira. Uhamasishaji wa Wanachama, Wakulima na jamii kwa ujumla utafanyika kuhusiana na uoteshaji wa miti rafiki kwa mazingira.

## 2.8 Uchambuzi wa Wadau wa Chama na Kujenga Mahusino

### 2.8.1 Uchambuzi wa Wadau

Tangu kuanzishwa kwake, Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao Ltd kimefanikiwa kutekeleza shughuli zake kupitia ushirikiano na wadau mbalimbali. Hivyo katika kutekeleza Mpango Mkakati huu, Chama kitaendelea kufanya kazi na wadau hao na kutafuta wadau wengine wapya. Sehemu hii imefanya uchambuzi wa wadau mbalimbali wa ndani na nje ya Chama ambao wanahitajika zaidi katika kutekeleza Mpango Mkakati huu. Uchambuzi huo umeoneshwa katika Jedwali Na. 9. Jumla ya wadau muhimu ishirini na moja (21) wamebainika.

### 2.8.2 Kuanzisha na Kuendeleza Uhusiano na Wadau

Chama kinatambua kuwa kina wajibu wa kuanzisha na kuendeleza mahusiano na wadau mbalimbali. Hivyo katika kutekeleza Mpango Mkakati huu, Chama kitaendelea kubaini wadau wapya na kuanzisha uhusiano nao. Chama kitaimarisha mahusiano na wadau wake wote kwa manufaa ya pande zote. Baadhi ya mikakati ya kuanzisha na kukuza mahusiano hayo ni pamoja na kutumia huduma wanazozitoa, kuwatembelea na kuwashirikisha katika mambo mbalimbali ya Chama ikiwemo mikutano, vikao vya Bodi au Menejimenti na matukio ya hisani/kijamii. Aidha katika mahusiano hayo, Chama kitahakikisha kuwa maslahi yake na yale ya Wanachama na wakulima yanalindwa.

**Jedwali Na. 9: Uchambuzi wa Wadau Muhimu wa Chama**

| Na. | Mdau | Umuhimu wake | Matarajio | Madhara endapo matarajio hayo hayatafikiwa | Mikakati ya Kutekeleza |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Wanachama | Hutoa maamuzi ya juu katika Chama, kuchangia mtaji na kuidhinisha matumizi ya rasilimali<br>Watumiaji wa huduma, wamiliki na wanufaika wa huduma na uwekezaji unaofanywa na Chama | Kupata huduma bora kukidhi mahitaji yao<br>Kupata masoko mazuri ya mazao mbalimbali<br>Bodi na watendaji wanakuwa wabunifu wa miradi na huduma ili kukuza faida | Malalamiko na migogoro katika Chama<br>Ushiriki hafifu katika maendeleo ya Chama | Chama kitahakikisha kuwa wakati wote kinatoa huduma nzuri kwa Wanachama na wakulima ikiwemo pembejeo, masoko na elimu. Pia kitawahamasisha watumie huduma zinazotolewa na Chama. |
| 2 | Bodi | Kusimamia shughuli za kila siku za Chama na kubuni miradi, sera na mipango ya maendeleo<br>Kushawishi Wanachama kuidhinisha matumizi ya rasilimali na kufanya uwekezaji | Kupata rasilimali za kutosha kutekeleza Mpango Mkakati huu na shughuli nyingine na kupata ushirikiano mzuri kutoka kwa Wanachama, Wakulima na watendaji wa Chama<br>Mafanikio ya Mpango Mkakati na shughuli nyingine za maendeleo ya Chama na kuacha alama ya uwepo wao | Kuwakatisha tamaa Wanachama na kupoteza uaminifu kwao<br>Kuwajibishwa na Wanachama | Chama kitaendelea kujenga uwezo wa wajumbe wa Bodi katika kusimamia Chama, miradi na shughuli za kila siku, ubunifu na kuandaa mipango na miongozo mbalimbali. |
| 3 | Menejimenti<br>(watendaji) | Hutekeleza majukumu ya kila siku ya Chama ili kufikia malengo ya Chama na mipango ya Bodi | Kupewa rasilimali za kutosha kutoka kwa Bodi ili kutekeleza majukumu yao<br>Mafanikio ya mipango ya Chama, uhakika wa ajira na kupata motisha kwa utendaji kazi mzuri | Hofu juu ya usalama wa ajira zao na kuharibu mahusiano mazuri na Bodi na Wanachama | Chama kitaendelea kuweka mazingira mazuri ya kazi ikiwemo maslahi ya watendaji na vitendea kazi na kutoa mafunzo endelevu ili kuwawezesha watendaji kuwajibika ipasavyo, kuwa wabunifu na kufanikisha malengo ya Chama |
| 4 | TCDC na Ofisi za Ushirika Wilaya | Uhamasishaji, uandikishaji, ushauri na usimamizi wa Chama na Wanachama wake | Chama na Wanachama wake wanakuwa imara wakati wote kibiashara, uendeshaji na usimamizi kwa faida na tija. Pia | Kushindwa kufanikisha malengo ya taasisi kuhusu kuimarisha usimamizi na maendeleo ya Ushirika nchini | Chama kitaendelea kufanya kazi kwa ukaribu na TCDC na Maafisa Ushirika wa Halmashauri zote na kufuata |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Chama na Wanachama wanazingatia Sera, Sheria na Kanuni za Ushirika na miongozo mingine ya ndani na nje | na kutokuwa na uhusiano mzuri na Chama | maagizo yao au ushauri. Pia kitahakikisha kuwa kinafuata Sheria, Kanuni na Miongozo mingine ya Ushirika na ile ya ndani. |
| 5 | Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC) | Msemaji mkuu wa Vyama vya Ushirika nchini na mwakilishi wao katika masuala mbalimbali kitaifa na kimataifa. Pia hutetea maslahi ya Vyama vya Ushirika | Chama na Wanachama wanakuwa imara kibiashara na kuzalisha faida pamoja na kuinua uchumi wa Wanachama na wakulima.<br><br>Chama kinashiriki mikutano, kuchangia ada na kuwa mstari wa mbele kuendeleza ushirika nchini | Kushindwa kufikia malengo yake ya kujenga ushirika wenye nguvu nchini na hata kuharibu taswira nzuri kwa wadau wengine na kutokuwa na uhusiano mzuri na Chama | Chama kitaendelea kufanya kazi kwa ukaribu na TFC |
| 6 | Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) | Msimamizi mkuu wa tasnia ndogo ya korosho nchini. Pia hutoa miongozo, kuratibu masoko, uwekezaji na kuhamasisha ukuaji wa tasnia hiyo. | Chama kinaimarisha uzalishaji na ubora wa korosho pamoja na kuwekeza kwenye uongezaji wa thamani wa zao hilo. | Kushindwa kufikia malengo ya kuwepo wake na kusaidia mkakati wa Serikali kuongeza uzalishaji, ubora na uongezaji wa thamani wa zao la korosho nchini. Pia kunaweza kuathiri uhusiano mzuri ulioko kati ya Chama na Bodi hiyo. | Chama kitafanya kazi kwa ukaribu na Bodi ya Korosho (CBT) katika masuala mbalimbali |
| 7 | Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) | Mhamasishaji na mdhibiti wa uzalishaji na ubora wa nafaka na mazao mengine, uongezaji thamani, kusimamia uhifadhi na kuratibu masoko | Chama kinazalisha kwa wingi na ubora mazao mbalimbali, kuuza kwa mfumo rasmi, kuongeza thamani mazao husika na kufuata miongozo iliyoko | Kushindwa kufikia malengo ya kuwepo kwake na kusaidia mkakati wa Serikali kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali ikiwemo ufuta, mbaazi, choroko, alizeti n.k.<br><br>Pia kunaweza kuathiri uhusiano mzuri ulioko kati ya Chama na Bodi hiyo. | Chama kitafanya kazi kwa ukaribu na COPRA katika kuhamasisha uzalishaji wa mazao mbalimbali ya kibiashara. Pia kitawekeza katika kiwanda kuongeza thamani ya alizeti na ufuta. |
| 8 | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) | Kufanya tafiti za mazao mbalimbali na pamoja kuzalisha mbegu bora za mazao na miche ya korosho. Pia kuhamasisha, kutoa elimu na ushauri juu ya | Chama na Wanachama wanatumia mbegu bora za mazao husika na miche bora ya korosho, matumizi ya mbinu bora za | TARI itashindwa kufikia lengo lake kusaidia kukuza uzalishaji wa mazao husika. Chama pia kitashindwa kufanikisha uzalishaji | Chama kitashirikiana kwa ukaribu na TARI katika kuhamasisha Wanachama na wakulima na kutumia mbegu bora za mazao na miche bora |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kilimo bora | kilimo na kuongeza uzalishaji | mkubwa wa mazao ya kibiashara | ya korosho |
| 9 | Shirika la Ukaguzi wa Hesabu na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) | Kufanya ukaguzi wa shughuli za Chama ikiwemo fedha, mali na masuala ya uongozi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo iliyoko | Chama kinaandaa taarifa za fedha na taarifa nyingine kwa wakati na ubora na kuzipeleka kukaguliwa. Pia Chama kinaendelea kutumia huduma za COASCO wakati wote | Kuongeza ugumu wa kufanya ukaguzi, kuathiri kufika malengo ya kitaasisi na kuathiri uhusiano mzuri na Chama | Chama kitahakikisha wakati wote kinaandaa taarifa za fedha na za kiutendaji kwa wakati na kwa viwango sahihi na kukaguliwa. Chama kitafanyia kazi kwa wakati dosari zote za ukaguzi. |
| 10 | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri za Lindi Manispaa, Mtama na Kilwa | Wasimamizi wakuu wa shughuli zote za kimaendeleo katika Mkoa, Wilaya na Halmashauri husika na pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa Chama, Wanachama na wakulima kufanya shughuli zao kwa ufanisi. Pia husaidia kuhamasisha uzalishaji wa mazao mbalimbali na kuwezesha huduma za ugani | Chama kinasimamia vyema uzalishaji wa mazao ya kibiashara kutoka kwa Wanachama na wakulima, kutoa huduma nzuri na kuboresha kipato cha Wanachama na wakulima na kusaidia maendeleo ya jamii<br><br>Chama kinalipa ushuru stahiki wa Halmashauri kwa wakati | Kukwamisha jitihada za Mkoa na Halmashauri zake katika kuhudumia wananchi, kufikia malengo ya uzalishaji na kupunguza umaskini<br><br>Kukosa mapato ya kutosha | Chama kitafanya kazi kwa ukaribu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri zote katika eneo lake |
| 11 | Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) | Kutoa huduma za elimu, mafunzo, utafiti na ushauri kuimarisha Vyama vya Ushirika nchini | Chama kinakuwa imara kibiashara na usimamizi wa shughuli za kila siku kwa kufuata misingi ya ushirika, weledi na kuhimili ushindani<br><br>Kuwa moja ya Vyama Vikuu vya mfano vinavyonufaika na uwepo wa Chuo | Chuo kitashindwa kufikia lengo lake la kuwa taasisi tegemeo katika kuimarisha ushirika nchini kupitia elimu, mafunzo, tafiti na ushauri wa kitaalam. Pia Chama kinaweza kushindwa kufikia malengo yake kwa kukosa elimu na ushauri sahihi. | Chama kitafanya kazi kwa ukaribu na Chuo kupitia Ofisi yake ya Mtwara na Lindi ili kupata elimu na mafunzo, ushauri wa kitaalam na huduma za utafiti, kuandaa sera mbalimbali na huduma za elimu kwa Wanachama na wakulima |
| 12 | Shirika la Viwango vya Bidhaa (TBS) | Husimamia na kushauri kuhusu masuala ya ubora na viwango vya bidhaa mbalimbali nchini. Pia hutoa leseni ya uendeshaji na mafunzo ya ubora kwa wazalishaji wa bidhaa mbalimbali nchini. | Chama kinazingatia ubora wa bidhaa vinazozalishwa kwa viwango vinavyostahili. | Chama kinaweza kupata changamoto za kuuza bidhaa zake kama hazitazingatia viwango vya ubora | Chama kitafanya kazi kwa ukaribu na TBS, kutumia huduma zake na pia kitazingatia viwango vya ubora wa bidhaa wakati wote |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 13 | Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA) | Husimamia masuala ya vipimo vya bidhaa na ubora wa vifaa vya kupima uzito na kutoa elimu na ushauri katika masuala husika | Chama kinasimamia viwango sahihi vya vipimo katika mazao na bidhaa zitakazozalishwa ikiwemo mizani na vifungashio vinavyokubalika | Kushindwa kuzingatia vipimo katika kupima mazao na bidhaa za kiwandani au kutumia vifaa visivyo sahihi kunaweza kusababisha Chama kuchukuliwa hatua za kisheria | Chama kitafanya kazi kwa ukaribu na WMA na kuzingatia viwango sahihi vya vipimo na kutumia vifaa sahihi |
| 14 | Mamlaka ya Mapato (TRA) | Kutoa elimu ya ulipaji wa kodi, kufanya makadirio ya kodi, kukusanya kodi na kusimamia Sheria husika | Chama kinafanya kazi katika mazingira ya uwazi na kulipa kodi zote kwa mujibu wa Sheria na miongozo | Mamlaka kukosa mapato ya kutosha na kutokuwa na mahusiano mazuri na Chama<br>Chama huweza kuwajibishwa kisheria hivyo kuathiri uendeshaji wa shughuli zake | Chama kitaandaa vyema taarifa zake za fedha na kulipa kodi stahiki wakati wote |
| 15 | Mamlaka za Maji Safi na Mazingira | Husimamia utunzaji wa mazingira, vyanzo vya maji na usambazaji wa maji | Chama kinatumia huduma za maji katika ofisi zake, viwanda na miradi mingine. Pia Chama kinatunza mazingira na vyanzo vya maji katika eneo lake la kazi | Chama kinaweza kushindwa kupata huduma endelevu ya maji kwa shughuli zake za kila siku na viwandani | Chama kitafanya kazi kwa ukaribu na taasisi hizi, kitatunza vyanzo vya maji na kutumia huduma zake pamoja na kulipa gharama husika kwa wakati. Pia kutunza mazingira na vyanzo vya maji. |
| 16 | Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) | Husimamia uzalishaji na usambazaji wa nishati ya umeme na ushauri husika | Chama kinatumia vyema nishati ya umeme katika viwanda, matumizi ya ofisi na miradi mingine na pia kutumia huduma nyingine za ushauri | Kukosekana kwa nishati hii huweza kuathiri uzalishaji wa bidhaa katika kiwanda na shughuli nyingine za kila siku | Chama kitatumia huduma za Shirika hili ikiwemo ushauri na ufungaji wa mfumo wa umeme katika viwanda, matumizi rafiki ya umeme na kulipa ankara wakati. |
| 17 | Taasisi za Fedha na Makampuni ya Mitandao ya Simu | Kupokea na kuhifadhi fedha za Chama na Wanachama kwa usalama na kuwalipa wakulima.<br>Kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha za kutekeleza miradi na shughuli za kila siku za Chama na Wanachama | Chama kinaendeleza mahusiano mazuri yaliyopo na kuendelea kutumia huduma zao | Huweza kuathiri urahisi wa Chama, wanachama na wakulima kufanya miamala mbalimbali kwa urahisi na huduma nyingine za kifedha | Chama kitaendelea kutoa kufanya kazi na mabenki na Makampuni ya Mitandao ya Simu |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 18 | Wasafirishaji | Kutoa huduma ya usafirishaji wa mazao na bidhaa nyingine za Chama | Chama kinaendelea kutumia huduma za wadau hawa kusafirisha mazao na bidhaa mbalimbali na kuwalipa kwa wakati | Huweza kuathiri usafirishaji wa mazao/malighafi na bidhaa kwa wakati | Chama kitaendelea kufanya kazi kwa ukaribu na wadau wanaotoa huduma za usafiri. Pia kitaendelea kuboresha mradi wake wa usafirishaji. |
| 19 | Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) | Husimamia uendeshaji wa mfumo wa stakabadhi ghalani ikiwemo kutoa leseni za uendeshaji wa maghala na kusimamia maghala husika | Chama na Wanachama wanafuata ipasavyo sheria, miongozo na taratibu zote za mfumo wa stakabadhi ghalani. Pia Chama kinatumia waendesha maghala wenye sifa na kufuata taratibu zote za uendeshaji wa maghala | Huweza kusababisha Chama kushindwa kuhifadhi mazao ya wakulima na kuendesha minada kama kikikiuka taratibu za mamlaka hiyo | Chama na Wanachama watazingatia matakwa yote ya mfumo wa stakabadhi ghalani. Pia kitashirikiana kwa ukaribu na WRRB katika utekelezaji wa shughuli zake. |
| 20 | Korosho Cooperative Joint Enterprise Enterprise (KCJE) Ltd | Msimamizi wa mfumo wa ununuzi mkubwa wa pamoja wa pembejeo, mabomba ya kupulizia madawa, magunia, mizani ya kidigitali na huduma mbalimbali kwa niaba ya Vyama Vikuu vya Ushirika vinavyojihusisha na zao la korosho | Chama kinakuwa mwanachama hai wa KCJE Ltd kushiriki ipasavyo katika shughuli zake na kutumia huduma zilizoko | Huweza kuathiri uwezo wa Chama kupata pembejeo, mabomba ya kupulizia madawa, magunia, mizani ya kidigitali na huduma nyingine kwa urahisi hivyo kuingia gharama kubwa | Chama kitaendelea kuwa mwanachama hai wa KCJE Ltd kwa kuwajibika ipasavyo ikiwemo kutumia huduma zote zinazotolewa |
| 21 | Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira | Msimamizi wa masuala ya mazingira nchini na mtoaji wa vibali vya ujenzi wa miradi | Chama kinafuata taratibu za kisheria kabla ya kujenga viwanda na miradi mingine na kuwa mstari wa mbele katika kutunza mazingira | Chama huweza kuchukuliwa hatua za kisheria na kuathiri uhusiano wake na NEMC | Chama kitafanya kazi kwa ukaribu na NEMC katika masuala ya miradi na utunzaji wa mazingira |
| | | | | | |

## 2.9 Uchambuzi wa Vihatarishi na Mpango wa Udhibiti

### 2.9.1 Aina za Vihatarishi

Vihatarishi ni matukio au mambo yoyote yasiyoonekana au yasiyotarajiwa ambayo yakitokea yanaweza kuathiri uendeshaji na usimamizi wa shughuli za Chama. Vihatarishi hivyo vinaweza kusababishwa na vyanzo vya ndani au nje ya Chama. Katika kutekeleza Mpango Mkakati huu, Chama kinatambua uwezekano wa kukumbwa na vihatarishi mbalimbali hivyo hutakiwa kuweka mikakati ya kuvidhibiti. Katika sehemu hii, Chama kimebaini vihatarishi mbalimbali vilivyogawanywa katika makundi sita (6). Makundi hayo ni vihatarishi vya; uendeshaji, usimamizi wa fedha, masoko, menejimenti ya Chama, uzalishaji, mabadiliko ya sera, sheria na miongozo. Makundi na aina husika za vihatarishi vimeoneshwa katika Jedwali Na. 10.

**Jedwali Na. 10: Vihatarishi katika Utekelezaji wa Mpango Mkakati**

| Na. | Kundi la vihatarishi | Vihatarishi husika |
|---|---|---|
| 1 | Vihatarishi vya uzalishaji | Kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya kibiashara; Upungufu wa mvua na ukame; Mlipuko wa magonjwa na wadudu shambulizi katika mazao; Mwitikio mdogo wa wakulima kutumia mbinu bora za kilimo; Utunzaji hafifu wa mashamba ya wakulima; Ukosefu wa pembejeo za kutosha kwa bei nafuu na; Wakulima kujihusisha zaidi na mazao mengine yasiyohusiana na Chama |
| 2 | Vihatarishi vya uendeshaji | Uhaba wa vifungashio (magunia na viroba) vya kuhifadhia mazao; Umakini mdogo katika kupima mazao ya wakulima; Ukaguzi duni wa ubora wa mazao, Kuharibika kwa magari ya usafirishaji na mashine katika kiwanda; Kupanda kwa bei za mafuta (na vipuri, vilainishi n.k) kwa matumizi ya kiwanda na magari; Ajali za watumishi na majanga mengine kiwandani na kwenye magari; Upotevu wa mazao ghalani na bidhaa zilizozalishwa kiwandani; Uhaba wa vifungashio vya bidhaa zinazozalishwa kiwandani; na Uhaba wa malighafi za kutosha kiwandani |
| 3 | Vihatarishi vya usimamizi wa fedha | Upotevu na usimamizi mbaya wa fedha; Uandishi wa taarifa za fedha bila kuzingatia viwango sahihi vya kihasibu na fedha; Gharama kubwa za uendeshaji wa biashara; Utunzaji hafifu wa taarifa za fedha na kumbukumbu nyingine; Uhaba wa rasilimali fedha za kutekeleza shughuli zilizopangwa; Ucheleweshaji wa malipo ya wakulima; na Uchelewaji wa wateja kulipia bidhaa walizonunua kiwandani. |
| 4 | Vihatarishi vya ki-menejimenti | Ufanisi mdogo wa kazi miongoni mwa watendaji; Muingiliano wa majukumu kati ya Bodi na Watendaji; Uchelewaji wa kushughulikia mahitaji ya bidhaa kutoka kwa wateja; Upoteaji wa bidhaa wakati wa kusafirisha kwenda sokoni (kwa wateja); Udukuzi wa taarifa za kielektroniki na mifumo ya TEHAMA; Usimamizi duni wa Bodi katika shughuli za Chama; na Udhibiti hafifu wa ubora wa malighafi na bidhaa |
| 5 | Vihatarishi katika masoko | Kupanda kwa bei ya malighafi; Kushuka kwa bei ya bidhaa sokoni; Kukua kwa ushindani kutoka kwa wazalishaji/wauzaji wengine wa bidhaa; Ukuaji mdogo wa masoko ya ndani; na Kuongezeka kwa uingizaji wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Vihatarishi kutokana na Sera, Sheria na miongozo | Uwepo wa Sera, Sheria au Kanuni zisizokuwa rafiki kwa maendeleo ya ushirika na biashara zake; na Uwepo wa miongozo/maagizo yasiyo rafiki kwa uendeshaji na usimamizi wa Chama |

### 2.9.2 Uchambuzi wa Vihatarishi na Mpango wa Udhibiti

Baada ya kubaini vihatarishi hivi, Bodi na Menejimenti ya LMCU Ltd imefanya uchambuzi wa kila kihatarishi. Uchambuzi huo umeangalia uwezekano wa kutokea kwa kila kihatarishi, athari endapo kikitokea na mikakati ya udhibiti wake. Katika Kutekeleza Mpango Mkakati huu, Meneja Mkuu ataandaa rejesta ya kuweka kumbukumbu ya vihatarishi vilivyotokea. Uchambuzi wa vihatarishi na mikakati ya udhibiti umefanywa kupitia Jedwali Na. 11.

**Jedwali Na. 11: Mpango wa Udhibiti wa Vihatarishi**

| **Na.** | **Kundi la vihatarishi** | **Vihatarishi husika** | **Uwezekano wa kutokea** | | | | | **Uwezo wa kuathiri Chama** | | | | | **Mikakati ya kutekeleza** | **Mhusika** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **5** | **4** | **3** | **2** | **1** | **5** | **4** | **3** | **2** | **1** | | |
| 1 | Vihatarishi vya uzalishaji | Kupungua kwa kiasi cha uzalishaji wa mazao makuu ya kibiashara | | | | | | | | | | | Kuratibu upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakati na kuzisambaza kwa Wanachama na wakulima<br><br>Kuanzisha mfuko wa ndani wa pembejeo<br><br>Kuimarisha huduma za ugani na elimu kwa Wanachama<br><br>Kuanzisha mashamba darasa maeneo ya wakulima | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Wanachama |
| | | Upungufu wa mvua na ukame | | | | | | | | | | | Kuhamasisha uoteshaji wa mbegu bora za mazao zinazohimili ukame na mvua chache<br><br>Kuhamasisha uoteshaji wa miche bora ya korosho inayohimili ukame na mvua chache | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | Mlipuko wa magonjwa na wadudu shambulizi kwa mazao | | | | | | | | | | | Kuimarisha upatikanji wa viuatilifu vyenye ubora kwa wakati<br><br>Kuimarisha huduma za ugani na elimu kwa Wanachama<br><br>Kuanzisha mashamba darasa maeneo wa wakulima<br><br>Kuweka mfumo wa ufuatiliaji wa hali za mashamba ya wakulima | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Wanachama |
| | | Mwitikio mdogo wa wakulima katika kutumia mbinu bora za kilimo | | | | | | | | | | | Kuelimisha wakulima kuhusu matumizi ya mbinu bora za kilimo kwa mazao yote ya kibiashara | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | Kufanya ufuatiliaji wa wakulima wote waliopewa mbegu za mazao mbalimbali na miche ya korosho ili kuhakikisha wanaotesha kwa wakati na wanatunza mashamba vizuri<br><br>Kuimarisha upatikanaji wa huduma za ugani | Wanachama |
| | | Utunzaji duni wa mashamba miongoni mwa wakulima | | | | | | | | | | | Kuelimisha wakulima kuhusu utunzaji wa mashamba<br><br>Kuimarisha huduma za ugani kwa wakulima | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Wanachama |
| | | Ukosefu wa pembejeo bora za kutosha kwa bei nafuu | | | | | | | | | | | Kuanzisha mfuko wa ndani wa pembejeo<br><br>Kuratibu upatikanaji wa pembejeo bora na za kutosha kwa wakati | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Wanachama |
| | | Baadhi ya wakulima kujihusisha zaidi na mazao mengine yasiyohusiana na Chama | | | | | | | | | | | Kuhamasisha wakulima kulima zaidi mazao ya kibiashara yanayohusiana na Chama na kuwaelimisha faida zake kiuchumi<br><br>Kuwaelimisha wakulima kuhusu matumizi bora ya ardhi kwa kilimo endapo wanahitaji kuzalisha mazao mengine | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Wanachama |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| 2 | Vihatarishi vya uendeshaji | Uhaba wa malighafi (mazao) za kutosha kwa ajili ya kiwanda | | | | | | | | | | | Kushirikiana na Wanachama na kuweka mfumo mzuri wa kukusanya mazao kutoka kwa wakulima<br><br>Kuajiri watendaji wa kutosha kusimamia manunuzi ya mazao<br><br>Kununua malighafi (mazao) ya kuzalishia bidhaa kwa wingi wakati mavuno na kuhifadhi ghalani ikiwemo alizeti na ufuta | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Wanachama |
| | | Uhaba wa vifungashio vya kuhifadhia mazao | | | | | | | | | | | Kubaini mahitaji ya magunia na viroba kabla ya kuanza msimu wa manunuzi ya mazao | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | Kuratibu manunuzi wa magunia na viroba kwa wakati | |
| | | Upotevu wa mazao ghalani na bidhaa zilizozalishwa kiwandani | | | | | | | | | | | Kuimarisha ulinzi katika maghala ya mazao na stoo ya kuhifadhia bidhaa kutoka kiwandani<br><br>Kudhibiti watu wasiohusika kuingia maeneo ya kiwanda na maghalani<br><br>Kutunza vizuri kumbukumbu za bidhaa zilizozalishwa na mazao yaliyohifadhiwa ghalani | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | Majanga ya moto kwenye majengo ya Chama | | | | | | | | | | | Kukinga majengo na mali nyingine za Chama kwa bima<br><br>Kufanya ukaguzi wa mifumo ya umeme na mitambo mara kwa mara<br><br>Kuweka vifaa vya kuzimia moto na milango ya dharura katika majengo ya Chama na kutoa mafunzo ya usalama kwa watendaji<br><br>Kuandaa mwongozo wa usalama kazini | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | Umakini mdogo katika kupima mazao yanayonunuliwa | | | | | | | | | | | Kupima kwa umakini na kutunza kumbukumbu za mazao yaliyonunuliwa kila wakati kwa kutumia mizani yenye sifa. | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Wanachama |
| | | Ukaguzi duni wa ubora wa malighafi (mazao) | | | | | | | | | | | Kukagua unyevu na usafi wa mazao yote yaliyonunuliwa kabla ya kuyasafirisha au kuyapeleka kiwandani | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Wanachama |
| | | Kuharibika kwa mashine kiwandani na magari ya usafirishaji | | | | | | | | | | | Kufanya ukaguzi na matengenezo ya mashine na magari kwa wakati<br><br>Kuajiri watendaji wenye weledi wa ufundi wa mashine na magari | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | Kuwa na hifadhi ya vipuri vya mashine na magari wakati wote | |
| | | Kupanda kwa bei za mafuta (na vipuri, vilainishi n.k) kwa ajili ya kiwanda na magari | | | | | | | | | | | Kuingia mikataba na wauzaji wa mafuta, vipuri na bidhaa nyingine muhimu ili kuwa na uhakika wa kupata bidhaa hizo wakati wote kwa bei nafuu | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | Ajali za watumishi kiwandani, ofisini na mradi wa usafirishaji | | | | | | | | | | | Kuwapa watumishi wote vifaa vya kujikinga wanapokuwa kiwandani na maeneo mengine<br><br>Kuelimisha watendaji masuala ya usalama eneo la kazi<br><br>Kuelimisha madereva kuzingatia Sheria za usalama barabara na uendeshaji kwa umakini | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | Uhaba wa vifungashio vya kutosha kwa bidhaa zinazozalishwa | | | | | | | | | | | Kubaini wazalishaji wakubwa wa vifungashio na kuingia nao mikataba ili kuwa na uhakika wa malighafi hizo | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| 3 | Vihatarishi vya usimamizi wa fedha | Upotevu au usimamizi hafifu wa fedha | | | | | | | | | | | Kuzingatia taratibu za kifedha wakati wa kufanya miamala<br><br>Kuhuisha Sera ya uhasibu na fedha<br><br>Kuzingatia bajeti ya Chama iliyoidhinishwa | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | Uandishi wa taarifa za fedha bila kuzingatia viwango sahihi | | | | | | | | | | | Kuhakikisha kuwa taarifa za fedha zinaandaliwa kwa viwango vinavyotakiwa<br><br>Kutoa mafunzo ya rejea ya uhasibu na fedha kwa watendaji husika | Meneja Mkuu |
| | | Utunzaji hafifu wa taarifa za fedha na kumbukumbu nyingine | | | | | | | | | | | Kutunza kumbukumbu za fedha na kuandika taarifa za fedha kwa wakati<br><br>Kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA kutunza taarifa za fedha | Meneja Mkuu |
| | | Ucheleweshaji wa malipo ya wakulima | | | | | | | | | | | Kuhakiki na kuwalipa wakulima kwa wakati | Bodi |

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | | Meneja Mkuu |
| | | Uhaba wa rasilimali fedha za kutekeleza shughuli zilizopangwa | | | | | | | | | | | Kuandaa na kuzingatia bajeti ya utekelezaji ya shughuli muhimu kila mwaka<br><br>Kubaini vyanzo vipya vya mapato kutoka ndani au nje ya Chama | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | Gharama kubwa za uendeshaji wa biashara | | | | | | | | | | | Kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa<br><br>Kuzingatia Sera ya uhasibu na fedha katika kufanya matumizi<br><br>Kubainisha mambo yanayotumia gharama kubwa na kuweka mikakati ya kupunguza matumizi | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | Uchelewaji wa baadhi ya wateja kulipia bidhaa walizonunua | | | | | | | | | | | Kuwasiliana mara kwa mara na wateja wanaochukua bidhaa kwa makubaliano maalum ya malipo<br><br>Kuweka utaratibu mzuri wa kupokea malipo kutoka kwa wateja husika | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| 4 | Vihatarishi vya ki-menejimenti | Ufanisi mdogo wa kazi miongoni mwa watendaji | | | | | | | | | | | Kuandaa mpango kazi wa watendaji kila mwaka<br><br>Kuweka mfumo wa kupima ufanisi wa watendaji (*performance appraisal system*)<br><br>Kujenga uwezo wa watendaji kuhusu majukumu yao | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | Muingiliano wa majukumu kati ya Bodi na watendaji | | | | | | | | | | | Kuandaa mwongozo wa mamlaka ya Bodi (*Board charter*)<br><br>Kuhuisha Masharti ya Chama kuonesha mipaka ya kimajukumu kati ya Bodi na watendaji na mambo mengine | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | Uchelewaji wa kushughulikia mahitaji ya bidhaa kutoka kwa wateja | | | | | | | | | | | Kuweka vizuri kumbukumbu za mahitaji ya wateja<br><br>Kuzalisha na kusambaza bidhaa kwa wakati | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | kwenda kwa wateja | |
| | | Upoteaji wa bidhaa na mazao wakati wa kusafirisha | | | | | | | | | | | Kuweka mfumo imara wa kusimamia usafirishaji wa bidhaa zinazozalizwa kiwandani na mazao ya wakulima<br><br>Kutunza vizuri kumbukumbu za bidhaa zote toka kiwandani na mazao yanayosafirishwa kila siku | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | Udukuzi wa taarifa za kielektroniki katika mifumo ya TEHAMA | | | | | | | | | | | Kuelimisha watendaji wote kuhusu matumizi ya mifumo TEHAMA na mbinu za kuhakikisha usalama wa taarifa za Chama<br><br>Kutumia mifumo migumu na milaini kama mbadala wa kuhifadhi taarifa (*backup system*)<br><br>Kuajiri watendaji wenye sifa kusimamia mifumo na masuala yote ya TEHAMA<br><br>Kuandaa Sera ya TEHAMA | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | Usimamizi duni wa Bodi na watendaji wa ngazi za juu katika shughuli za Chama | | | | | | | | | | | Kujenga uwezo wa Bodi na watendaji wa ngazi za juu kuhusu usimamizi wa biashara, mali, miradi na shughuli za kila siku za Chama<br><br>Kuweka mfumo wa kupima ufanisi wa utendaji wa Bodi na watendaji<br><br>Kuandaa mipango kazi ya mwaka ya Bodi na watendaji | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | Udhibiti hafifu wa ubora wa bidhaa toka kiwandani | | | | | | | | | | | Kuandaa mwongozo wa usimamizi wa shughuli za kiwanda ikiwemo ubora wa bidhaa<br><br>Kuzingatia viwango vya ubora wa bidhaa na usafi wa mazingira wakati wote<br><br>Kujenga uwezo wa watendaji husika | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | kusimamia ubora wa bidhaa | |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| 5 | Vihatarishi katika masoko | Kupanda kwa bei ya malighafi | | | | | | | | | | | Kufuatilia mara kwa mara mwenendo wa bei za malighafi sokoni<br><br>Kununua kwa malighafi kwa wingi wakati wa mavuno bei zikiwa chini | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | Kushuka kwa bei za bidhaa sokoni | | | | | | | | | | | Kuzalisha bidhaa kwa kuzingatia mahitaji ya wateja walioko na mwenendo wa soko kwa ujumla pamoja na gharama za uendeshaji na faida tarajiwa | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | Ushindani kutoka kwa wazalishaji/wauzaji wengine wa mafuta ya kula | | | | | | | | | | | Kuzalisha kwa tija bidhaa nyingi zenye ubora ili kukidhi mahitaji ya soko na kuhimili ushindani bila kuongeza gharama za uendeshaji | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | Kuongezeka kwa uingizaji wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi | | | | | | | | | | | Kuimarisha juhudi za kutangaza bidhaa za Chama kwa wateja katika masoko mbalimbali<br><br>Kuzalisha bidhaa zenye ubora mzuri na kuziuza kwa bei nafuu kulingana na mwenendo wa soko<br><br>Kuelimisha jamii kuhusu faida za kiafya za bidhaa zinazozalishwa na Chama ukiliganisha na zile zinazotoka nje ya nchi | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| 6 | Vihatarishi kutokana na Sera, Sheria na miongozo | Uwepo wa Sera, Sheria au Kanuni zisizokuwa rafiki kwa maendeleo ya ushirika na biashara kwa ujumla | | | | | | | | | | | Kufanya ushawishi binafsi wa Chama na kwa kushirikiana na Vyama vya Ushirika vingine ili kuishauri Serikali na Mamlaka nyingine kuhusu masuala muhimu yanayoweza kustawisha Vyama vya Ushirika nchini na mambo yanayohitaji kuboreshwa wakati wa kuandaa au kuhuisha Sera, Sheria na Kanuni za ushirika, kilimo, biashara na masuala mengine. | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Wanachama |

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Uwepo wa miongozo au maagizo yasiyokuwa rafiki kwa uendeshaji na usimamizi wa Chama | | | | | | | | | | | Kufanya majadiliano binafsi moja kwa moja na Mamlaka zinazotoa miongozo au maagizo ili kupata suluhisho juu ya mambo ambayo huweza kuathiri ufanisi wa biashara au uendeshaji wa Chama kwa ujumla<br><br>Kushirikiana na wadau wengine katika kushauri maboresho au utekelezaji mzuri wa miongozo na maagizo kutoka mamlaka mbalimbali | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Wanachama |

**Tafsiri ya rangi na namba:** 1= Hakuna, 2= Mdogo sana (kijani), 3= Mdogo (bluu), 4=Mkubwa (njano) and 5= Mkubwa sana (nyekundu)

## SURA YA TATU

## MPANGO WA CHAMA KATIKA MIAKA MITANO IJAYO (2026/27 – 2030/31)

### 3.1 Tamko la Dira

Dira ya Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao Ltd ni "Kuwa Chama Kikuu kinachoaminika katika kuwezesha maendeleo endelevu ya Wanachama na Wakulima kupitia kilimo cha kibiashara".

### 3.2 Tamko la Dhamira

Dhamira/Dhima ya Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao Ltd ni "kuwaendeleza Wanachama na Wakulima ili kustawi kiuchumi na kijamii kupitia huduma bora, usimamizi mzuri, ubunifu na uwekezaji wa kimkakati katika sekta ya kilimo".

### 3.3 Kauli Mbiu

Kauli mbiu ya Chama ni "Lindi Mwambao, Maendeleo Daima"

### 3.4 Maadili

Wakati wa utekelezaji wa Mpango Mkakati huu, Chama kitazingatia maadili mbalimbali katika kuendesha shughuli zake za kila siku. Hii itasaidia pia kusimamia vyema mambo ambayo Chama kinayaamini. Maadili ya Chama yameelezewa katika Jedwali Na. 12.

**Jedwali Na. 12: Maadili ya Chama katika Kutekeleza Mpango Mkakati**

| Na. | Maadili | Tafsiri yake |
|---|---|---|
| 1 | **Ushirikiano** | Ili kupata mafanikio na kutimiza malengo yake, Chama kitahakikisha kunakuwa na ushirikiano mzuri wa wadau wote wa ndani na nje. Pia kila mdau ana wajibu wa kutoa ushirikiano pale inapohitajika. Chama kitahakikisha kinadumisha na kuanzisha uhusiano endelevu na wadau mbalimbali ili kutekeleza shughuli zake na kutatua changamoto zitakazojitokeza. |
| 2 | **Uadilifu** | Bodi na Menejimenti za Chama wanatambua umuhimu wa kuwa waadilifu wakati wote wanapotekeleza majukumu yao. Uadilifu husaidia kujenga imani kwa Wanachama na wakulima hivyo kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Chama ikiwemo kutumia huduma zinazotolewa. |
| 3 | **Haki na usawa** | Viongozi na watendaji wa Chama watahakikisha wanatenda haki katika kuwahudumia Wanachama. Chama hakitaruhusu upendeleo katika utoaji wa huduma, taarifa au fursa zozote kwa kuhakikisha Wanachama wanapata kile wanachostahili. Pia wakati wa kugawana ziada ya biashara, kila Mwanachama atapewa stahiki zake kwa kuzingatia ushiriki wake kwa shughuli husika. Chama |

| | | |
|---|---|---|
| | | kitazingatia pia usawa wa kijinsia na ushiriki wa vijana na wanawake katika uongozi wa Chama na Wanachama wake. |
| 4 | **Uwazi** | Chama siku zote kitaendesha shughuli zake kwa kuzingatia uwazi na kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyoko. Chama kitafikisha taarifa zote muhimu kwa Wanachama na Wakulima kwa wakati na kwa usahihi na kuweka njia rafiki kufikisha taarifa hizo. |
| 5 | **Uwajibikaji** | Viongozi, Menejimenti na Wanachama watawajibika kwa maslahi mapana ya Chama. Bodi na Menejimenti pia wanahitajika kuzingatia weledi katika kuendesha shughuli za Chama na kuweka na mfumo wa kupima ufanisi. Viongozi, Menejimenti na Wanachama wanatakiwa pia kuwa na moyo wa kujitolea kwa manufaa ya Chama. |
| 6 | **Kuijali jamii** | Chama kinatambua kuwa kina wajibu wa kuchangia maendeleo ya jamii kwa namna mbalimbali. Hivyo Chama kitahakikisha kuwa kinaendelea kutekeleza kwa vitendo msingi wa "ushirika kuijali jamii". Chama kitatenga sehemu ya ziada/mapato yake kusaidia shughuli za maendeleo ya jamii katika eneo lake la kazi. |
| 7 | **Demokrasia** | Chama kinatambua kuwa demokrasia ni moja ya nguzo muhimu kwa uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika. Hivyo Chama kitahakikisha kuwa misingi ya kidemokrasia inazingatiwa katika uendeshaji wa shughuli za kila siku. Demokrasia pia itazingatiwa katika kufanya maamuzi, chaguzi za Bodi za Chama na Wanachama wake na kuhakikisha maamuzi yote yanayofikiwa hayaathiri maslahi ya wachache. |
| 8 | **Ubunifu** | Chama kitahakikisha wakati wote kinakuwa na viongozi na watendaji wenye ubunifu wa mawazo, huduma, bidhaa na mikakati inayoweza kuleta ustawi zaidi kwa Chama. Pia Chama kitahakikisha kuwa kunakuwa na ubunifu katika uendeshaji na usimamizi wa Chama na AMCOS. |
| 9 | **Weledi katika utendaji kazi** | Chama kitahakikisha kuwa wakati wote kinafanya kazi kwa kuzingatia utaalam na sio kufanya vitu kwa maamuzi yasiyo na tija au maagizo kutoka nje. Chama kitahakikisha kuwa kinaajiri watendaji wa kutosha na wenye sifa sahihi katika nafasi husika. Chama kitaendelea kujenga uwezo wa wajumbe wa Bodi na watendaji ili kuweza kufanya maamuzi sahihi na kutekeleza ipasavyo majukumu yao. |
| | | |

### 3.5 Msingi ya Ushirika katika Uendeshaji na Usimamizi wa Chama

Katika kusimamia na kuendesha shughuli zake, Chama kitahkikisha kuwa kinafuata misingi saba (7) ya Vyama vya Ushirika iliyoasisiwa na Shirikisho la Ushirika Duniani (ICA). Misingi hiyo ni;

(i) Uanachama Ulio Wazi na wa Hiari
(ii) Udhibiti wa Wanachama Kidemokrasia
(iii) Ushiriki wa Wanachama Kiuchumi
(iv) Uhuru na Kujitegemea
(v) Elimu, Mafunzo na Taarifa
(vi) Ushirikiano miongoni mwa Vyama vya Ushirika
(vii) Ushirika Kuijali Jamii

### 3.6 Kanuni za Kimenejimenti Zitakazofuatwa

Katika utekelezaji wa Mpango Mkakati huu, Bodi na Menejimenti ya LMCU Ltd watafanya kazi kwa ufanisi na tija ili kufikia malengo yake na kukabiliana na mabadiliko mbalimbali katika mazingira ya kibiashara. Ili kufanikiwa haya, pamoja na mambo mengine, watahakikisha wanajiendesha kwa mfumo wa uendeshaji na usimamizi unaozingatia matokeo chanya (*result-based management*) ili kutoa huduma bora na endelevu kwa Wanachama. Hivyo Chama kitazingatia kanuni zifuatazo za kimenejimenti katika kuendesha na kusimamia shughuli zake;

(a) Kuendesha shughuli za Chama kwa kuzingatia mtazamo wa kuleta matokeo endelevu;
(b) Kutekeleza shughuli za Chama na utoaji wa huduma kwa kuzingatia manufaa makubwa kwa Wanachama na wakulima;
(c) Kujiendesha kimkakati kwa kupanga na kutekeleza shughuli zenye manufaa mapana kwa mtazamo wa muda mrefu kwa Chama, Wanachama na wakulima;
(d) Kuhakikisha kuwa shughuli zinazofanywa, huduma zinazotolewa na matokeo yake, vyote vinaakisi thamani ya fedha zilizotumika (*value for money*);
(e) Kujiendesha kwa kuzingatia ubunifu na uwajibikaji katika kutekeleza shughuli zote za Chama;
(f) Kuwashirikisha wadau katika ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa malengo, mikakati na shughuli za Chama; na
(g) Kulinda hadhi ya Chama na ushirika kwa ujumla katika kutekeleza shughuli za Chama

### 3.7 Vipaumbele vya Mpango Mkakati

Kupitia Mpango Mkakati huu, Chama kimeweza kubaini vipaumbele mbalimbali vitakavyotekelezwa kwa kipindi cha 2026/27 hadi 2030/31. Katika kipindi hiki, Chama kinalenga kutekeleza jumla ya vipaumbele tisa (9) ambavyo ni;

(i) Uanachama
(ii) Usimamizi wa huduma
(iii) Uzalishaji na ubora wa mazao
(iv) Masoko na uhusiano na wadau
(v) Usimamizi endelevu wa miradi na uwekezaji
(vi) Usimamizi wa fedha na mali

(vii) Uongozi, utawala bora na menejimenti ya rasilimali watu

(viii) Matumizi endelevu ya TEHAMA, na

(ix) Utunzaji wa mazingira asilia na kujali jamii

### 3.7.1 Kipaumbele Na. 1: Uanachama

Wanachama walianzisha Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao Ltd ili kuinua hali zao za kiuchumi na kijamii. Hivyo Wanachama ndio nguzo ya maendeleo ya Chama. Wanasaidia kufikisha huduma za Chama kwa Wakulima ikiwemo kuwezesha uzalishaji na ukusanyaji wa mazao, usambazaji wa pembejeo na huduma nyingine. Wanachama pia huchangia mtaji wa Chama, kuwajibika katika katika shughuli za Chama. Katika Mpango Mkakati huu, Chama kinalenga kuongeza idadi ya Wanachama kutoka 61 hadi 65 ifikapo 2030/31.

**Lengo la 1: Wanachama na wakulima wanaongezeka**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuongeza idadi ya Wanachama katika Chama | Wanachama wanaongezeka kutoka 61 hadi 65 ifikapo 2030/31 | Ongezeko la Wanachama, uzalishaji na mapato katika Chama |
| MK2 | Kuongeza idadi ya wakulima wanaojiunga uanachama katika AMCOS | Angalau 50% ya wakulima wanaohudumiwa na AMCOS wanajiunga uanachama ifikapo 2030/31 | Ongezeko la wakulima waliojiunga uanachama katika AMCOS na kukua kwa uzalishaji |
| | | | |

**Lengo la 2: Ufanisi wa uendeshaji wa AMCOS (Wanachama) unaimarishwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kujenga uwezo wa viongozi na watendaji wa AMCOS | Viongozi na watendaji wa AMCOS wanapata mafunzo ya kuimarisha usimamizi na uendeshaji angalau mara 1 kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa weledi na ufanisi miongoni mwa viongozi na watendaji wa AMCOS |
| | | Ufanisi wa kiutendaji kwa viongozi na watendaji wa AMCOS katika kutekeleza shughuli zao (mipango kazi) unafikia angalau 70% kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | |
| MK2 | Kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi muhimu katika AMCOS | Kuandaa na kuhuisha rejesta ya mahitaji ya vitendea kazi muhimu katika AMCOS kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa uwezo wa AMCOS kutoka huduma kwa wakulima |
| | | Vitendea kazi muhimu katika ofisi na maghala ya AMCOS vinakuwepo kwa angalau 80% ifikapo 2030/31 | |
| | | | |

**Lengo la 3: Ushiriki wa Wanachama katika shughuli za Chama unaimarishwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuboresha uhusiano kati ya Chama na Wanachama | Uhusiano mzuri kati ya Chama na Wanachama unaendelezwa hadi kufikia 2030/31 | Ushiriki mzuri wa Wanachama katika shughuli za Chama, kufanikisha malengo yaliyoko na ustawi wa Chama na Wanachama |
| MK2 | Kuimarisha utoaji wa taarifa muhimu kwenda kwa Wanachama na wakulima | Taarifa muhimu zinafika kwa Wanachama na Wakulima kwa wakati kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa uwazi wa taarifa na ushiriki mzuri wa Wanachama na Wakulima katika maendeleo ya Chama |
| MK3 | Kuendeleza utaratibu wa vikao kazi kati ya Chama na viongozi na watendaji wa AMCOS | Kila mwaka, vikao kazi kati ya Chama na viongozi na watendaji wa AMCOS vinafanyika kabla na baada ya msimu wa mazao hadi kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa ufanisi katika maandalizi na usimamizi wa msimu, utoaji huduma kwa wakulima na utatuzi wa changamoto husika kwa wakati |
| MK4 | Kuweka utaratibu wa kukusanya maoni kutoka kwa wakulima ili kuboresha Chama | Mfumo imara wa kukusanya maoni ya Wanachama ya kuboresha huduma za Chama unakuwepo na kutumika hadi kufikia 2030/31 | Maboresho ya uendeshaji na usimamizi wa shughuli na huduma katika Chama |
| MK5 | Kuendeleza uanachama wa Wanachama walioko | Wanachama wote wanaendeleza uanachama wao na kushiriki kikamilifu katika Chama hadi kufikia 2030/31 | Uwepo wa Wanachama wa kutosha na wawajibikaji na kufanikisha mipango na shughuli za Chama |
| MK6 | Kukuza uhusiano miongoni mwa Wanachama | Ushirikiano mzuri miongoni mwa Wanachama unaendelezwa wakati wote hadi ifikapo 2030/31 | Kukua kwa ushirikiano miongoni mwa Wanachama |
| MK7 | Kuendeleza utaratibu wa zawadi kwa Wanachama na wakulima wanaofanya vizuri katika mambo mbalimbali (mf: uzalishaji, hisa, miradi n.k) | Mfumo wa kutoa motisha au zawadi kwa Wanachama na wakulima unaendelezwa hadi kufikia 2030/31 | Hamasa ya kuongeza ufanisi wa utendaji kazi miongoni mwa Wanachama na Wakulima |
| | | | |

### 3.7.2 Kipaumbele Na. 2: Usimamizi wa Huduma

Tangu kuanzishwa kwake, Chama kimekuwa kikitoa huduma mbalimbali kwa Wanachama na wakulima. Chama kinatambua kuwa kina jukumu la kuendelea kutoa huduma bora na za uhakika kwa Wanachama na wakulima ili waweze kuona matunda ya uwepo wa Chama na kuchochea maendeleo yao. Katika Mpango Mkakati huu, Chama kitaendelea kuboresha utoaji wa huduma na kubuni huduma mpya zinazowalenga zaidi Wanachama na wakulima. Huduma bora zikiwepo husaidia kuongeza utiifu na ushiriki mzuri wa Wanachama na wakulima katika maendeleo ya Chama.

**Lengo la 1: Uwezo wa Chama katika utoaji wa huduma unaimarishwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuimarisha ufanisi wa Watendaji na viongozi wa Chama katika kutoa huduma kwa Wanachama | Viongozi na watendaji wa Chama wanapata mafunzo ya kuimarisha usimamizi na utoaji wa huduma kwa Wanachama na Wakulima angalau mara 1 kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa ufanisi katika kuhudumia Wanachama na wakulima, utiifu wao kwa Chama na ushiriki mzuri katika shughuli za maendeleo ya Chama |
| | | Ufanisi wa kiutendaji kwa viongozi na watendaji wa Chama katika kutekeleza shughuli zao (mipango kazi) unafikia angalau 90% kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | |
| MK2 | Kuweka mfumo endelevu wa kufuatilia na kutathmini hali ya utoaji huduma kwa Wanachama na wakulima | Ufuatiliaji na tathmini endelevu ya utoaji wa huduma inafanyika mara 2 kwa mwaka hadi ifikapo 2030/31 | Kubaini kwa wakati mafanikio na changamoto katika utoaji wa huduma na kuchukua hatua stahiki |
| MK3 | Kutenga rasilimali za kutosha kuimarisha utoaji wa huduma kwa Wanachama na Wakulima | Angalau 95% ya fedha zinazohitajika kutoa huduma kwa Wanachama na Wakulima zinakuwepo kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Kuimarika kwa uwezo wa kufukisha huduma muhimu kwa Wanachama na Wakulima |
| | | Angalau 80% ya watendaji wanaohitajika katika kutoa huduma kwa Wanachama na Wakulima wanakuwepo hadi kufikia 2030/31 | |
| MK4 | Kuendeleza uhusiano mzuri na watoa huduma wa Chama na Wanachama | Uhusiano mzuri kati ya Chama na w atoa huduma unakuwepo wakati wote na kuimarishwa hadi kufikia 2030/31 | Uhakika wa kufikisha huduma kwa Wanachama na wakulima kwa ufanisi |
| | | | |

**Lengo la 2: Upatikanaji wa huduma za msingi kwa Wanachama na Wakulima unaongezeka**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuratibu upatikanaji wa viuatilifu kwa wakati | Angalau 60% ya mahitaji ya viuatilifu (pembejeo) kwa Wanachama na wakulima yanafikiwa kila mwaka hadi ifikapo 2030/31 | Kuongezeka kwa uzalishaji na ubora wa mazao ya kibiashara |
| MK2 | Kuratibu upatikanaji wa vifungashio kwa wakati | Angalau 95% ya mahitaji ya vifungashio (magunia na viroba) kwa wanachama na wakulima yanafikiwa kila mwaka hadi ifikapo 2030/31 | Uhakika wa uwepo wa vifungashio na kuongezeka kwa uwezo wa kukusanya mazao na ubora |
| MK3 | Kuratibu huduma za huduma za mashine za kupulizia madawa shambani kwa wakati | Angalau 50% ya mahitaji ya mashine za kupulizia madawa mashambani yanafikiwa kila mwaka hadi ifikapo 2030/31 | Kuongezeka kwa uzalishaji na ubora wa mazao ya kibiashara ikiwemo korosho |
| MK4 | Kuratibu upatikanaji wa mizani ya kidijitali kwa wakati | Angalau mizani mpya 150 ya kidijitali inanunuliwa na kusambazwa kwa Wanachama kabla ya 2030/31 | Kuongezeka kwa uwazi na ufanisi katika kupima mazao yaliyokusanywa |
| MK5 | Kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wakulima | Angalau 60% ya wakulima katika AMCOS wanapata huduma ya bima ya afya ifikapo 2030/31 | Uwepo wa wakulima wengi wenye afya njema na wanaoweza kushiriki |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | ipasavyo katika uzalishaji na shughuli nyingine za maendeleo ya Chama na AMCOS zake |
| MK6 | Kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa Wanachama na Wakulima | SACCOS ya Wanachama inaanzishwa kabla ya Mei 2027 na kuhudumia Wanachama | Upatikanaji wa huduma za uhakika za kifedha kwa masharti nafuu hivyo kukidhi mahitaji ya Wanachama kwa wakati |
| | | Angalau 80% ya mahitaji ya kifedha ya Wanachama yanafikiwa kupitia SACCOS ya Chama na mabenki kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | |
| | | Angalau 60% ya mahitaji ya mikopo kwa wakulima yanafikiwa kila mwaka hadi ifikapo 2030/31 | Upatikanaji wa mikopo ya uhakika kwa wakulima na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya kibiashara |
| MK7 | Kuwezesha malipo ya wakulima na Wanachama kwa wakati | Kila mwaka, angalau 97% ya wakulima na Wanachama wanalipwa kwa wakati kila msimu wa minada hadi ifikapo 2030/31 | Upatikaanaji wa fedha kwa wakati kuwezesha utekelezaji wa shughuli zao za kimaendeleo na kuongezeka kwa imani yao kwa Chama na kushiriki ipasavyo |
| | | Kabla ya 2030/31, Ofisi 3 za Kanda zinajengwa ili kurahisisha malipo ya wakulima na utoaji wa huduma nyingine | Kuimarika kwa ufanisi katika malipo ya wakulima na utoaji wa huduma nyingine za Chama kwa urahisi kwenda kwa Wanachama, wakulima na wadau wengine |
| MK8 | Kuongeza uwezo katika kuhifadhi mazao ya Wanachama na wakulima | Maghala ya Chama na Wanachama yanakuwa na hali nzuri wakati wote kuwezesha uhifadhi salama wa mazao ya wakulima hadi kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa imani ya Wanachama na wakulima kwa Chama na uwezo wa kuhifadhi kiasi kikubwa cha mazao ya kibiashara |
| | | Ukarabati wa ghala kuu la Ilulu Mtama DC unafanyika kabla ya 2030/31 | |
| MK9 | Kuwezesha upatikanaji wa zana na teknolojia rafiki za kilimo kwa Wanachama na wakulima | Uratibu wa upatikanaji na usambazaji wa zana na teknolojia za kilimo kwa Wanachama na wakulima unafanyika kila inapohitajika hadi kufikia 2030/31 | Kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao |
| | | | |

### 3.7.3 Kipaumbele Na. 3: Uzalishaji na Ubora wa Mazao ya Kibiashara

Kwa sehemu kubwa, wakulima katika AMCOS ndio huhusika na uzalishaji wa mazao ya kibiashara yaani; korosho, ufuta na mbaazi. Chama kinafanya kazi ya kutoa huduma muhimu kuwezesha uzalishaji, uhifadhi, usafirishaji na uuzaji wa mazao husika. Kwa miaka ya karibuni, Chama na baadhi ya Wanachama wameanza kujihusisha na uzalishaji wa mazao hasa korosho kupitia mashamba yao.

Chama pia kimebaini uwepo wa mazao mengine ya kibiashara yanayozalishwa na wakulima hivyo kuna uhitaji wa kuweka mikakati ya kukuza uzalishaji wake ikiwemo alizeti na choroko.

**Lengo la 1: Uzalishaji na ukusanyaji wa korosho unaongezeka**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuratibu uzalishaji na uoteshaji wa miche bora ya korosho | Angalau miche bora ya korosho 100,000 inazalishwa na kuoteshwa kwa kila mwaka hadi 2030/31 | Kuongezeka kwa uzalishaji wa korosho ghafi kutoka kwa wakulima na Wanachama |
| MK2 | Kuratibu uboreshaji wa mikorosho ya zamani isiyozaa vizuri katika mashamba ya Wakulima | Angalau 50% ya mikorosho ya zamani katika mashamba ya wakulima inaboreshwa hadi kufikia 2030/31 | |
| MK3 | Kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima | Ufanisi katika utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima wa korosho unafikia angalau 50% ya wakulima kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | |
| MK5 | Kuongeza ukubwa wa mashamba yanayolimwa korosho katika eneo la Chama | Mashamba mapya yanayolimwa korosho yanaongezeka kwa angalau 20% kufikia 2030/31 | |
| MK6 | Kuongeza makusanyo ya korosho kutoka kwa Wanachama na wakulima | Makusanyo ya korosho ghafi yanaongezeka kutoka tani 43,000 hadi angalau tani 80,000 ifikapo 2030/31 | Ongezeko la makusanyo ya korosho ghafi kutoka kwa wakulima na Wanachama |
| MK7 | Kuongeza tija ya uzalishaji wa korosho katika mashamba ya wakulima | Uzalishaji kwa kila mkorosho unafikia angalau kilo 50 kwa mwaka hadi kufika 2030/31 | |
| | | | |

**Lengo la 2: Uzalishaji na ukusanyaji wa ufuta, mbaazi, alizeti na choroko unaongezeka**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuongeza matumizi ya mbegu bora za ufuta, mbaazi, choroko na alizeti miongoni mwa wakulima | Angalau 50% ya wakulima wanatumia mbegu bora za mazao kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa uzalishaji wa ufuta, mbaazi, alizeti na choroko kutoka kwa wakulima na Wanachama |
| MK2 | Kuwezesha upatikanaji wa huduma za ugani kwa wakulima | Angalau 50% ya wakulima wanapata huduma za uhakika za ugani kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | |
| MK3 | Kuongeza ukubwa wa mashamba yanayolimwa ufuta, mbaazi, alizeti na choroko katika eneo la Chama | Mashamba mapya yanayolimwa ufuta, mbaazi, alizeti na choroko yanaongezeka kwa angalau 10% kufikia 2030/31 | |
| MK4 | Kuongeza makusanyo ya ufuta, mbaazi, alizeti na choroko kutoka kwa Wanachama na | Kuongeza makusanyo ya ufuta kutoka tani 52,000 hadi tani 100,000 ifikapo 2030/31 | Ongezeko la makusanyo ya ufuta, mbaazi, alizeti na choroko |
| | | Kuongeza makusanyo ya mbaazi kutoka tani 3,000 hadi tani 10,000 ifikapo 2030/31 | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Wakulima | Kufikisha angalau makusanyo ya tani 10,000 za choroko ifikapo 2030/31 | |
| | | Kufikisha angalau makusanyo ya tani 10,000 za alizeti ifikapo 2030/31 | |
| MK5 | Kuongeza tija ya uzalishaji wa ufuta, mbaazi, alizeti na choroko katika mashamba ya wakulima | Uzalishaji wa ufuta kwa kila ekari moja (1) ya mkulima unaongezeka kutoka kilo 300 hadi 500 ifikapo 2030/31 | |
| | | Uzalishaji wa mbaazi kwa kila ekari moja (1) ya mkulima unaongezeka kutoka kilo 500 hadi 800 ifikapo 2030/31 | |
| | | Uzalishaji wa choroko kwa kila ekari moja (1) ya mkulima unaongezeka kutoka kilo 300 hadi 400 ifikapo 2030/31 | |
| | | Uzalishaji wa alizeti kwa kila ekari moja (1) ya mkulima unafikia angalau magunia 5 kufikia 2030/31 | |
| | | | |

**Lengo la 3: Ubora wa mazao yanayozalishwa unaimarishwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuimarisha usimamizi wa ubora wa mazao miongoni mwa Wanachama na wakulima kabla ya kufika maghala makuu | Angalau 97% ya korosho inayokusanywa inakuwa na ubora wa daraja la kwanza (grade A) kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa ubora wa mazao ya kibiashara na uwezo wa kushawishi bei nzuri sokoni |
| | | Wakulima na Wanachama wanazingatia ubora wa ufuta, mbaazi, alizeti na choroko kwa angalau 90% hadi kufikia 2030/31 | |
| MK2 | Kuratibu upatikanaji wa vifaa vya kutunzia mazao na kupima ubora kwa Wanachama | Mahitaji ya Wanachama ya vifaa vya kupimia ubora yanafikiwa kwa angalau 95% kila msimu wa mauzo hadi kufikia 2030/31 | |
| MK3 | Kuimarisha usimamizi wa ubora wa mazao ya wakulima katika maghala makuu | Hadi kufikia 2030/31 angalau 97% ya mazao ya kibiashara yaliyoko maghala makuu yanabaki na ubora stahiki hadi yanapouzwa kwa kila msimu | |
| | | | |

### 3.7.4 Kipaumbele Na. 4: Masoko na uhusiano na wadau

Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao Ltd kilianzishwa pia kwa lengo la kuratibu utafutaji wa masoko ya uhakika ya mazao yanayozalishwa na Wanachama na wakulima. Hivyo, kila msimu wa minada, Chama kimekuwa kikiratibu uuzaji wa mazao ya korosho, ufuta na mbaazi. Wakati wa kutekeleza Mpango Makati huu, Chama kitaendelea kuuza mazao hayo katika masoko yaliyoko na kutafuta masoko mbadala. Chama kitaratibu pia utafutaji wa masoko ya uhakika kwa mazao mengine hasa choroko na alizeti. Katika kufanya shughuli zake, Chama kimekuwa kikishirikiana na wadau

(taasisi) mbalimbali. Hivyo Chama kitaendeleza na kuboresha mahusiano na wadau walioko na kubaini wadau wapya wa kushirikiana nao. Pia Chama kinatambua umuhimu wa kuzitangaza shughuli zake kwa wadau mbalimbali wa ndani na nje ya Nchi.

**Lengo la 1: Masoko yenye uhakika kwa mazao ya kibiashara yanakuwepo**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuendeleza uuzaji wa mazao kwenye masoko yaliyoko | Uuzaji wa mazao ya kibiashara katika masoko yaliyoko unaendelezwa kila msimu wa mauzo hadi kufikia 2030/31 | Kufanikisha upatikanaji wa masoko ya uhakika ya mazao ya kibiashara |
| MK2 | Kuratibu ununuzi wa choroko na alizeti kupitia Chama | Mfumo wa rasmi wa uuzaji alizeti na choroko kutoka kwa wakulima unakuwepo kuanzia 2026/27 na kuendelezwa | |
| MK3 | Kutafiti masoko mapya ya mazao ya kibiashara | Masoko mapya ya uhakika kwa mazao ya kibiashara ya wakulima na Wanachama yanapatikana hadi kufikia 2030/31 | Kubaini masoko mbadala yenye fursa kwa mazao ya kibiashara |
| MK4 | Kuimarisha ushiriki wa Wanachama katika shughuli za masoko | Kila msimu wa minada, viongozi na watendaji wa AMCOS wanashiriki kikamilifu katika shughuli za masoko ya mazao hadi kufikia 2030/31 | Kuongezeka na uwazi na imani kwa Wanachama na wakulima kuhusu mchakato mzima wa masoko |
| MK5 | Kudhibiti uuzaji wa mazao ya kibiashara katika masoko yasiyo rasmi | Angalau 95% ya mazao ya wakulima yanakusanywa na AMCOS na kuuzwa kupitia Chama kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Kumlinda mkulima kwa kumpa masoko ya uhakika yenye bei nzuri na kukuza kipato chake na mapato kwa Chama na Wanachama |
| | | | |

**Lengo la 2: Uhusiano mzuri kati ya Chama na Wadau wake unaimarishwa na kuendelezwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuimarisha na kuendeleza uhusiano na wadau wa sasa wa Chama | Uhusiano wa Chama na wadau wa sasa unaimarishwa na kuendelezwa hadi kufikia 2030/31 | Uwepo wa wadau wa uhakika wa kushirikiana nao katika kutekeleza mipango na shughuli za Chama na kufikia huduma muhimu kwa urahisi |
| MK2 | Kuanzisha na kuendeleza uhusiano na wadau wapya wa Chama | Mahusiano kati ya Chama na wadau wapya yanaanzishwa na kuendelezwa hadi kufikia 2030/31 | |
| MK3 | Kuimarisha kitengo cha masoko ili kushughulikia mahusiano na wadau na huduma kwa wateja | Muundo na majukumu ya Kitengo cha Masoko vinaboreshwa kabla ya Mei 2027 | Kuongezeka kwa ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yanayohusu huduma wa wateja na mahusiano na wadau |
| | | | |

**Lengo la 3: Kufahamaika kwa Chama miongoni mwa wadau kunaongezeka**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuongeza kufahamika kwa Chama miongoni mwa wadau wa ndani ya Nchi | Kufahamika kwa Chama miongoni mwa wadau mbalimbali nchini kunaongezeka zaidi ifikapo 2030/31 | Chama kinafahamika zaidi miongoni mwa wadau hivyo kukuza jina lake (*brand*) na kupata fursa za masoko, mitaji, uwekezaji wa ubia na huduma za msingi |
| MK2 | Kuongeza kufahamika kwa Chama miongoni mwa wadau wa nje ya Nchi | Kufahamika kwa Chama miongoni mwa wadau wa nje ya nchi kunaongezeka zaidi ifikapo 2030/31 | |
| | | | |

### 3.7.5 Kipaumbele Na. 5: Usimamizi endelevu wa miradi na uwekezaji

Uwepo wa miradi ya kiuchumi na uwekezaji mwingine ni muhimu kwa ustawi wa Chama. Husaidia kukuza mapato ya Chama na uwezo wake wa kuwahudumia Wanachama na wakulima. Kwa miaka yote ya uhai wake, Chama kimeweza kufanya uwekezaji mbalimbali ikiwemo; ujenzi wa maghala, kununua ardhi, uwekezaji katika hisa na jengo la ofisi na ununuzi wa magari ya mizigo. Katika kutekeleza Mpango Mkakati huu, Bodi na watendaji wataendelea kubuni na kuwekeza katika vitega uchumi mbalimbali vyenye manufaa kwa Chama, Wanachama na wakulima. Chama kitahakikisha kinatafuta rasilimali za kutosha ili kufanikisha uwekezaji husika. Kwa sehemu kubwa, uwekezaji husika utafanyika zaidi ndani ya eneo la Chama (Halmashauri za Kilwa, Mtama na Lindi Manispaa). Wanachama pia watahamasishwa kuanzisha miradi mbalimbali ya kiuchumi.

**Lengo la 1: Uwekezaji wa hisa katika taasisi za kibiashara unaongezeka na kufuatiliwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuendeleza uwekezaji kwenye Benki ya Ushirika Tanzania (Coop Bank) | Uwekezaji wa hisa wa ziada Coop Bank unaendelezwa kila inapohitajika hadi kufikia 2030/31 | Kukua kwa mtaji na mapato katika Chama na kuimarisha uwezo wake katika kutoa huduma kwa Wanachama na wakulima |
| MK2 | Kuwekeza hisa kwenye taasisi mbalimbali za kibiashara zenye mwenendo mzuri | Uwekezaji (ununuzi) wa hisa kwenye angalau taasisi 2 za kibiashara unafanyika hadi kufikia 2030/31 | |
| | | Kuwekeza hisa za Wanachama katika taasisi angalau 2 za kibiashara ifikapo 2030/31 | Ongezeko la thamani ya hisa za uanachama |
| MK3 | Kufuatilia mwenendo wa kibiashara wa taasisi zilizowekezwa hisa | Ufuatiliaji wa mwenendo wa kibiashara wa taasisi husika unafanyika na kutoa mrejesho kwa Wanachama kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Uwepo wa taarifa za kutosha za kuwezesha maamuzi sahihi ya uwekezaji ndani ya Chama |
| | | | |

## Lengo la 2: Miradi endelevu ya kiuchumi ya Wanachama inaanzishwa na kusimamiwa

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuwezesha uanzishaji wa miradi ya kiuchumi ya Wanachama | Angalau 50% ya Wanachama wanawekeza katika miradi ya kiuchumi hadi kufikia 2030/31 | Kupungua kwa utegemezi wa ushuru kama chanzo kikuu cha mapato ya Wanachama, kuwa na miradi yenye tija na endelevu na kukuza uwezo wa AMCOS kuwahudumia wakulima |
| MK2 | Kuimarisha usimamizi wa miradi ya kiuchumi ya Wanachama | Viongozi na watendaji wa AMCOS wanapewa mafunzo ya usimamizi wa miradi ya kiuchumi angalau mara 1 kwa mwaka hadi kufikia 2030/31 | |
| | | Angalau 80% ya miradi ya kiuchumi ya Wanachama inakuwa endelevu na kusimamiwa ipasavyo hadi kufikia 2030/31 | |
| | | | |

## Lengo la 3: Miradi mipya ya kimkakati katika Chama inaanzishwa na kuendelezwa

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuanzisha mradi wa mashamba ya kuzalisha korosho (na mazao mengine ya kibiashara) | Ukubwa wa mashamba ya korosho unaongezwa kutoka ekari 82 hadi 300 kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa mapato ya ziada na uzalishaji wa korosho (na mazao mengine ya kibiashara) hivyo kukuza uchumi wa Chama na uwezo wa kuwahudumia wanachama na wakulima pamoja na kuwekeza zaidi |
| MK2 | Kuanzisha kiwanda cha kuzalisha mafuta ya kula | Kiwanda kimoja (1) cha kuzalisha mafuta ya kula kinaanzishwa kabla ya 2030/31 | Kuongezeka kwa mapato ya ziada hivyo kukuza uchumi wa Chama, uwezo wa kuwahudumia wanachama na wakulima pamoja na kuwekeza zaidi |
| MK3 | Kuwa na maghala makuu ya ziada ya kuhifadhia mazao | Angalau maghala makuu mapya mawili (2) yanajengwa katika eneo la Chama kabla ya 2030/31 | |
| MK4 | Kuwa na ukumbi wa kisasa wa mikutano na matumizi kibiashara | Angalau ukumbi mmoja (1) wa kisasa wa mikutano na matumizi ya kibiashara unajengwa kabla ya 2030/31 | |
| MK5 | Kuanzisha mradi wa usafirishaji wa mazao na bidhaa nyingine | Mradi wa usafirishaji wenye magari angalau kumi na tano (15) unaanzishwa na kuendelezwa kabla ya 2030/31 | |
| MK6 | Kuanzisha mradi wa hoteli ya kisasa | Hoteli ya kisasa angalau moja (1) inajengwa eneo la Lindi Manispaa na kuendelezwa kabla ya 2030/31 | |
| MK7 | Kuanzisha mradi wa maduka ya pembejeo za kilimo | Angalau duka moja (1) la pembejeo linaanzishwa kila Halmashauri ya eneo la Chama hadi kufikia 2030/31 | |
| MK8 | Kuanzisha taasisi za kusimamia miradi ya kiuchumi ya Chama | Angalau kampuni mbili (2) zinaanzishwa ili kusimamia miradi ya kiuchumi ya Chama kabla ya 2030/31 | Kuongezeka kwa ufanisi katika uendeshaji na usimamizi wa miradi ya Chama |

### 3.7.6 Kipaumbele Na. 6: Usimamizi wa fedha na mali

Kwa wakati wote, Chama kina wajibu wa kuhakikisha kuwa fedha na mali zake zinasimamiwa vizuri. Hadi sasa, Chama kimeweza kumiliki mali mbalimbali tangu kuanzishwa kwake. Mali hizi ni pamoja na; fedha, hisa katika taasisi mbalimbali, majengo, vyombo vya usafiri (magari na pikipiki), vifaa vya ofisini, maghala na ardhi/mashamba na mali nyingine. Kupitia Mpango Mkakati huu, Chama kitaendelea kuboresha usimamizi wa mali na fedha zake ili ziendelee kuwanufaisha Wanachama na wakulima.

**Lengo la 1: Uwezo wa Chama katika usimamizi wa kifedha unaimarishwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuimairisha uwezo wa Bodi na watendaji katika usimamizi wa fedha za Chama | Viongozi na watendaji wa Chama wanapata mafunzo ya usimamizi wa fedha angalau mara 1 kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa ufanisi katika usimamizi wa mapato na matumizi katika Chama, kukua kwa mtaji na uwezo wa kutoa huduma na uwekezaji |
| MK2 | Kukuza kiwango cha mapato na udhibiti wa matumizi ya Chama | Mapato ya Chama yanakusanywa kwa angalau 100% kulinganisha makisio ya mwaka husika hadi kufikia 2030/31 | |
| | | Matumizi ya fedha za Chama yanafanyika kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa kwa 100% kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | |
| | | Matumizi ya mwaka ya Chama hayazidi 85% ya mapato yake hadi kufikia 2030/31 | |
| | | Kuhuisha viwango vya ada ya uanachama angalau mara 1 hadi ifikapo 2030/31 | |
| MK3 | Kuimarisha mtaji wa ndani wa Chama | Mtaji wa Chama unaongezeka kwa angalau 20% ya mwaka uliopita hadi kufikia 2030/31 | |
| | | Kuanzisha mifuko ya ndani angalau mitatu (3) ya matengo ya hiari (revenue reserves) hadi kufikia 2030/31 | |
| MK4 | Kukuza kiwango cha hisa za uanachama | Angalau 95% ya Wanachama wanakamilisha hisa zao za uanachama kabla ya 2028/29 | Kuongezeka kwa hisa za uanachama |
| | | Kuhuisha viwango vya hisa za uanachama angalau mara 1 hadi ifikapo 2030/31 | |
| MK5 | Kuzingatia uwekaji wa matengo yote ya kisheria | Matengo yote ya kisheria kutokana na ziada ya kibiashara yanawekwa kwa 100% kila mwaka hadi ifikapo 2030/31 | Kukua kwa mtaji wa Chama |
| MK6 | Kuimarisha udhibiti wa madeni ya kibiashara ya Chama | Madeni ya kibiashara hayazidi 30% ya thamani ya mali za Chama kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa ufanisi katika udhibiti wa madeni ya Chama na kuwezesha mali za Chama kujengwa zaidi na mtaji kuliko madeni |
| | | Ufanisi katika ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wadaiwa unafikia angalau 70% kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Kuongeza kiwango cha mali za Chama na kuimarisha ukwasi hivyo kuweza kutoa huduma na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | kugharamia uwekezaji na shughuli za kila siku kwa ufanisi |
| MK7 | Kuimarisha mfumo wa uthibiti wa ndani katika Chama | Mfumo imara wa udhibiti wa ndani unakuwepo wakati wote hadi kufikia 2030/31 | Uwezo wa Chama kusimamia vyema fedha zake na shughuli nyingine kwa tija |
| | | | |

**Lengo la 2: Umiliki na usimamizi wa mali za Chama unaimarishwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kukamilisha umiliki wa kisheria wa ardhi za Chama | Urasmishaji wa ardhi zote zinazomilikiwa na Chama unafanyika kwa wakati hadi kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa ufanisi katika usimamizi wa mali ikiwemo matumizi rafiki ya mali zilizoko |
| MK2 | Kuendeleza ardhi za Chama zilizonunuliwa | Ardhi zote zinazomilikiwa Chama zinaendelezwa kwa matumizi yaliyokusudiwa hadi kufikia 2030/31 | |
| MK3 | Kufanya uhakiki na utathminishaji wa mali za Chama | Uthaminishaji wa mali za Chama unafanyika kwa wakati (mara 3 hadi 5) hadi kufikia 2030/31 | |
| | | Uhakiki mali za Chama (stock taking) unafanyika kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | |
| MK4 | Kuimairisha uwezo wa Bodi na watendaji katika usimamizi wa mali za Chama | Viongozi na watendaji wa Chama wanapata mafunzo ya usimamizi wa mali angalau mara 1 kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | |
| | | Mali za Chama zinatumika vyema na kuwa katika hali nzuri wakati wote hadi kufikia 2030/31 | |
| | | | |

### 3.7.7 Kipaumbele Na. 7: Uongozi, utawala bora na menejimenti ya rasilimali watu

Mipango na shughuli za Chama hufanikiwa endapo kuna uongozi bora na watendaji wa kutosha wenye weledi na uzoefu mkubwa. Uwepo wa viongozi na watendaji wanaofuata misingi ya utawala bora huwezesha kujenga mahusiano mazuri ya wadau wa ndani na nje ya Chama, kufanikisha utekelezaji, kudhibiti migogoro na kusimamia vyema rasilimali. Pia Chama huhitaji watendaji enye sifa katika kila Kitengo/Idara. Hivyo katika Mpango Mkakati huu, Bodi itaendelea kupanga na kusimamia Chama kwa mujibu wa Sheria, Sera, Kanuni husika na misingi ya utawala bora na kuhakikisha kuna watendaji wa kutosha wenye sifa.

**Lengo la 1: Kuwa na Wanachama, Bodi na Watendaji wenye uelewa mzuri kuhusu Sera, Sheria na misingi ya uongozi na utawala bora**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kujenga uwezo wa Bodi, Menejimenti na Wanachama juu ya sera, sheria na misingi ya uongozi na utawala bora | Viongozi na watendaji wa Chama wanapata mafunzo kuhusu sera, sheria na misingi ya uongozi na utawala bora angalau mara 1 kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Kuimarika kwa ufanisi katika usimaizi wa shughuli za Chama, ushirikiano mzuri miongoni mwa wadau wa ndani na mahusinao mazuri na Mamlaka mbalimbali |
| MK2 | Kuanzisha mfumo wa kurithishana weledi wa uongozi katika Chama na Wanachama (succession planning) | Mfumo wa kurithishana weledi wa uongozi katika Chama na Wanachama unakuwepo kabla ya 2030/31 | Uwepo wa hazina kubwa ya viongozi watarajiwa |
| MK3 | Kuanzisha mfumo wa kubadilishana uzoefu kati ya Chama, Wanachama na wadau wa nje | Angalau ziara za mafunzo moja (1) ya kubadilishana uzoefu wa uendeshaji na usimamizi wa Chama na AMCOS inafanyika kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Kuimarika kwa ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa Chama na AMCOS |
| MK4 | Kuhakikisha uzingatiaji wa sera, sheria na misingi ya uongozi na utawala bora katika shughuli za Chama na Wanachama | Uendeshaji na usimamizi wa Chama na Wanachama unazingatia Sera, sheria na misingi ya uongozi na utawala bora wakati wote hadi kufikia 2030/31 | Kuaminika kwa Chama miongoni mwa wadau wake ikiwemo Mamlaka zinazosimamia Vyama vya Ushirika |
| | | | |

**Lengo la 2: Ufanisi wa Bodi na Menejimenti katika kutekeleza majukumu yao unaimarishwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kujenga uwezo wa Bodi na Watendaji kuhusu majukumu yao | Bodi na Menejimenti wanapewa mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa shughuli za Chama angalau mara 2 kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Kuimarika kwa uwezo wa wajumbe wa Bodi na Watendaji katika usimamizi na uendeshaji wa shughuli za Chama |
| MK2 | Kuweka mfumo wa kupima ufanisi wa Bodi na Watendaji | Mpango/mwongozo wa kupima ufanisi wa Bodi na watendaji wa Chama unakuwepo kuanzia 2026/27 | Kuongezeka kwa ufanisi na uwajibikaji miongoni mwa wajumbe wa Bodi na Watendaji |
| | | Tathmini ya ufanisi wa utendaji kazi wa Bodi na watendaji unafanyika mara 2 kwa mwaka hadi kufikia 2030/31 | |
| MK3 | Kuboresha mazingira ya kazi kwa Watendaji na wajumbe wa Bodi wa Chama | Mazingira bora ya kazi kwa watendaji na wajumbe wa Bodi wa Chama yanakuwepo wakati wote hadi kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa ufanisi katika utendaji kazi wa Bodi na Watendaji |
| MK4 | Kuimarisha hali za kiafya kwa watendaji na viongozi wa Chama | Utaratibu wa kuchangia bima na huduma nyingine za kiafya kwa watendaji wa Chama unaendelezwa hadi kufikia 2030/31 | Uwepo wa viongozi na watendaji wenye afya njema na wanaowajibika na shughuli za Chama |
| | | Utaratibu wa kuchangia bima na huduma | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | nyingine za kiafya kwa watendaji wa Chama unakuwepo kuanzia 2026/27 na kuendelezwa | |
| | | | |

**Lengo la 3: Sera na miongozo muhimu ya usimamizi na uendeshaji wa Chama na Wanachama inakuwepo**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuboresha Masharti na sera zilizoko kuendana na mahitaji ya Chama na Wanachama | Maboresho ya Masharti na sera zilizoko yanafanyika kuanzia 2026/27 | Uwepo wa Masharti na sera za kutosha zinazotoa mwongozo sahihi na kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa Chama na AMCOS |
| MK2 | Kuandaa sera na miongozo mingine mipya inayohitajika kwa Chama na Wanachama | Sera mpya zinazohitajika zinaandaliwa kwa wakati kabla ya 2030/31<br>(mf: uwekezaji, utatuzi wa migogoro, elimu na mafunzo, huduma kwa wateja, huduma wa jamii, masoko, TEHAMA, mawasiliano, mazingira, jinsia na vijana, muundo wa utumishi n.k) | |
| MK3 | Kuwezesha uandaaji wa Masharti na sera muhimu katika AMCOS | Angalau 90% ya wanachama wanakuwa na Masharti na sera muhimu kufikia kabla ya 2027/28 | |

**Lengo la 4: Uendelezaji wa Watendaji katika Chama unaimarishwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuongeza watendaji wapya wenye sifa na kuwajengea uwezo | Angalau 90% ya watendaji wapya wanaohitajika katika kada mbalimbali ndani ya Chama wanakuwepo hadi kufikia 2030/31 | Uwepo wa watendaji wa kutosha na wenye weledi na uzoefu mkubwa katika Chama |
| | | 100% ya watendaji wapya wanapata ufahamu wa majukumu yao na shughuli za Chama hadi kufikia 2030/31 | |
| MK2 | Kuwawezesha watendaji wa Chama kupata fursa za kujiendeleza kielimu | Mpango wa kuwezesha watendaji kujiendeleza kielimu unakuwepo na kutekelezwa kuanzia 2026/27 | |
| | | Utaratibu wa kuwagharamia Watendaji kwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu unakuwepo kuanzia 2026/27 na kuendelezwa | |
| MK3 | Kuhuisha muundo wa utumishi | Muundo wa utumishi wa Chama unahusishwa kila inapohitakjika hadi kufikia 2030/31 | Uwepo wa uwajibikaji na kutokuingiliana kwa majukumu miongoni mwa watendaji na uwazi katika utambuzi wa haki na stahiki zao |
| | | | |

**Lengo la 5: Uhusiano miongoni mwa Wadau wa Ndani wa Chama unaboreshwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuendeleza uhusiano mzuri kati ya Bodi na Watendaji | Uhusiano mzuri kati ya Bodi na watendaji unakuwepo wakati wote hadi kufikia 2030/31 | Uwepo wa ushirikiano mzuri miongoni mwa wadau wa ndani wa Chama na uwajibikaji hivyo kufanikisha malengo na shughuli za Chama |
| MK2 | Kuendeleza uhusiano kati ya Chama na Wanachama wake | Uhusiano mzuri kati ya Chama na Wanachama unakuwepo wakati wote hadi ifikapo 2030/31 | |
| | | | |

**Lengo la 6: Ushiriki wa wanawake na vijana katika shughuli za Chama na Wanachama unaboreshwa na kuendelezwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuimarisha ushiriki wa wanawake katika Chama na Wanachama | Ushiriki wa wanawake kwenye uongozi, uanachama na shughuli nyingine katika Chama na AMCOS unafikia angalau 40% ifikapo 2030/31 | Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao, ubunifu, uwajibikaji na hazina ya viongozi wa baadae katika Chama na AMCOS |
| MK2 | Kuimarisha ushiriki wa vijana katika Chama na Wanachama | Ushiriki wa vijana kwenye uongozi, uanachama na shughuli nyingine za Chama na Wanachama unafikia angalau 40% ifikapo 2030/31 | |
| | | | |

### 3.7.8 Kipaumbele Na. 8: Matumizi endelevu ya TEHAMA

Uendeshaji na usimamizi wa shughuli na biashara za Chama na Wanachama ni sharti viendane na mabadiliko ya kiteknolojia. Hii ni pamoja kuongeza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasialiano (TEHAMA). Katika Mpango Mkakati huu, Chama kitaendelea kutumia na kuboresha mifumo mbalimbali ya TEHAMA iliyoko ikiwemo; Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU), mfumo wa ugawaji wa pembejeo wa Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), mfumo wa uhasibu na fedha na mingine. Chama kitaendelea pia kuwalipa wakulima kupitia mifumo ya kibenki na mitandao ya simu). Chama kinatarajia kuanzisha tovuti yake na kuongeza matumizi vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwa lengo la kufikisha taarifa na elimu kwa wanachama, wakulima na jamii kwa ujumla.

**Lengo la 1: Usimamizi na matumizi ya TEHAMA katika Chama na AMCOS yanaboreshwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kuboresha utumiaji wa mifumo ya TEHAMA katika shughuli za Chama | Matumizi ya mifumo ya TEHAMA iliyoko katika Chama yanaendelezwa hadi kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa Chama ikiwemo kufikisha taarifa sahihi kwa wakati na kupunguza gharama za uendeshaji |
| | | Angalau mfumo mpya mmoja (1) wa TEHAMA unakuwepo katika Chama kufikia 2030/31 | |
| | | Matumizi ya karatasi katika shughuli za Chama yanapungua kwa angalau 50% kufikia 2030/31 | |
| MK2 | Kuanzisha tovuti ya Chama | Tovuti ya Chama yenye ubora stahiki inakuwepo kuanzia 2026/27 | |
| MK3 | Kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwa Wanachama | Angalau 70% ya watendaji wa AMCOS wanakuwa na uelewa mzuri wa matumizi ya TEHAMA katika shughuli zao hadi kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa AMCOS ikiwemo kufikisha taarifa sahihi kwa wakati na kupunguza gharama za uendeshaji |
| | | Matumizi ya karatasi katika AMCOS yanapungua kwa angalau 50% kufikia 2030/31 | |
| MK4 | Kuimarisha uwezo wa Chama na Wanachama katika usimamizi wa mifumo ya TEHAMA | Kutoa mafunzo angalau mara 1 kila mwaka kwa viongozi na watendaji wa Chama na Wanachama kuhusu matumizi na usimamizi wa mifumo ya TEHAMA hadi kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa shughuli za Chama na Wanachama, kupunguza gharama na uwepo wa watendaji wenye weledi katika usimamizi na matumizi rafiki ya TEHAMA |
| | | Uwezo wa usimamizi wa mifumo ya TEHAMA katika Chama na Wanachama unaimarishwa hadi kufikia 2030/31 | |
| MK5 | Kuongeza matumizi ya mitandao ya kijamii na vyombo vya habari kwa maslahi ya Chama na Wanachama | Matumizi rafiki ya vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwa Chama na Wanachama yanakuwepo wakati wote hadi kufikia 2030/31 | Kuongeza uwezo wa Chama na Wanachama kufikisha taarifa na elimu kwa walengwa mbalimbali na kutangaza shughuli zao |
| MK6 | Kushirikiana na mabenki na makampuni ya simu kuwezesha malipo ya wakulima | Kila msimu wa minada, wakulima wanaendelea kupata malipo ya mazao yao kupitia mabenki na mitandao ya simu hadi ifikapo 2030/31 | Kuongezeka kwa ufanisi katika malipo ya wakulima na kujenga imani yao kwa Chama |
| | | | |

### 3.7.9 Kipaumbele Na. 9: Utunzaji wa mazingira na kujali jamii

Katika kuendesha shughuli za kila siku za Chama, Wanachama na wakulima, ni vyema pia kufikiria kuhusu utunzaji wa mazingira. Wakati wa utekelezaji wa Mpango Mkakati huu, Chama kinatambua kuwa ongezeko la shughuli za kilimo za Wanachama na wakulima na uwekezaji wake katika ujenzi wa kiwanda na majengo ya kibiashara pamoja na uanzishaji mashamba makubwa huweza kuathiri

mazingira kwa namna mbalimbali. Hivyo, Chama kitahakikisha katika shughuli zote hizi mazingira yanatunzwa. Chama pia kitaendelea kuwajibika kusaidia shughuli za maendeleo ya jamii katika eneo lake.

**Lengo la 1: Juhudi za utunzaji wa mazingira ngazi ya Chama na Wanachama zinaimarishwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kujenga uwezo wa Wanachama na wakulima kuhusu utunzaji wa mazingira na udhibiti wa taka | Wakulima wanapata elimu kuhusu kilimo bora na utunzaji wa mazingira angalau mara moja (1) kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Kuongezeka kwa uelewa kuhusu mahusinao ya kilimo na utunzaji wa mazingira na wajibu wa Chama, Wanachama na wakulima |
| | | Viongozi na watendaji wa Chama na Wanachama wanapata elimu kuhusu kilimo bora na utunzaji wa mazingira angalau mara moja (1) kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | |
| MK2 | Kushirikiana na wadau katika juhudi za utunzaji wa mazingira | Kushiriki angalau matukio mawili (2) ya masuala ya mazingira kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Ushirikiano na wadau katika utunzaji wa mazingira na kutambulika kwa juhudi za Chama katika suala husika |
| MK3 | Kuratibu uoteshaji wa miti rafiki kwa mazingira kwenye mashamba ya Chama, Wanachama, Wakulima na maeneo mengine ya wazi | Angalau miche ya miti na matunda 300,000 (ikiwemo mikorosho) inaoteshwa kila mwaka katika eneo la Chama hadi kufikia 2030/31 | |
| MK3 | Kuweka vifaa na miundombinu ya kuhifadhi taka mbalimbali kutoka katika ofisi na miradi ya Chama | Vifaa na miundombinu muhimu vya kuhifadhi taka inakuwepo katika ofisi na miradi ya Chama hadi kufikia 2030/31 | Ufanisi katika udhibiti wa taka na utunzaji wa mazingira |
| MK4 | Kuwezesha uanzishaji wa miradi ya kiuchumi inayolenga utunzaji wa mazingira | Angalau mradi mmoja (1) wa utunzaji wa mazingira unafadhiliwa kila mwaka katika eneo la Chama hadi kufikia 2030/31 | Kukuza kipato cha wanufaika kupitia shughuli za utunzaji mazingira na pia kukuza hadhi ya Chama |
| | | | |

**Lengo la 2: Ushiriki wa Chama katika huduma za kijamii unaendelezwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Matokeo |
|---|---|---|---|
| MK1 | Kushiriki katika shughuli za maendeleo ya jamii katika eneo la Chama | Kushiriki angalau matukio mawili (2) ya kusaidia watu wenye uhitaji au shughuli za maendeleo ya jamii kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Upatikanaji wa huduma za msingi katika jamii na mahitaji ya watu wa makundi maalum hivyo kukuza hadhi/saifa ya Chama kwa jamii |
| | | | |

## 3.8 Nguzo za Uandaaji wa Mpango Mkakati

Katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Chama msimu wa 2024/25, Wanachama waliiagiza Bodi na watendaji kuhakikisha kuwa Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Chama unaandaliwa. Hivyo uandaaji wa Mpango Mkakati huu ni sehemu ya utekelezaji wa azimio la Mkutano Mkuu huo.

Pia uandaaji wa Mpango Mkakati huu umeakisi miongozo mbalimbali ya kitaifa inayohusu Ushirika na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Baadhi ya miongozo iliyofanyiwa rejea katika kuandaa vipaumbele vya Mpango Mkakati huu ni pamoja na; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano; Sera ya Maendeleo ya Ushirika 2002; Sera ya Kilimo 2013; Ilani ya Chama Tawala (2025-2030); na Vipaumbele vya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC).

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inaelezea malengo ya kitaifa ya muda mrefu ambayo nchi yetu inatazamia kuyafikia. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inaongozwa na misingi ya *Demokrasia, Haki na Uhuru*; *Utu; Amani na Umoja*; *Utajiri na Rasilimali Asilia; na Utamaduni na Maadili ya Taifa*. Pia Dira hii ina nguzo kuu tatu - *Uchumi Imara, Jumuishi, na Shindani*; *Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii*; na *Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi*. Nguzo hizi zinatoa mwelekeo na nyenzo muhimu kwa utekelezaji wa vipaumbele vya maendeleo ya Tanzania kuelekea mwaka 2050 na kufikia Uchumi wa juu (*advanced economy*) wenye thamni ya Dola za Kimarekani trilioni moja (1). Ili kuchochea maendeleo endelevu ya wananchi na kupunguza umaskini, Serikali imeendelea kuwa mstari wa mbele kusaidia maendeleo ya Vyama vya Ushirika kushiriki kikamilifu kwenye mnyororo wa thamani wa mazao ya kimkakati na kufanikisha dira ya maendeleo ya taifa.

Serikali imeendelea kuandaa na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano ikiwemo ule wa unaoisha sasa wa 2021/22 hadi 2025/26. Mipango hii inalenga kujenga uchumi shindani na Viwanda kwa maendeleo ya Watu. Vyama vya Ushirika, ikiwemo LMCU Ltd na Wanachama wake ni sehemu ya kufanikiwa malengo haya ya Serikali. Sera ya Ushirika 2002 inatoa mwongozo wa uhamasishaji na uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika vya kilimo na masoko (AMCOS) kwenye maeneo mbalimbali yanayojihusisha na kilimo. Serikali inaendelea kutoa hamasa kuhusu uanzishwaji wa AMCOS vijijini. LMCU Ltd ina mchango mkubwa katika kuwezesha utekelezaji wa Sera hii na inaendelea kuwaunganisha Wanachama na wakulima na kuwapa huduma muhimi ili wanufaike kwa kilimo cha kibiashara.

Sera ya Maendeleo ya Kilimo ya 2013 inalenga kuendeleza tasnia ya kilimo yenye ufanisi, ushindani na faida ili kuboresha maisha ya Watanzania na kufikia ukuaji wa uchumi mpana na kupunguza

umaskini. Sera inahimiza uwepo wa Vyama vya Wakulima vyenye nguvu na endelevu katika maeneo ya vijijini ili kuimarisha nguvu zao na ushindani. Pia sera inahimiza kuboresha uongozi, stadi za ujasiriamali na ujuzi. Hivyo LMCU Ltd, Wanachama na wakulima ni wadau muhimu katika kutekeleza sera hii kwani ushiriki wao katika mnyororo wa thamani wa mazao mbalimbali ni muhimu kwa ukuaji na uendelevu wa sekta ya kilimo nchini.

Ilani ya Chama tawala ya 2025 hadi 2030 inaamini kuwa ushirika ni njia ya uhakika ya kuwezesha Wanachama na wakulima kuwa na uwezo mkubwa wa kutatua changamoto zao za kiuchumi na kijamii. Vyama vya Ushirika huwezesha wananchi kutumia juhudi za pamoja katika kufikia malengo ambayo yasingeweza kufikiwa kwa juhudi za mtu mmoja mmoja. Ilani inahimiza kufufua, kuimarisha na kuhamasisha Vyama vya Ushirika kushiriki katika shughuli za kiuchumi ikiwemo kumiliki viwanda kuongeza mnyororo wa thamani wa bidhaa.

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) ndiye msimamizi wa Vyama vya Ushirika nchini. Ili kuimarisha nguvu ya Vyama vya Ushirika, TCDC imeweka vipaumbele saba (7) ambavyo inalenga kuvitekeleza. Vipaumbele hivi ni; Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kidigitali; Uanzishaji wa Benki ya Ushirika Tanzania; Kuhamasisha Vyama vya Ushirika kujiendesha kibiashara; Kuboresha sera, sheria na usimamizi wa Vyama vya Ushirika; Kuhamasisha uanzishaji wa Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali na makundi maalum; Kuimarisha uwekezaji na mali za Ushirika katika uzalishaji; na Kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuendeleza sekta ya Ushirika. Hivyo, uandaaji wa Mpango Mkakati huu umezingatia pia vipaumbele hivi vya TCDC.

### 3.9 Madhanio ya Msingi Kuhusu Utekelezaji wa Mpango Mkakati

Wakati wa kutekeleza Mpango Mkakati huu, Chama kinatarajia kuwa kitafanya kazi katika mazingira rafiki hivyo kuweza kutekeleza mipango na shughuli zake kwa mafanikio makubwa. Wanachama, Bodi na Menejimenti ya LMCU Ltd wanaamini mambo yafuatayo yatakuwepo wakati wote katika miaka mitano ijayo;

(i) Wadau wote wa nje (taasisi za Serikali na sekta binafsi) watashirikiana vyema na Chama ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli zote kwa ufanisi hivyo kufanikisha malengo na shughuli zilizopangwa;

(ii) Wakati wa utekelezaji, kutakuwa na mazingira rafiki ya kibiashara na uendeshaji wa Chama na pamoja na utulivu wa kisiasa na amani nchini;

(iii) Kutakuwa na ushirikiano na uhusiano mzuri miongoni mwa Wajumbe wa Bodi, Watendaji na Wanachama;

(iv) Wajumbe wa Bodi na watendaji wa Chama watawajibika ipasavyo na kuzingatia misingi ya ushirika na utawala bora;

(v) Wakati wote, shughuli za kibiashara za Chama na miradi mbalimbali havitakumbwa na vihatarishi vikubwa vinavyoweza kuathiri ufanisi katika utekelezaji wa malengo ya kimkakati;

(vi) Rasilimali za kutosha zitakuwepo wakati wote wa utekelezaji;

(vii) Uzalishaji na ubora wa mazao mbalimbali eneo la Chama utaongezeka;

(viii) Serikali kupitia Wizara na taasisi husika itaendelea kuimarisha maendeleo ya ushirika na kilimo kwa kutunga Sera, Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali na kuepusha mwingiliano mkubwa wa kisiasa au mambo mengine hatarishi kwa Vyama vya Ushirika;

(ix) Usimamizi mzuri wa rasilimali za Chama utakuwepo hivyo kufanikisha malengo yaliyopangwa; na

(x) Mwenendo wa hali ya kiuchumi nchini na duniani kwa ujumla utakuwa mzuri hivyo kukiwezesha Chama, Wanachama na wakulima kuendelea kufanya shughuli zao kwa ufanisi na tija

# SURA YA NNE

# MPANGO WA UTEKELEZAJI

Kwa kuzingatia vipaumbele na malengo ya kimkakati yaliyobainishwa, sura hii inaelezea jinsi Mpango Mkakati huu utakavyotekelezwa. Mpango huo wa utekelezaji umeonesha; malengo, mikakati, shabaha, viashiria vya utekelezaji, njia za kuthibitisha, muda na wahusika. LMCU Ltd itakuwa ikitumia mpango huo wa utekelezaji ili kuandaa bajeti na mpango kazi kila mwaka kuanzia 2026/27 hadi 2030/31.

## 4.1 Mfumo wa Utekelezaji

Utekelezaji wa Mpango Mkakati huu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo utafanyika kwa utaratibu ufuatao;

(i) Bodi ya LMCU Ltd itahakikisha kuwa wadau wote kutoka ndani na nje ya Chama wanapewa taarifa za kutosha kuhusu malengo na matarajio ya Mpango Mkakati huu na itahakikisha kuwa wanahusishwa ipasavyo katika utekelezaji wake;

(ii) Bodi na Menejimeti ya Chama watahakikisha kuwa shughuli za msingi na mipango kazi ya mwaka inafahamika mapema na kuandaliwa bajeti ikiwa ni sehemu ya kutekeleza Mpango Mkakati huu;

(iii) Kutakuwa na utaratibu wa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mpango Mkakati huu kila baada ya miezi mitatu (robo mwaka);

(iv) Bodi ya Chama itakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa wadau wote waliopangiwa shughuli mabalimbali za kutekeleza katika Mpango Mkakati huu wanazifanya kwa wakati na kwa ufanisi ili kufanikisha malengo yaliyopangwa;

(v) Vipimo vya ufanisi vilivyooneshwa katika mpango wa utekelezaji ndio vitatumika kama vigezo vya kupima hali ya utekelezaji wa malengo, mikakati na shabaha zilizopangwa; na

(vi) Utekelezaji wa Mpango Mkakati huu utasimamiwa na Bodi iliyoko madarakani na utatekelezwa na watendaji walioko kwa wakati husika. Mabadiliko ya Bodi au watendaji hayatazuia kuendelea kwa utekelezaji wa Mpango Mkakati huu.

## 4.2 Mpango wa Utekelezaji

Mpango wa utekelezaji wa Mpango Mkakati huu kwa miaka mitano umeoneshwa kupitia Kiambatanisho Na. 1.

## 4.3 Mpango Kazi wa Mwaka wa Utekelezaji wa Shughuli za Kimkakati

Katika miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango Mkakati huu, Chama kitahakikisha kuwa mikakati, shabaha na shughuli mahsusi zilizopangwa vinatekelezwa ipasavyo. Kila mwaka, Chama kitakuwa kikiandaa mpango kazi (*Strategic Action Plan*) ili kuwaongoza wajumbe wa Bodi na Watendaji katika kutekeleza Mpango Mkakati huu. Muundo wa mpango kazi wa mwaka umeoneshwa kupitia Kiambatanisho Na. 2.

## 4.4 Wajibu wa Wadau wa Chama Katika Utekelezaji

Utekelezaji wa Mpango Mkakati huu, utawahusisha wadau wote wa ndani na nje ya Chama. Wadau wa ndani ni; Wanachama, Bodi, na Watendaji. Chama pia kitafanya kazi kwa ukaribu sana na wakulima na wadau wengine kama ilivyooneshwa katika Jedwali la Uchambuzi wa Wadau.

Mkutano Mkuu utaendelea kuwa ndiyo chombo cha juu kabisa kwenye Chama na utahusika na kufanya maamuzi mbalimbali na kutekeleza majukumu mengine yote kama ilivyobainishwa katika Masharti ya Chama, Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika pamoja na sera na miongozo mingine katika Chama. Pia Chama kitaendelea kuhakikisha kuwa Mikutano Mikuu ya kisheria inafanyika kila inapohitajika. Mikutano hiyo ni pamoja na Mkutano Mkuu wa Mwaka na Mkutano Mkuu wa Kawaida. Endapo itahitajika, Mkutano Mkuu Maalum unaweza kufanyika. Kupitia Mkutano Mkuu, Wanachama watahusika kujadili mapendekezo ya bajeti, kufuatilia utekelezaji na kutoa maazimio ya kutekeleza ikiwemo uzalishaji na ubora wa mazao ya kibiashara, ukomo wa madeni, uwekezaji, huduma na mambo mengine ya kimkakati.

Bodi ya Chama itaendelea kuchaguliwa na Mkutano Mkuu na itahusika kusimamia utekelezaji wa shughuli za kila siku za Chama, kuandaa sera na miongozo ya uendeshaji pamoja na kutekeleza maazimio ya Mkutano Mkuu na majukumu mengine kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika na Masharti ya Chama. Bodi itahusika pia kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati huu ikiwemo kufuatilia na kutathmini mwenendo wa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Bodi itahakikisha kuna rasilimali za kutosha kwa ajili ya utekelezaji. Bodi inaweza kuunda pia Kamati

ndogo ndogo na kuajiri watendaji wenye sifa kuwezesha utekelezaji wa Mpango Mkakati huu. Bodi itaendelea kuwajibika kwa Mkutano Mkuu.

Chama kitaendelea kuwatumia watendaji walioko kutekeleza Mpango Mkakati huu na majukumu mengine kwa mujibu wa sera na miongozo iliyoko. Kila mtendaji aliyeajiriwa atatakiwa kutimiza majukumu yake kwa ufanisi ikiwemo kutumia weledi wa kutosha, ubunifu na kushirikiana ipasavyo na wenzake. Meneja Mkuu wa Chama ataendelea kuwa ndiye mtendaji mkuu wa shughuli za kila siku za Chama na kuwasimamia watendaji wote walioko chini yake katika kutimiza majukumu yao. Meneja Mkuu atawajibika moja kwa moja kwa Bodi sya Chama na ataendelea kutekeleza majukumu mengine ya Chama kama ilivyooneshwa katika sera na miongozo mbalimbali ya Chama.

### 4.5 Kugharamia Utekelezaji wa Mpango Mkakati

Ili kutekeleza Mpango Mkakati huu, uwepo wa rasilimali fedha za kutosha ni muhimu sana. Chama kitatafuta fedha za utekelezaji kutoka katika vyanzo mbalimbali vya ndani na vya nje. Hivyo Mpango Mkakati huu utagharimiwa kupitia vyanzo vifuatavyo;

(i) Ushuru wa mazao
(ii) Ziada itokanayo na miradi ya Chama
(iii) Viingilio vya uanachama
(iv) Fedha kutoka kwa wahisani wa Chama
(v) Mikopo kutoka taasisi za kifedha ikiwemo mabenki na vyanzo vingine

### 4.6 Maboresho ya Mpango Mkakati

Mpango Mkakati huu wa Chama utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2026/27 hadi 2030/31) na unaweza kuboreshwa wakati wowote kutokana na mahitaji yaliyoko wakati huo. Maboresho husika yatapelekwa kwenye Mkutano Mkuu na kisha kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika ili kuidhinishwa. Wakati wa kufanya maboresho hayo, Chama kinaweza kuwashirikisha wadau wake wa nje.

# SURA YA TANO

# UFUATILIAJI NA TATHMINI

## 5.1 Malengo ya Ufuatiliaji na Tathmini

Katika Mpango Mkakati, Chama kitahitaji kubaini hali ya utekelezaji wa yale yaliyopangwa hivvyo kimeandaa mpango wa ufuatiliaji na tathmini. Sura hii inafafanua kuhusu namna utekelezaji wa malengo, mikakati na shughuli husika utafuatiliwa na kutathminiwa. Zoezi la ufuatiliaji litakuwa endelevu litahusisha ukusanyaji taarifa na takwimu mbalimbali ili kuiwezesha Bodi na Menejimenti kubaini mwenendo wa utekelezaji na kufanya maboresho yanayotakiwa. Tathmini zitafanyika baada ya ufuatiliaji ili kubaini mafanikio na changamoto kwa kipindi husika cha utekelezaji.

## 5.2 Ufuatiliaji

Ufuatiliaji utakuwa ni endelevu na unalenga kubaini mwenendo wa utekelezaji na mambo ya kuboresha ili kufanikisha mikakati na shabaha zilizowekwa. Zoezi hili litahusu ukusanyaji wa taarifa na takwimu za utekelezaji, kuzichambua na kuzitumia kufanya maamuzi ya Bodi na Menejimenti ikiwemo maboresho yanayotakiwa. Meneja Mkuu atahusika kufuatilia hali ya utekelezaji kila siku na kukusanya taarifa na takwimu muhimu ili kuiwezesha Bodi kufanya maamuzi na mikakati ya kuboresha utekelezaji. Pia ataongoza vikao vya kila mwezi vya watendaji kujadili hali ya utekelezaji na kufanya maboresho kwa wakati. Kwa ujumla ufuatiliaji utafanyika kwa malengo yafuatayo;

(a) Kuwezesha uandaaji ya taarifa za kiutendaji za Bodi na Menejimenti kuhusu utekelezaji wa Mpango Mkakati;
(b) Kuwapa fursa Bodi na Menejimenti kubaini mapema changamoto za utekelezaji na viashiria vya kwenda kinyume na shabaha au shughuli zilizopangwa;
(c) Kuweza kutambua kama utekelezaji unafanyika ipasavyo kuelekea kufanikisha dira, dhamira, vipaumbele na malengo ya kimkakati yaliyopangwa na Chama.
(d) Kuhakikisha kuwa malengo yaliyopangwa yanatekelezwa ndani ya muda uliopangwa; na
(e) Kuhakikisha kuwa fedha na rasilimali nyingine zinatumika vizuri na zinakuwepo kila wakati.

## 5.3 Tathmini

Tathmini zitakuwa zikifanyika ili kubaini kiwango cha utekelezaji wa malengo katika kila kipaumbele na kubaini namna shabaha na shughuli zilizopangwa na matokeo tarajiwa vimetekelezwa. Katika

Mpango Mkakati huu, Chama kitafanya tathmini za aina kuu mbili (2) yaani; tathmini za ndani na tathmini za nje. Tathmini za ndani zitafanywa na Chama kupitia Kikosi kazi (Kamati) maalum ambapo kutakuwa na angalau wajumbe watano (5) wakiwemo wajumbe wa Bodi wawili (2), Meneja Mkuu, Mtendaji mmoja (1) na Mwakilishi wa Wanachama mmoja (1). Tathmini za ndani zitafanyika katika kila kipindi cha miezi mitatu (robo mwaka). Chama kitafanya pia tathmini za jumla kila mwisho wa mwaka. Taarifa hizo zitakuwa zikitumika kufanya maamuzi mbalimbali kabla ya kuanza kipindi kingine cha utekelezaji wa Mpango Mkakati huu.

Pia Chama kitafanya tathmini za nje kwa kutumia Washauri Waelekezi (*Consultants*) ambao watakuwa na weledi na uzoefu stahiki wa kutathmini mipango ya maendeleo ya Vyama vya Ushirika. Kutakuwa na aina tatu (3) za tathmini za nje. Tathmini ya kwanza itafanyika baada ya mwaka mmoja (1) wa utekelezaji, tathmini ya pili itafanyika baada ya miaka miwili (2) hadi mitatu na ya mwisho itafanyika mwaka wa tano. Kwa ujumla, tathmini za ndani na za nje zitakazofanyika zitakuwa na malengo yafuatayo;

(i) Kuchunguza kama rasilimali zilizotengwa kwa utekelezaji zinatumika ipasavyo;
(ii) Kubaini kama hali ya utekelezaji wa Mpango Mkakati itaweza kufanikisha shughuli na shabaha zilizowekwa;
(iii) Kubaini sababu zilizowezesha kufanikiwa au kutofanikiwa kwa malengo ya kimkakati;
(iv) Kubaini changamoto mbalimbali za utekelezaji wa Mpango Mkakati na njia za utatuzi;
(v) Kujua kama malengo na shabaha husika zinafanikiwa au hapana; na
(vi) Kubaini kama rasilimali za kutosha zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji.

### 5.4 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini

Katika utekelezaji wa Mpango Mkakati huu, Bodi itaweka mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kuhakikisha kuwa malengo yake yanafikiwa. Mfumo wa ufuatiaji na tathmini utakuwa kama ifuatavyo;

(i) Kikosi kazi au Kamati ya ufuatiliaji na tathmini ya ndani itaundwa ili kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa kipindi chote cha utekelezaji;

(ii) Kamati ya ufuatiliaji na tathmini itakutana kila baada ya miezi mitatu (robo mwaka) ili kuandaa taarifa na kuiwasilisha kwa Bodi;

(iii) Meneja na watendaji watakuwa wakifanya vikao vya mara kwa mara (angalau kila mwezi) ili kutathmini hali ya utekelezaji wa Mpango Mkakati kulingana na majukumu yao;

(iv) Shughuli za kimkakati na shabaha zilizowekwa ndio vitakuwa vigezo vikuu vya kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa kila lengo la kimkakati;

(v) Bodi na Menejimenti watatumia mikakati na shabaha zilizopangwa kama kigezo cha kutengeneza mipango kazi yao ya mwaka ya utekelezaji;

(vi) Mshauri Mwelekezi atahusishwa kwa wakati uliopangwa ili kufanya tathmini huru ya nje;

(vii) Vigezo vya ufanisi vitapimwa kwa asilimia za utekelezaji na vipimo vingine vinavyothibitisha uwepo wa mabadiliko baada ya utekelezaji;

(viii) Viongozi wa Chama watahakikisha kuwa wanatekeleza majukumu yao kama yalivyooneshwa kwenye Mpango Mkakati huu na kuwasimamia ipasavyo watendaji wote; na

(ix)Meneja Mkuu atatumia jedwali lifuatalo wakati wa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mpango Mkakati huu kwa Bodi ya Chama.

**Kipaumbele Na……:**

**Lengo Na…………..:**

| Na. | Shabaha | Shughuli | Mhusika | Matokeo | Muda wa matokeo | Tofauti | Maelezo | Mapendekezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |

## 5.5 Matumizi ya Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini

Bodi na Menejimenti ya Chama watazitumia taarifa za ufuatiliaji na tathmini kutoka kwa Kamati au Mshauri Mwelekezi ili kufanya maamuzi mbalimbali. Meneja Mkuu atahakikisha taarifa za ufuatiliaji na tathmini za ndani zinaandaliwa kwa wakati na kwa ubora. Chama kinaweza pia kuwaalika wadau wake wa nje ili kujadili na kutoa maoni yao kuhusu taarifa husika za ufuatiliaji na tathmini. Bodi na Meneja Mkuu wanaweza kuandaa muundo mwingine maalumu wa kuandaa taarifa za ufuatiliaji na tathmini. Taarifa zilizoandaliwa kwa kila kipindi cha miezi mitatu (robo mwaka) zitatumika kama sehemu za ajenda za vikao vya Bodi na kutolewa maamuzi. Tarifa hizi zitawasilishwa pia katika Mkutano Mkuu kupitia Taarifa ya Bodi ili Wanachama wajue hali ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Chama na kushauri.

## SURA YA SITA

## MABADILIKO KATIKA MUUNDO WA CHAMA

### 6.1 Mahitaji ya Rasilimali Watu na Sifa Husika

Kwa lengo la kufanikisha Mpango Mkakati huu, Chama kinahitaji kuajiri pia watendaji wapya katika kada mbalimbali. Kwa miaka mitano ijayo, Chama kinahitaji jumla ya watendaji wapya ishirini na tisa (29) ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 13. Watendaji hao ni pamoja na; Afisa Utumishi (1), Dereva wa trekta 1, Dereva wa magari wa mizigo (15), Afisa Masoko Msaidizi (1), Mwanasheria (1), Afisa Ugavi na Manunuzi Msaidizi (1), Afisa TEHAMA (1), Afisa TEHAMA Msaidizi (1), Afisa Miradi, Ardhi na Majengo (1), Afisa Miradi Msaidizi (1), Afisa Usafirishaji (1), Mratibu wa Ofisi ya Kanda (3) na Mkaguzi wa Hesabu (1).

Watendaji husika kwa kuzingatia vyeo vyao, Vitengo/Idara, sifa za ajira na stahiki zao vitaoneshwa katika Muundo wa Utumishi na Sera ya Menejimenti ya Rasilimali Watu ya Chama. Bodi na Meneja Mkuu wataandaa mpango wa mafunzo kwa watendaji wapya na vikao vya maelekezo (orientation meetings) kuhusu majukumu yao kabla ya kuanza rasmi shughuli zao.

**Jedwali Na. 13: Mahitaji na Sifa za Watendaji Wapya**

| Na. | Nafasi | Idadi | Sifa za kuajiriwa | | Uzoefu wa kazi (angalau miaka…) | Atawajibika kwa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kiwango cha chini cha elimu | Maeneo ya ubobezi | | |
| 1 | Afisa Utumishi | 1 | Shahada ya Kwanza | Menejimenti ya Rasilimali Watu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Usimamizi wa Biashara, Sosholojia au taaluma nyingine zinazohusiana | 3 | Meneja Mkuu |
| 2 | Mwanasheria | 1 | Shahada ya Kwanza (na Stashahada ya Sheria kutoka Shule ya Sheria Tanzania (Law School) | Sheria | 3 | Meneja Mkuu |
| 3 | Afisa TEHAMA | 1 | Shahada ya Kwanza | TEHAMA, Sayansi ya Kompyuta, Maktaba na TEHAMA au taaluma nyingine zinazohusiana | 3 | Meneja Mkuu |
| 4 | Afisa Miradi, Ardhi na Majengo | 1 | Shahada ya Kwanza | Uchumi, Kupanga na kusimamia miradi, Menejimenti ya Mali, Uhasibu na Fedha, Uchumi wa Kilimo, Uchumi na Mipango, | 3 | Meneja Mkuu |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Uchumi na Fedha, Kilimo Biashara au taaluma nyingine zinazohusiana | | |
| 5 | Afisa Usafirishaji | 1 | Shahada ya Kwanza | Usafirishaji, Uhasibu na Fedha, Kilimo, Kilimo Biashara, Uinjinia wa magari au mitambo, Uinjia wa Kilimo au taaluma nyingine zinazohusiana. Pia awe amepata mafunzo ya udereva | 3 | Afisa Miradi, Ardhi na Majengo |
| 6 | Mratibu wa Ofisi ya Kanda | 3 | Stashahada | Uchumi, Uhasibu na Fedha, Kilimo, Kilimo Biashara, Maendeleo ya Jamii, Sosholojia, Masoko au taaluma nyingine zinazohusiana | 2 | Meneja Mkuu |
| 7 | Afisa Masoko Msaidizi | 1 | Stashahada | Masoko, Uchumi, Uhasibu na Fedha, Ujasiriamali na Masoko, Kilimo Biashara, Ujasiriamali na Usimamizi wa Biashara, Usimamizi wa Biashara au taaluma nyingine zinazohusiana | 2 | Afisa Shughuli na Masoko |
| 8 | Afisa Ugavi na Manunuzi Msaidizi | 1 | Stashahada | Ugavi na manunuzi, Usimamizi wa Stoo, Uhasibu na Fedha au taaluma nyingine zinazohusiana | 2 | Afisa Ugavi na Manunuzi |
| 9 | Afisa Miradi Msaidizi | 1 | Stashahada | Uchumi, Kupanga na kusimamia miradi, Menejimenti ya Mali, Uhasibu na Fedha, Uchumi wa Kilimo, Uchumi na Fedha, Kilimo Biashara au taaluma nyingine zinazohusiana | 2 | Afisa Miradi, Ardhi na Majengo |
| 10 | Mkaguzi wa Hesabu | 1 | Stashahada | Uhasibu na Fedha, Usimamizi wa Biashara, Benki na Fedha au taaluma nyingine zinazohusiana | 2 | Mkaguzi wa Ndani |
| 11 | Afisa TEHAMA Msaidizi | 1 | Stashahada | TEHAMA, Sayansi ya Kompyuta, Maktaba na TEHAMA au taaluma nyingine zinazohusiana | 2 | Afisa TEHAMA |
| 12 | Dereva wa trekta | 1 | Kidato cha IV | Udereva, Ufundi wa magari | 3 | Afisa Usafirishaji |
| 13 | Dereva wa magari wa mizigo | 15 | Kidato cha IV | Udereva, Ufundi wa magari | 3 | Afisa Usafirishaji |
| | **Jumla** | **29** | | | | |

## 6.2 Mapendekezo ya Idara na Vitengo

Katika kutekeleza Mpango Mkakati huu, Chama kitafanya shughuli zake kupitia Idara na Vitengo kama ifuatavyo;

(i) Ofisi ya Meneja Mkuu
(ii) Kitengo cha Sheria
(iii) Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
(iv) Kitengo cha Ugavi na Manunuzi
(v) Kitengo cha TEHAMA
(vi) Idara ya Rasilimali Watu
(vii) Idara ya Miradi, Ardhi na Majengo
(viii) Idara ya Kilimo na Masoko
(ix) Idara ya Uhasibu na Fedha

## 6.3 Mapendekezo ya Mabadiliko ya Muundo wa Chama

Kwa kuzingatia watendaji walioko na wale wapya wanaotarajia kuajiriwa na Chama, muundo wa utawala ulioko utabadilika. Mapendekezo ya muundo mpya wa utawala wa Chama yameoneshwa katika Umbo Na. 4. Chama kitaendelea kuboresha muundo huo kila wakati endapo kitaajiri watendaji zaidi ikiwemo wale watakaofanya kazi katika miradi ya kiwanda, hoteli, mashamba, maghala na miradi mingine.




**Umbo Na. 4: Mapendekezo ya Muundo Mpya wa Utawala wa LMCU Ltd**

## VIAMBATANISHO

### Kiambatanisho Na. 1: Mpango wa Utekelezaji wa Miaka Mitano (2026/27 hadi 2030/31)

**Kipaumbele Na. 1: Uanachama**

**Lengo la 1: Wanachama na wakulima wanaongezeka**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Vipimo vya shabaha | Njia za kuthibitisha | Muda | | | | | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 | |
| MK1 | Kuongeza idadi ya Wanachama katika Chama | Wanachama wanaongezeka kutoka 61 hadi 65 ifikapo 2030/31 | Idadi ya wanachama wapya | Taarifa za fedha<br>Daftari la wanachama<br>Fomu/barua ya maombi | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu |
| MK2 | Kuongeza idadi ya wakulima wanaojiunga uanachama katika AMCOS | Angalau 50% ya wakulima wanaohudumiwa na AMCOS wanajiunga uanachama ifikapo 2030/31 | Idadi ya wakulima waliojiunga | Taarifa za fedha za AMCOS<br>Madaftari ya Wanachama ya AMCOS<br>Fomu/barua ya maoni | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Shughuli na Masoko |
| | | | | | | | | | | |

**Lengo la 2: Ufanisi wa uendeshaji wa AMCOS (Wanachama) unaimarishwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Vipimo vya shabaha | Njia za kuthibitisha | Muda | | | | | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 | |
| MK1 | Kujenga uwezo wa viongozi na watendaji wa AMCOS | Viongozi na watendaji wa AMCOS wanapata mafunzo ya | Idadi ya viongozi na watendaji waliopata mafunzo | Taarifa ya mafunzo<br>Orodha ya washiriki | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kuimarisha usimamizi na uendeshaji angalau mara 1 kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu | | | | | | Afisa Utumishi |
| | | Ufanisi wa kiutendaji kwa viongozi na watendaji wa AMCOS katika kutekeleza shughuli zao (mipango kazi) unafikia angalau 70% kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Idadi ya malengo ya mwaka yaliyotekelezwa kwa kila AMCOS | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Nakala za mipango kazi ya AMOS | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK2 | Kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi muhimu katika AMCOS | Kuandaa na kuhuisha rejesta ya mahitaji ya vitendea kazi muhimu katika AMCOS kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Idadi na aina ya vitendea kazi vinavyohitajika | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Rejesta ya manunuzi<br><br>Taarifa za manunuzi<br><br>Taarifa za fedha | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Manunuzi |
| | | Vitendea kazi muhimu katika ofisi na maghala ya AMCOS vinakuwepo kwa angalau 80% ifikapo 2030/31 | Idadi na aina ya vitendea kazi vilivyonunuliwa na kusambazwa<br><br>Idadi ya maghala yaliyowekwa vitendea kazi<br><br>Idadi na majina ya AMCOS zilizopewa vitendea kazi | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Rejesta ya manunuzi<br><br>Taarifa za manunuzi<br><br>Taarifa za fedha | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Manunuzi |
| | | | | | | | | | | |

**Lengo la 3: Ushiriki wa Wanachama katika shughuli za Chama unaimarishwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Vipimo vya shabaha | Njia za kuthibitisha | Muda | | | | | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 | |
| MK1 | Kuboresha uhusiano kati ya Chama na Wanachama | Uhusiano mzuri kati ya Chama na Wanachama unaendelezwa hadi kufikia 2030/31 | Hali ya uhusiano iliyoko kati ya Chama na wanachama wake | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK2 | Kuimarisha utoaji wa taarifa muhimu kwenda kwa Wanachama na wakulima | Taarifa muhimu zinafika kwa Wanachama na Wakulima kwa wakati kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Aina ya taarifa zilizofikishwa<br>Idadi na majina ya AMCOS zilizofikishiwa taarifa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br>Nakala za barua au baruapepe | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Shughuli na Masoko<br>Afisa TEHAMA |
| MK3 | Kuendeleza utaratibu wa vikao kazi kati ya Chama na viongozi na watendaji wa AMCOS | Kila mwaka, vikao kazi kati ya Chama na viongozi na watendaji wa AMCOS vinafanyika kabla na baada ya msimu wa mazao hadi kufikia 2030/31 | Idadi ya vikao kazi vilivyofanyika<br>Idadi na majina ya washiriki wa vikao kazi | Mihtasari ya vikao kazi<br>Orodha ya washiriki<br>Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK4 | Kuweka utaratibu wa kukusanya maoni kutoka kwa wakulima ili kuboresha Chama | Mfumo imara wa kukusanya maoni ya Wanachama ya kuboresha huduma za Chama unakuwepo na kutumika hadi kufikia 2030/31 | Utaratibu wa ukusanyaji maoni uliowekwa<br>Aina na idadi ya maoni yaliyokusanywa<br>Idadi na majina ya watu waliotoa maoni | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Shughuli na Masoko<br>Afisa TEHAMA |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MK5 | Kuendeleza uanachama wa Wanachama walioko | Wanachama wote wanaendeleza uanachama wao na kushiriki kikamilifu katika Chama hadi kufikia 2030/31 | Idadi na majina ya wanachama waliondeleza uanachama wao | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Mihtasari ya mikutano mikuu | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| MK6 | Kukuza uhusiano miongoni mwa Wanachama | Ushirikiano mzuri miongoni mwa Wanachama unaendelezwa wakati wote hadi ifikapo 2030/31 | Idadi na aina ya shughuli au matukio ya ushirikiano yaliyofanyika<br><br>Idadi na majina ya AMCOS zilizoshirikiana | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK7 | Kuendeleza utaratibu wa zawadi kwa Wanachama na wakulima wanaofanya vizuri katika mambo mbalimbali (mf: uzalishaji, hisa, miradi n.k) | Mfumo wa kutoa motisha au zawadi kwa Wanachama na wakulima unaendelezwa hadi kufikia 2030/31 | Aina ya zawadi zilizotolewa<br><br>Kiasi cha fedha zilizotumika<br><br>Idadi na majina ya waliotunukiwa zawadi | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za fedha | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| | | | | | | | | | | |

**Kipaumbele Na. 2: Usimamizi wa Huduma**

**Lengo la 1: Uwezo wa Chama katika utoaji wa huduma unaimarishwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Vipimo vya shabaha | Njia za kuthibitisha | Muda | | | | | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 | |
| MK1 | Kuimarisha ufanisi wa Watendaji na viongozi wa Chama katika kutoa huduma kwa Wanachama | Viongozi na watendaji wa Chama wanapata mafunzo ya kuimarisha usimamizi na utoaji wa huduma kwa Wanachama na Wakulima angalau mara 1 kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Idadi ya viongozi na watendaji waliopata mafunzo | Taarifa ya mafunzo<br>Orodha ya washiriki<br>Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Utumishi |
| | | Ufanisi wa kiutendaji kwa viongozi na watendaji wa Chama katika kutekeleza shughuli zao (mipango kazi) unafikia angalau 90% kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Idadi ya malengo ya mwaka yaliyotekelezwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br>Mipango kazi ya mwaka | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Utumishi |
| MK2 | Kuweka mfumo endelevu wa kufuatilia na kutathmini hali ya utoaji huduma kwa Wanachama na wakulima | Ufuatiliaji na tathmini endelevu ya utoaji wa huduma inafanyika mara 2 kwa mwaka hadi ifikapo 2030/31 | Aina na idadi ya tathmini za utoaji huduma zilizofanyika<br>Idadi na majina ya AMCOS zilizofikiwa wakati wa tathmini | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br>Taarifa za tathmini | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Mkaguzi wa Ndani |
| MK3 | Kutenga rasilimali za kutosha kuimarisha utoaji wa huduma | Angalau 95% ya fedha zinazohitajika kutoa huduma kwa | Kiasi ch fedha zilizotengwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | kwa Wanachama na Wakulima | Wanachama na Wakulima zinakuwepo kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | | Taarifa za fedha | | | | | | Mhasibu Mkuu |
| | | Angalau 80% ya watendaji wanaohitajika katika kutoa huduma kwa Wanachama na Wakulima wanakuwepo hadi kufikia 2030/31 | Idadi ya watendaji walioko na kada zao | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Matangazo ya ajira<br><br>Taarifa za utumishi | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Utumishi |
| MK4 | Kuendeleza uhusiano mzuri na watoa huduma wa Chama na Wanachama | Uhusiano mzuri kati ya Chama na watoa huduma unakuwepo wakati wote na kuimarishwa hadi kufikia 2030/31 | Hali ya uhusiano wa Chama na watoa huduma | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| | | | | | | | | | | |

**Lengo la 2: Upatikanaji wa huduma za msingi kwa Wanachama na Wakulima unaongezeka**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Vipimo vya shabaha | Njia za kuthibitisha | Muda | | | | | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 | |
| MK1 | Kuratibu upatikanaji wa viuatilifu kwa wakati | Angalau 60% ya mahitaji ya viuatilifu (pembejeo) kwa Wanachama na wakulima yanafikiwa kila mwaka hadi ifikapo 2030/31 | Aina na kiasi cha viutatilifu vilivyonunuliwa na kusambazwa<br><br>Idadi na majina ya AMCOS na wakulima waliopata | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji<br><br>Taarifa za manunuzi | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko<br><br>Afisa Manunuzi |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | viuatilifu | | | | | | | |
| MK2 | Kuratibu upatikanaji wa vifungashio kwa wakati | Angalau 95% ya mahitaji ya vifungashio (magunia na viroba) kwa wanachama na wakulima yanafikiwa kila mwaka hadi ifikapo 2030/31 | Idadi na aina ya vifungashio vilivyonunuliwa na kusambazwa<br><br>Idadi na majina ya AMCOS na wakulima waliopata vifungashio | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji<br><br>Taarifa za manunuzi | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko<br><br>Afisa Manunuzi |
| MK3 | Kuratibu huduma za huduma za mashine za kupulizia madawa shambani kwa wakati | Angalau 50% ya mahitaji ya mashine za kupulizia madawa mashambani yanafikiwa kila mwaka hadi ifikapo 2030/31 | Idadi na aina ya mashine zilizonunuliwa na kusambazwa<br><br>Idadi na majina ya AMCOS na wakulima waliopewa mashine | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji<br><br>Taarifa za manunuzi | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko<br><br>Afisa Manunuzi |
| MK4 | Kuratibu upatikanaji wa mizani ya kidijitali kwa wakati | Angalau mizani mpya 150 ya kidijitali inanunuliwa na kusambazwa kwa Wanachama kabla ya 2030/31 | Idadi ya mizani ya kidigitali iliyonunuliwa na kusambazwa<br><br>Idadi na majina ya AMCOS zilizopewa mizani husika | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji<br><br>Taarifa za manunuzi | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko<br><br>Afisa Manunuzi |
| MK5 | Kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wakulima | Angalau 60% ya wakulima katika AMCOS wanapata huduma ya bima ya afya ifikapo 2030/31 | Idadi na majina ya wakulima waliopata huduma za bima za afya | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Orodha ya wakulima waliojiunga na bima ya afya<br><br>Kadi za bima ya afya | | | | | | Wanachama<br><br>Bodi<br><br>Meneja Mkuu |
| MK6 | Kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha | SACCOS ya Wanachama inaanzishwa kabla ya | Uwepo wa SACOS | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu | | | | | | Wanachama<br><br>Bodi |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | kwa Wanachama na Wakulima | Mei 2027 na kuhudumia Wanachama | | Cheti cha usajili wa SACCOS<br>Ofisi ya SACCOS na watendaji walioajiriwa | | | | | | Meneja Mkuu |
| | | Angalau 80% ya mahitaji ya kifedha ya Wanachama yanafikiwa kupitia SACCOS ya Chama na mabenki kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Idadi na majina ya AMCOS zilizopata huduma za mikopo | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu |
| | | Angalau 60% ya mahitaji ya mikopo kwa wakulima yanafikiwa kila mwaka hadi ifikapo 2030/31 | Idadi na majina ya wakulima waliopata huduma za mikopo | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu | | | | | | Wanachama<br>Bodi<br>Meneja Mkuu |
| MK7 | Kuwezesha malipo ya wakulima na Wanachama kwa wakati | Kila mwaka, angalau 97% ya wakulima na Wanachama wanalipwa kwa wakati kila msimu wa minada hadi ifikapo 2030/31 | Idadi na majina ya wakulima na wanachama waliolipwa<br>Muda ulitumika kukamalisha malipo | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br>Taarifa za fedha | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Mhasibu Mkuu |
| | | Kabla ya 2030/31, Ofisi 3 za Kanda zinajengwa ili kurahisisha malipo ya wakulima na utoaji wa huduma nyingine | Idadi ya ofisi zilizojengwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br>Taarifa za fedha<br>Taarifa za zabuni ya ujenzi<br>Taarifa za manunuzi<br>Majengo ya ofisi | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Miradi, Ardhi na Majengo<br>Afisa Manunuzi |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MK8 | Kuongeza uwezo katika kuhifadhi mazao ya Wanachama na wakulima | Maghala ya Chama na Wanachama yanakuwa na hali nzuri wakati wote kuwezesha uhifadhi salama wa mazao ya wakulima hadi kufikia 2030/31 | Hali ya maghala ya Chama na wanachama | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za hali ya majengo | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Miradi, Ardhi na Majengo |
| | | Ukarabati wa ghala kuu la Ilulu Mtama DC unafanyika kabla ya 2030/31 | Shughuli za ukarabati wa ghala zilizofanyika | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za fedha<br><br>Taarifa za zabuni ya ukarabati<br><br>Taarifa za manunuzi<br><br>Ghala lililokarabatiwa | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Miradi, Ardhi na Majengo<br><br>Afisa Manunuzi |
| MK9 | Kuwezesha upatikanaji wa zana na teknolojia rafiki za kilimo kwa Wanachama na wakulima | Uratibu wa upatikanaji na usambazaji wa zana na teknolojia za kilimo kwa Wanachama na wakulima unafanyika kila inapohitajika hadi kufikia 2030/31 | Aina ya zana na teknolojia za kilimo zilizowafikia wanachama na Wakulima<br><br>Idadi na majina ya wanachama na wakulima waliofikiwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| | | | | | | | | | | |

**Kipaumbele Na. 3: Uzalishaji na Ubora wa Mazao ya Kibiashara**

## Lengo la 1: Uzalishaji na ukusanyaji wa korosho unaongezeka

| Na. | Mikakati | Shabaha | Vipimo vya shabaha | Njia za kuthibitisha | Muda | | | | | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 | |
| MK1 | Kuratibu uzalishaji na uoteshaji wa miche bora ya korosho | Angalau miche bora ya korosho 100,000 inazalishwa na kuoteshwa kwa kila mwaka hadi 2030/31 | Idadi ya miche ya korosho iliyozalishwa na kusambazwa<br>Idadi ya Wakulima na wanachama waliopata miche<br>Ukubwa wa ardhi iliyooteshwa korosho | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br>Taarifa za uzalishaji | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Shughuli na Masoko<br>Afisa Manunuzi |
| MK2 | Kuratibu uboreshaji wa mikorosho ya zamani isiyozaa vizuri katika mashamba ya Wakulima | Angalau 50% ya mikorosho ya zamani katika mashamba ya wakulima inaboreshwa hadi kufikia 2030/31 | Idadi ya mikorosho iliyoboreshwa<br>Ekari za mashamba zilizoboreshwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br>Taarifa za uzalishaji | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK3 | Kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima | Ufanisi katika utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima wa korosho unafikia angalau 50% ya wakulima kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Idadi ya wakulima waliohudumiwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br>Taarifa za uzalishaji | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK5 | Kuongeza ukubwa wa mashamba yanayolimwa | Mashamba mapya yanayolimwa korosho yanaongezeka kwa angalau 20% kufikia | Idadi ya mashamba mapya ya korosho yaliyoanzishwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br>Taarifa za uzalishaji | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | korosho katika eneo la Chama | 2030/31 | | | | | | | | Afisa Shughuli na Masoko |
| MK6 | Kuongeza makusanyo ya korosho kutoka kwa Wanachama na wakulima | Makusanyo ya korosho ghafi yanaongezeka kutoka tani 43,000 hadi angalau tani 80,000 ifikapo 2030/31 | Kiasi cha korosho zilizozalishwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji<br><br>Taarifa za masoko | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK7 | Kuongeza tija ya uzalishaji wa korosho katika mashamba ya wakulima | Uzalishaji kwa kila mkorosho unafikia angalau kilo 50 kwa mwaka hadi kufika 2030/31 | Wastani wa uzalishaji kwa kila mkorosho | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| | | | | | | | | | | |

**Lengo la 2: Uzalishaji na ukusanyaji wa ufuta, mbaazi, alizeti na choroko unaongezeka**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Vipimo vya shabaha | Njia za kuthibitisha | Muda | | | | | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 | |
| MK1 | Kuongeza matumizi ya mbegu bora za ufuta, mbaazi, choroko na alizeti miongoni mwa wakulima | Angalau 50% ya wakulima wanatumia mbegu bora za mazao kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Idadi ya Wakulima wanaotumia mbegu bora<br><br>Kiasi cha mbegu bora kilichosambazwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK2 | Kuwezesha upatikanaji wa huduma za ugani kwa wakulima | Angalau 50% ya wakulima wanapata huduma za uhakika za ugani kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Idadi ya wakulima waliohudumiwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK3 | Kuongeza ukubwa | Mashamba mapya | Idadi ya mashamba | Taarifa za utendaji za | | | | | | Bodi |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | wa mashamba yanayolimwa ufuta, mbaazi, alizeti na choroko katika eneo la Chama | yanayolimwa ufuta, mbaazi, alizeti na choroko yanaongezeka kwa angalau 10% kufikia 2030/31 | mapya ya ufuta, mbaazi, alizeti na choroko yaliyoanzishwa | Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji | | | | | | Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK4 | Kuongeza makusanyo ya ufuta, mbaazi, alizeti na choroko kutoka kwa Wanachama na Wakulima | Kuongeza makusanyo ya ufuta kutoka tani 52,000 hadi tani 100,000 ifikapo 2030/31 | Kiasi cha ufuta uliozalishwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji<br><br>Taarifa za masoko | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| | | Kuongeza makusanyo ya mbaazi kutoka tani 3,000 hadi tani 10,000 ifikapo 2030/31 | Kiasi cha mbaazi zilizozalishwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji<br><br>Taarifa za masoko | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| | | Kufikisha angalau makusanyo ya tani 10,000 za choroko ifikapo 2030/31 | Kiasi cha choroko zilizozalishwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji<br><br>Taarifa za masoko | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| | | Kufikisha angalau makusanyo ya tani 10,000 za alizeti ifikapo 2030/31 | Kiasi cha alizeti iliyozalishwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji<br><br>Taarifa za masoko | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK5 | Kuongeza tija ya uzalishaji wa ufuta, mbaazi, alizeti na choroko katika mashamba ya wakulima | Uzalishaji wa ufuta kwa kila ekari moja (1) ya mkulima unaongezeka kutoka kilo 300 hadi 500 ifikapo 2030/31 | Wastani wa kiasi cha ufuta uliozalishwa kwa ekari | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji<br><br>Taarifa za masoko | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| | | Uzalishaji wa mbaazi | Wastani wa kiasi cha mbaazi zilizozalishwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu | | | | | | Bodi |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kwa kila ekari moja (1) ya mkulima unaongezeka kutoka kilo 500 hadi 800 ifikapo 2030/31 | kwa ekari | Taarifa za uzalishaji<br><br>Taarifa za masoko | | | | | | Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| | | Uzalishaji wa choroko kwa kila ekari moja (1) ya mkulima unaongezeka kutoka kilo 300 hadi 400 ifikapo 2030/31 | Wastani wa kiasi cha choroko zilizozalishwa kwa ekari | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji<br><br>Taarifa za masoko | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| | | Uzalishaji wa alizeti kwa kila ekari moja (1) ya mkulima unafikia angalau magunia 5 kufikia 2030/31 | Wastani wa kiasi cha alizeti iliyozalishwa kwa ekari | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za uzalishaji<br><br>Taarifa za masoko | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| | | | | | | | | | | |

**Lengo la 3: Ubora wa mazao yanayozalishwa unaimarishwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Vipimo vya shabaha | Njia za kuthibitisha | Muda | | | | | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **2026/27** | **2027/28** | **2028/29** | **2029/30** | **2030/31** | |
| MK1 | Kuimarisha usimamizi wa ubora wa mazao miongoni mwa Wanachama na wakulima kabla ya kufika maghala makuu | Angalau 97% ya korosho inayokusanywa inakuwa na ubora wa daraja la kwanza (grade A) kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | Kiasi cha Korosho kwa kila daraja la ubora | Taarifa za masoko<br><br>Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| | | Wakulima na Wanachama | Hali ya ubora wa mazao | Taarifa za masoko | | | | | | Bodi |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | wanazingatia ubora wa ufuta, mbaazi, alizeti na choroko kwa angalau 90% hadi kufikia 2030/31 | yaliyokusanywa na kuuzwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu | | | | | | Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK2 | Kuratibu upatikanaji wa vifaa vya kutunzia mazao na kupima ubora kwa Wanachama | Mahitaji ya Wanachama ya vifaa vya kupimia ubora yanafikiwa kwa angalau 95% kila msimu wa mauzo hadi kufikia 2030/31 | Idadi na aina ya vifaa vya kupimia ubora vilivyonunuliwa na kusambazwa<br><br>Idadi na majina ya AMCOS ilizopewa vifaa husika | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za manunuzi<br><br>Taarifa za fedha | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Manunuzi<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK3 | Kuimarisha usimamizi wa ubora wa mazao ya wakulima katika maghala makuu | Hadi kufikia 2030/31 angalau 97% ya mazao ya kibiashara yaliyoko maghala makuu yanabaki na ubora stahiki hadi yanapouzwa kwa kila msimu | Kiwango cha ubora wa mazao yaliyouzwa | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za masoko | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| | | | | | | | | | | |

**Kipaumbele Na. 4: Masoko na uhusiano na wadau**

## Lengo la 1: Masoko yenye uhakika kwa mazao ya kibiashara yanakuwepo

| Na. | Mikakati | Shabaha | Vipimo vya shabaha | Njia za kuthibitisha | Muda | | | | | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 | |
| MK1 | Kuendeleza uuzaji wa mazao kwenye masoko yaliyoko | Uuzaji wa mazao ya kibiashara katika masoko yaliyoko unaendelezwa kila msimu wa mauzo hadi kufikia 2030/31 | Kiasi na aina ya mazao yaliyouzwa katika masoko yaliyoko | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br>Taarifa za masoko | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK2 | Kuratibu ununuzi wa choroko na alizeti kupitia Chama | Mfumo wa rasmi wa uuzaji alizeti na choroko kutoka kwa wakulima unakuwepo kuanzia 2026/27 na kuendelezwa | Uwepo wa mfumo wa uuzaji wa alizeti na choroko | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br>Taarifa za masoko | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK3 | Kutafiti masoko mapya ya mazao ya kibiashara | Masoko mapya ya uhakika kwa mazao ya kibiashara ya wakulima na Wanachama yanapatikana hadi kufikia 2030/31 | Masoko mapya yaliyopatikana | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br>Taarifa za masoko<br>Majina na idadi ya wanunuzi wa mazao husika | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK4 | Kuimarisha ushiriki wa Wanachama katika shughuli za masoko | Kila msimu wa minada, viongozi na watendaji wa AMCOS wanashiriki kikamilifu katika shughuli za masoko ya mazao hadi kufikia 2030/31 | Idadi na majina ya viongozi na watendaji wa AMCOS walioshiriki kila mnada | Taarifa za masoko<br>Orodha ya washiriki wa minada kutoka kwenye AMCOS<br>Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK5 | Kudhibiti uuzaji wa | Angalau 95% ya mazao | Kiasi cha mazao | Taarifa za utendaji za | | | | | | Bodi |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | mazao ya kibiashara katika masoko yasiyo rasmi | ya wakulima yanakusanywa na AMCOS na kuuzwa kupitia Chama kila mwaka hadi kufikia 2030/31 | yaliyokusanywa na kuuzwa | Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za masoko | | | | | | Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| | | | | | | | | | | |

**Lengo la 2: Uhusiano mzuri kati ya Chama na Wadau wake unaimarishwa na kuendelezwa**

| Na. | Mikakati | Shabaha | Vipimo vya shabaha | Njia za kuthibitisha | Muda | | | | | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 | |
| MK1 | Kuimarisha na kuendeleza uhusiano na wadau wa sasa wa Chama | Uhusiano wa Chama na wadau wa sasa unaimarishwa na kuendelezwa hadi kufikia 2030/31 | Hali ya uhusiano wa Chama na wadau walioko<br><br>Idadi na majina ya wadau walioko<br><br>Matukio/shughuli za ushirikiano zilizofanyika | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za masoko | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK2 | Kuanzisha na kuendeleza uhusiano na wadau wapya wa Chama | Mahusiano kati ya Chama na wadau wapya yanaanzishwa na kuendelezwa hadi kufikia 2030/31 | Hali ya uhusiano wa Chama na wadau wapya<br><br>Idadi na majina ya wadau wapya<br><br>Matukio/shughuli za ushirikiano zilizofanyika | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br><br>Taarifa za masoko | | | | | | Bodi<br><br>Meneja Mkuu<br><br>Afisa Shughuli na Masoko |
| MK3 | Kuimarisha Idara ya masoko ili | Muundo na majukumu ya Kitengo cha Masoko | Maboresho ya Idara yaliyofanyika | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu | | | | | | Bodi |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | kushughulikia mahusiano na wadau na huduma kwa wateja | vinaboreshwa kabla ya Mei 2027 | | Taarifa za masoko | | | | | | Meneja Mkuu<br>Afisa Shughuli na Masoko |
| | | | | | | | | | | |

## Lengo la 3: Kufahamaika kwa Chama miongoni mwa wadau kunaongezeka

| Na. | Mikakati | Shabaha | Vipimo vya shabaha | Njia za kuthibitisha | Muda | | | | | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 | |
| MK1 | Kuongeza kufahamika kwa Chama miongoni mwa wadau wa ndani ya Nchi | Kufahamika kwa Chama miongoni mwa wadau mbalimbali nchini kunaongezeka zaidi ifikapo 2030/31 | Idadi ya matangozao yaliyoandaliwa na kusambazwa nchini<br>Majina na idadi ya vyombo vya habari na mitandao ya kijamii iliyotumika kutangaza shughuli za Chama nchini<br>Idadi ya matukio au shughuli ambazo Chama kimehudhuria au kudhamini nchini | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br>Nakala za matangazo<br>Taarifa za masoko | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Shughuli za Masoko<br>Afisa TEHAMA |
| MK2 | Kuongeza kufahamika kwa Chama miongoni mwa wadau wa nje ya Nchi | Kufahamika kwa Chama miongoni mwa wadau wa nje ya nchi kunaongezeka zaidi ifikapo 2030/31 | Idadi ya matangozao yaliyoandaliwa na kusambazwa<br>Majina na idadi ya vyombo vya habari na mitandao ya kijamii iliyotumika kutangaza shughuli | Taarifa za utendaji za Bodi na Meneja Mkuu<br>Nakala za matangazo<br>Taarifa za masoko | | | | | | Bodi<br>Meneja Mkuu<br>Afisa Shughuli na Masoko<br>Afisa TEHAMA |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | za Chama kimataifa<br>Idadi ya matukio au shughuli ambazo Chama kimehudhuria au kudhamini nje ya nchi | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |

**Kipaumbele Na. 5: Usimamizi endelevu wa miradi na uwekezaji**

## Lengo la 1: Uwekezaji wa hisa katika taasisi za kibiashara unaongezeka na kufuatiliwa

| Na. | Mikakati | Shabaha | Vipimo vya shabaha | Njia za kuthibitisha | Muda | | | | | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2030/31 | |
